# Nipashe

Alhamisi Februari 13, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580153

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Fidia inavyouweka njia panda uchimbaji wa graphite Ulanga


UKURASA 4


ama
ALHAMISI FEBRUARI 13, 2020
AFYA NA MAZINGIRA
Ukurasa 20
SIKU YA UKEKETAJI
Yanayojificha yaibuliwa upya hadharani
LINI CORONA ITAKOMA?
Ukurasa 19
Rais Trump, wataalamu dunia kila mmoja anabashiri lake
Ukurasa 14
KAMPENI TUMEBORESHA AFYA
TMDA yatamba ufanisi wa 90%
Balozi wa China: Uamuzi wa busara wanafunzi Watanzania kubaki Wuhan

UKURASA 13

# Hatima kina Membe, Kinana CCM siku saba

• **Kamati** Kuu yaagiza timu ya Mangula kuwasilisha taarifa kuhusu walivyohojiwa... *Endelea ukurasa 2*


YUSUF MAKAMBA


BENARD MEMBE


ABDULRAHMAN KINANA


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**TMA YATAJA CHANZO CHA JOTO KALI NCHINI**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema hali ya joto kali...

UKURASA WA 25

**KENYATTA, RAILA WANENA MAZITO MAZIKO YA MOI**

RAIS wa awamu ya pili wa Kenya hayati Daniel arap Moi, alizikwa hii...


## Idadi vifo vya corona sasa 1,113

UKURASA 3



## Muuguzi cheti feki mbaroni tuhuma za kuua mwanafunzi akimtoa mimba

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store



**MICHEZO** KOCHA AZAM ADAI MOJA MOJA SI HABA UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# TMA yataja chanzo cha joto kali

Na Faustine Feliciane

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imesema hali ya joto kali katika baadhi ya mikoa nchini imetokana na jua la utosi kuwa katika maeneo ya nchi.

Kwa siku tatu kuanzia Februari 9 hadi juzi, mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Morogoro na Tanga, kulitokea joto kali na kusababaisha adha kwa baadhi ya watu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alisema kumekuwa na vipindi vya jua kali la usawa wa utosi linalozunguka na kwa sasa kipindi cha jua hilo lipo katika maeneo ya nchi.

"Hali hii ndiyo imesababisha kwa siku tatu mfululizo kuwa na joto kali kwa baadhi ya mikoa yetu," alisema Dk. Kijazi.

Alisema hali hiyo si endelevu na pindi hali ya joto inapokuwa kubwa hutengeneza unyevunyevu angani na kutengeneza vipindi vya mvua.

Dk. Kijazi alisema kwa siku hizo, mikoa wa Dar es Salaam ulikuwa na joto kuanzia nyuzi joto 33.3 mpaka 33.9 kwa kipimo cha sentigredi na wastani wake ukiwa ni sentigredi 32.6 huku kwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro nyuzijoto ikifikia sentigredi 34.2.

Kijazi pia alisema kwa mkoa wa Tanga nyuzijoto ilikuwa juu mpaka kufikia sentigredi 36.

"Hatutegemei hali hii kuwa ya kudumu na kama mnaona kwa leo (jana) hali imebadilika, joto limepoa," alisema.

Katika hatua nyingine, TMA leo inatarajia kutoa utabiri wa mvua za masika zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni kwa baadhi ya maeneo ya mikoa na imewataka wananchi kufuatilia taarifa hizo kupitia vyombo vya habari.

**NINI JUA LA UTOSI?**

Machi 21, kila mwaka, inaaminika kuwa ni siku ambayo jua linapita sawia na mstari wa kubuni wa kijiografia wa Ikweta. Siku hiyo huitwa kitaalamu 'Siku ya Jua la Utosi'.

Tukio hilo la kipekee ambalo kijiogrofia huitwa 'Equinox', hutokea mara mbili kwa kila mwaka, yaani Machi 21 na Septemba 23. Katika siku hizo au zinazokaribiana na tarehe hiyo, maeneo husika, Tanzania ikiwamo, hukumbwa na joto kali kama ambavyo ilitokea katika siku tatu zilizopita.

Licha ya kuwa katika Ikweta nyakati hizo, jua pia huwa katika Tropiki ya Kansa (Kizio cha Kaskazini) Juni 21 na Tropiki ya Kaprikoni (Kizio cha Kusini), Desemba 22.

# Membe, Makamba, Kinana wawekwa kiporo siku saba

Na Mary Geofrey

HATIMA ya vigogo wa tatu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Makatibu Wakuu wastaafu, Yusuf Makamba, Abdulrahman Kinana na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, imewekwa kiporo kwa siku saba.

Kamati Kuu imetoa siku saba kwa Kamati Ndogo ya Udhibiti na Nidhamu kukamilisha taarifa inayowahusu makada hao watatu na kuiwasilisha katika vikao husika.

Taarifa iliyotolewa jana baada ya kikao cha Kamati Kuu kilichoongozwa na Mwenyekiti wake, Rais John Magufuli ilikaa jana jijini Dar es Salaam, ilieleza kuwa hatma ya vigogo itajulikana baada ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Philip Mangula, kuwasilisha taarifa zao ndani ya siku saba.

Katika taarifa hiyo iliyotolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Halmashauri Kuu ya Taifa CCM (HKT), Humphrey Polepole, ilieleza kuwa kamati kuu iliazimia kuwa taarifa zao ziwasilishwe katika vikao husika.

"Kamati Kuu imetoa siku saba kwa Kamati Ndogo ya Udhibiti na Nidhamu kukamilisha taarifa inayowahusu wanachama hawa watatu na kuiwasilisha katika vikao husika," alisema Polepole.

Alisema kamati hiyo ilipokea taarifa ya awali kutoka kwa Kamati ya Usalama na Maadili juu ya Utekelezaji wa Azimio la HKT katika kikao chake cha Desemba mwaka jana jijini Mwanza, kuhusu kuwaita na kuwahoji wanachama hao.

Vigogo hao waliitwa mbele ya Kamati ya Maadili ya baada ya sauti zao kusambaa katika mitandao ya kijamii.

Viongozi hao wastaafu walikuwa wakielezea namna CCM inavyopoteza mvuto, uendeshaji wa nchi na jinsi chama kilivyoshindwa kuwalinda makatibu hao dhidi ya mtu anayewachafua.

Jumatatu wiki hii, Makamba na Kinana walifika katika Ofisi Ndogo za CCM Lumumba kwa ajili ya kuitikia wito huo.

Alhamisi iliyopita, Membe alifika mbele ya kamati hiyo yenye wajumbe wanne katika Ofisi za

INAENDELEA UK. 8




Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Rais John Pombe Magufuli, akiongoza Kikao cha Kamati Kuu ya CCM, katika Ofisi Ndogo za chama hicho, Mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Muuguzi vyeti feki mbaroni tuhuma kuua mwanafunzi akimtoa mimba

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera, linamshikilia Dezber Kahwa (49), mkazi wa Kijiji cha Kibengwe, Bukoba Vijijini, kwa tuhuma za kusababisha kifo cha Alinda Leverian (14), mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Kilima, kwa kumtoa mimba kienyeji.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alidai jana kuwa tukio hilo lilitokea Februari 8 mwaka huu nyumbani kwa Vedastina Cleophace baada ya Kahwa kujaribu kumtoa mimba mwanafunzi huyo.

Alidai kuwa Kahwa aliwahi kuwa muuguzi katika Zahanati ya Buzi, lakini alifukuzwa kazi na serikali wakati wa uhakikiwa wa watumishi hewa na wenye vyeti feki kutokana na kutokuwa na cheti cha kidato cha nne.

"Mtuhumiwa huyo alikuwa hana cheti cha kidato cha nne, ulipofanyika uhakiki wa watumishi hewa, akafukuzwa kazi na serikali lakini akaendelea kuhudumia wagonjwa mtaani bila kibali na kwa kificho, na wakati mwingine alifanyia shughuli hizo nyumbani kwake," alidai.

Kamanda Malimi alidai kuwa baada ya jaribio hilo, binti huyo alipata maumivu ya tumbo na kwenda nyumbani kwa mtuhumiwa, ambako inadaiwa alipatiwa matibabu ya maumivu ya tumbo, kitendo ambacho ndugu na jamaa wanahisi ndiyo sababu ya kifo chake.

"Mtuhumiwa amekamatwa na anaendelea kuhojiwa na polisi, lakini tayari mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi na daktari wa binadamu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera na uchunguzi wa awali umebaini chanzo ni kutobolewa kwa mfuko wa uzazi na kuingizwa dawa sumu," alidai.

Katika tukio lingine lililotokea Februari 9 mwaka huu majira ya saa tano usiku katika Mtaa wa Rwazi, Kata ya Kahororo, Manispaa ya Bukoba, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kahororo, Buberwa Mberwa (14), alifariki dunia baada ya kudaiwa kujinyonga kwa kutumia mkanda aliokuwa akiutumia kufungia suruali.

"Alikutwa amejitundika kwa mkanda ambao alikuwa akiutumia kufungia suruali, aliufunga katika nondo ya dirisha, katika nyumba hiyo alikuwa akiishi na mama yake pekee, baada ya baba yake kuwatelekeza na kusababisha hali yao ya maisha kuwa ngumu," Kamanda Malimi alidai. Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alidai taarifa kutoka eneo la tukio zilidai kuwa, kabla ya tukio hilo, majira ya saa 12 jioni, mwanafunzi huyo aliporejea nyumbani, aliwakuta watoto wa baba yake mdogo ambao ni pacha; Kakuru Laurent (8) na Kato Laurent (8), wanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Kahororo, wakichezea mkanda huo, na kuwa aliwataka wampe mkanda wake wakamkatalia.

"Lakini walipomwona kachukia, waliamua kumpa mkanda wake na kuondoka kwenda kwao na baadaye ndipo ikabainika kuwa amejinyonga," alidai.

Kwa mujibu wa Kamanda Malimi, mwanafunzi huyo aliwahi kuwa na tatizo la afya ya akili.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera Charles (kulia), akishuhudia watendaji waliokuwa wakifanya mazoezi ya kujifunza namna ya kutumia mashine za BVR (Biometric Voters Registration Kit), alipotembelea kukagua mafunzo ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kwa maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: NEC**

# Idadi vifo corona sasa yafikia 1,113

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya waliofariki kwa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona imefikia 1,113, huku watu 38,800 wakiendelea na matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ubalozi wa China nchini, hadi Februari 11, mwaka huu, China kulikuwa na watu 44,653 waliothibitika kuugua ugonjwa huo na kati yao 4,740 walipona na kuruhusiwa.

Hadi Februari 11, mwaka huu, watu 16,067 walikuwa wanasubiri majibu ya vipimo.

Pia kufikia Februari 11 raia wa kigeni 27 kwa pamoja nchini China walithibitishwa kuambukizwa virusi vipya vya corona na hakuna Mtanzania.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kati ya kesi 27 zilizothibitishwa, saba wamepona na wameruhusiwa kutoka hospitalini, wawili wamekufa akiwamo raia wa Marekani mmoja ni raia wa Japan na 18 wanapata matibabu katika eneo maalumu.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa nje ya Hubei idadi ilipungua na kufikia 377 ikiwa ni siku ya nane mfululizo, huku idadi mpya katika mji ikipungua na kufikia chini ya 2,000 kwa mara ya kwanza.

Kadhalika taarifa hiyo, ilieleza kuwa kuna ongezeko la viwango vya uponaji nchini kote katika mji wa Wuhan, Hubei na China kwa ujumla kwa kuwa vilipanda hadi kufikia asilimia 6.2, 6.1 na 8.2 ikilinganishwa na asilimia 2.6, 1.7 na 1.3 mnamo Januari 27.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), Dk. Tedros Ghebreyesus, alikaririwa akisema asilimia 99 ya kesi za ugonjwa wa virusi vya corona (COVID-19) ziko China na asilimia 97 ya vifo ni katika Jimbo la Hubei.

Katika mkutano wa 146 wa Bodi Kuu ya Wakurugenzi ya WHO alipongeza mkakati wa China katika kupambana na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Dk. Ghebryesus, mkakati wa China ni kuchukua hatua kali katika eneo kuu, chanzo, ili kulinda watu wa China na kuzuia kuenea kwa virusi hivyo katika nchi nyingine.

"Kama isingekuwa juhudi za China, idadi ya kesi zilizo nje ya China zingekuwa kubwa zaidi," alisisitiza Dk. Tedros.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa, timu ya awali ya wataalamu wa kimataifa inayoongozwa na WHO imewasili nchini China na kwamba watabadilishana kwa kina na wenzao wa China kuhusu hali hiyo na pia kuzuia na kudhibiti janga.

**BALOZI WA TANZANIA**

Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, anawasiliana kwa karibuni na wanafunzi wa Tanzania walioko Wuhan. "Tunarudia ushauri wa Balozi kwamba njia salama kabisa iliyopendekezwa na WHO ni kukaa Wuhan, epuka kukusanyika na fuata kanuni za usafi. Mamlaka na vyuo vikuu huko Wuhan vitaendelea kuwajali na kutoa msaada kwa wanafunzi wa Tanzania na wa nchi nyingine," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Ndege kufundishia marubani kutua Okt.

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kinatarajia kupokea ndege mbili aina ya Cessna 172 Oktoba, mwaka huu, kwa ajili ya kufundishia masomo ya urubani.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salam alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati wa ziara ya wajumbe wa Baraza la Uongozi wa NIT maeneo ya chuo.

Prof. Mganilwa alisema mandalizi kwa ajili ya kuanza kufundishia mafunzo hayo kama vile madarasa na walimu, yameshakamilika na kinachosubiriwa ni ujio wa ndege hizo.

"Hizo ndege tunatarajia kuzipokea kuanzia kipindi cha Oktoba hadi Novemba, mwaka huu. Tutapokea ndege mbili mpya kwa ajili ya mafunzo na ni ndege aina ya Cessna 172 zitakazotoka Marekani zenye uwezo wa kuchukua abiria wanne," alisema Prof. Mganilwa.

Alisema kwa sasa NIT ina vifaa vya kufundishia wahandisi

INAENDELEA UK. 8

# ATCL yatangazia neema wafanyabiashara

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL), limesema linatarajia kuwasafirisha wafanyabiashara wazawa kwenda India kushiriki mkutano wa pamoja na wawekezaji wa nchini humo, ili wakaangalie fursa ya masoko ya kusafirisha bidhaa zaidi.

Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa ATCL, Josephat Kagirwa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akielezea safari hiyo ambayo itahusisha ndege yenye uwezo wa kubeba abiria 262.

"Safari hii inatarajia kufanyika Machi 4, mwaka huu na ni ya wafanyabiashara na wasio wafanyabiashara ambao watakwenda Mumbai, India ili kukutana na wafanyabiashara wa India," alisema na kuongeza:

"Wanatarajia kurejea nchini Machi 7 baada ya mkutano huu unaotarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Machi 5."

Kagirwa alisema gharama za ushiriki mkutano huo pamoja na tiketi ni kati ya Dola za Marekani 500 (sawa na Sh. milioni 1.1) na 700 (sawa na Sh. milioni 1.6).

"Ukichagua ushiriki wa Dola za Marekani 500 itajumuisha tiketi ya kwenda na kurudi, ushiriki na wale watakaochagua ushiriki wa Dola za Marekani 700 hii itajumuisha tiketi ya kwenda na kurudi, ushiriki na malazi.

"Fursa zitakazokuwepo huko ni mfanyabiashara kufahamu fursa za kibiashara kati ya nchi hizi mbili, kupata uelewa wa usafirishaji bidhaa, kupata wabia sahihi wa kufanya nao biashara na kutembelea masoko yanayopokea bidhaa India," alisema.

Pia alisema ATCL imeanza na India na baadaye inatarajia kufanya hivyo kupitia vituo vingine duniani ambako ndege zake zinakwenda lengo likiwa kupanua wigo mpana wa kibiashara.

"Awali, safari za India tulikuwa tunazifanya kwa wiki mara tatu lakini sasa wameziongeza na kufikia nne. Bidhaa nyingi zinatoka India kuja Tanzania, tunataka na sisi tupeleke nyingi kwenye masoko yao ndiyo maana ya safari hii ya wafanyabiashara," alisema.

Alisema watu wengine ambao si wafanyabiashara lakini wanapenda kwenda nchini humo kuangalia fursa nao wanakaribishwa kushiriki.

"Tumefanya maandalizi India na siku ambazo watakuwa huko watakutana na wafanyabiashara wenzao wa India kubadilishana mawazo na kutafuta fursa," alisema.


## TANGAZO KWA UMMA

Kwa niaba ya mteja wetu **TANZANIA ZHONFA CONSTRUCTION MATERIAL GROUP COMPANY LTD,** sisi kampuni ya uwakili ya **DAVOS ATTORNEYS** tunapenda kuutangazia umma wa Tanzania kukanusha vikali taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa LUCY MAGERELI, Mbunge wa Chadema Viti maalum mnamo tarehe 1/2/2020, kuhusu uwekezaji unaofanywa na wateja wetu Mkoani Morogoro.

Katika taarifa hiyo wakati akiwakilisha mada katika mkutano wa uwekezaji, mheshimiwa **LUCY MAGERELI** alidai kuwa mteja wetu amekuwa akiombwa rushwa ili kufanikisha kupata vibali vya uwekezaji. Mteja wetu anakanusha vikali madai ya Mheshimiwa huyo na wala hakutumwa na Uongozi wa Kampuni ya mteja wetu kutoa taarifa za kupotosha na zenye lengo la uchonganishi kati ya mteja wetu, Viongozi na Taasisi za Serikali.

Tangu kusajiliwa mwaka 2012 mteja wetu amekuwa akifanya biashara vizuri bila migogoro yoyote. Umma unaombwa kupuuza madai ya **Mheshimiwa LUCY MAGERELI,** Mbunge wa viti maalum, Chadema.

Jerome Joseph Msemwa
Wakili Mwandamizi

215627402

# Fidia inavyouweka njia panda uchimbaji wa graphite Ulanga

## ■Wakazi wako tayari kuondoka, mtihani 'chao'
## ■Miezi 27 wawekezaji hawajui mwanzo lini
## ■Mwenyekiti Halmashauri alia kutelekezwa

**Na Salome Kitomari**

BADO ni kitendawili ni namna gani utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa madini ya kinywe au graphite wilayani Ulanga mkoani Mororgoro, kikisimama katika njia panda; uanze vipi na uendelee vipi?

Wakati serikali kwa upande wake imeshatoa ruksa kwa mradi huo kuanza, upande wa pili wa sarafu, nyenzo kuu inayowezesha mradi kuanza msamiati wa 'fidia' bado haujatekelezwa kuwafanya wakazi na wawekezaji wengine wa huduma za umma kama vile kanisa, kupisha eneo wakiwa na rasilimali za kuanza maisha kwingineko.

Kimsingi, huo si uamuzi wa hiari tu au makubaliano chini ya mwembe wa halmashauri fulani, bali ni mwongozo rasmi ya sheria, tena unaoenda mbali zaidi, ukitoa kipindi maalum cha malipo kufanyika kwa miezi 24 liwe limeshatekelezwa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Nasoro Kihiyo, sheria inatamka kuwa ni miaka miwili fidia iwe imekwishalipwa na baada ya hapo ni lazima kufanyike hesabu mpya kutathmini gharama za kucheleweshana.

Kihiyo anasema tarehe hiyo ya kuanza kufanyiana hesabu mpya na gharama za ziada, ilishatimu wastani wa miezi mitatu sasa au kwa usahihi zaidi, Novemba mwaka jana.

### HALI IKOJE?

Kampuni tatu zimeshapata vibali vya kuchimba madini ya kinywe kutoka Wizara ya Madini, lakini hazijaanza kazi hiyo kutokana na sababu mbalimbli, moja ya kampunji hizo ikiwa imefanya tathmini miaka mitano iliyopita.

Kampuni hizo ni Mahenge Resource, Kibarani na Tanzania Graphite ambazo zimepewa kibali cha kuchimba madini hayo katika maeneo ya Nawenge, Msogezi, Epanko, Mdindo, Liandu, Msogezi na Kisewe.

Kampuni ya Tans Graphite ilianza taratibu ya tathimini tangu mwaka 2015, lakini hadi sasa imeshindwa kulipa fidia kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni mabadiliko ya Sheria ya Madini yaliyofanyika mwaka 2017 yaliyoilazimu isimamishe ulipaji wa fidia.

Tans Graphite ni kampuni tanzu ya kampuni ya Kibaran Resources Limited yenye makao makuu yake Australia ikiwa na maeneo matano ya uchimbaji wa madini, ambayo ni Mirerani (maeneo mawili), Tanga na Mehenge inakochimba graphite.

Katika tovuti ya Kampuni ya Kibaran Rerources, inaelezwa kuwa Kampuni ya Tans Graphite ilifanya utafiti mwaka 2012/13 na kubaini kuwapo kwa wingi kwa madini ya kinywe nchini.

Januari 2014, kampuni hiyo ilifanya tathimini ya mazingira katika eneo la Merarani, Arusha na ilipata leseni mwaka 2015 kwa ajili ya kuanza uchimbaji.

Kampuni hiyo inaeleza kuwa madini hayo yatauzwa Ujerumani na nchi zingine za Bara la Ulaya zenye viwanda vya chuma, huku ikibainisha kuwa masoko ya madini hayo pia yako Marekani, Asia, Japani na Korea Kusini.

Katika tovuti ya Tanzania Invest, inaelezwa kuwa mwaka 2014, China ilikuwa mzalishaji mkubwa wa madini hayo ikiwa na tani 780,000, ikifuatwa na India tani 170,000, Brazil tani 80,000 na kwamba Tanzania itakuwa nchi yenye uzalishaji mkubwa wa madini hayo.



Waziri wa Madini, Doto Biteko.

Diwani wa Nawenge, Protas Lunkombe, ambaye ni mmoja wa wanaotakiwa kufidiwa kupisha mradi huo, anasema wananchi wa Kijiji cha Epanko wanatakiwa kupisha eneo hilo na muda wa uthamini ulishaisha, lakini kampuni zimechelewa malipo ya fidia.

"Mara kadhaa tumeuliza wanasema uthamini hautaanza upya, bali watafanya malipo kabla muda haujapita sana. Wananchi wameshindwa kufanya maendeleo yoyote kwa kuwa wamezuiwa na hawajui lini watalipwa.

"Hakuna chochote kanachondelea, mtu anaogopa kufanya chochote, kadri wanavyozidi kuchelewa, ndivyo nasi tunazidi kukwama," analalamika.

### JUHUDI ZA MBUNGE

Jukumu la msingi la mbunge ni kutetea maslahi ya wananchi anaowawakilisha. Mbunge wa Ulanga Mashariki, Goodluck Mlinga, anasema sheria za madini zilizopitishwa miaka ya karibuni zimekuwa kikwazo kwa kampuni zilizokuwa zimefanya tathmini ya fidia katika mradi huo.

"Kuna wawekezaji wengi wamekwama kutokana na sheria mpya zilizopita, rasilimali zao na fedha walizokopa haziwiani," anasema.

Mbunge huyo anasema Kampuni ya Tanzania Graphite ilipaswa kulipa fidia mwishoni mwa mwaka jana, lakini haijafanya hivyo kutokana mabadiliko ya kisheria, hususani kwenye masuala ya kibenki.

Mlinga anasema uthamini wa kwanza umekufa na wanatakiwa wafanye makadirio kulingana na bei ya soko la sasa, lakini hakuna kilichofanyika.

"Kampuni ya Mahenge Resource wanahamasisha wananchi ili kufanya uthamini wa waliokuwa wameufanya awali, Tanzania Grahite wameshindwa kulipa kama walivyopaswa kufanya hivyo ndani ya miaka miwili," anasema.

Mbunge huyo pia anaeleza kuwa wapo wananchi waliokuwa wamekataa fidia, likiwamo Kanisa Katoliki Jimbo la Mahenge na mpaka sasa utatuzi wa tatizo hilo bado haujafanyika ipasavyo.

"Kanisa bado hawajafikia mwafaka mzuri kwa kuwa walitaka watafute mtu wao wa mthamini, eneo likishakuwa na soko au kanisa thamani inapanda, lakini wathamini walichukua kama mashamba,"anasema.

Mbunge huyo anasema kuwa familia 52 na vikundi mbalimbali vya kijamii vilikuwa vimekataa uthamini wa awali, lakini idadi yao imeendelea kupungua.

"Wananchi wamekaa muda mrefu bila kulipwa, kwa mahesabu ya kawaida ni miaka mitano sasa wananchi wanashindwa kuendeleza maeneo yao.

"Nazungumza na serikali, kuna vitu vingi havijakaa sawa, suala la hisa kwenye migodi mikubwa, mambo mengi yamekwama, wananchi wanapata tabu hasa wa Epanko, wanasubiri vitu ambavyo hawajui lini vitawezekana au watafidiwa na kuondoka," anasema.

### KAULI YA ASKOFU

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mahenge, Agapitus Ndorobo, anasema kanisa linamiliki ardhi katika maeneo ya Mdindo, Liandu, Epanko, Msogezi na Kisewe ambako kote kuna madini hayo.

Anasema kwa miaka mitano sasa, kanisa limeshindwa kufanya maendeleo yoyote katika eneo la Epanko kutokana na kusubiri taratibu mbalimbali kufanyika.

Askofu huyo alibainisha kuwa awali kanisa lilitaka kuwa na ubia na kampuni zinazokwenda eneo hilo na siyo kulipwa fidia, lakini baada ya tafakuri na kuona ambavyo watakapaswa kuwa na fedha nyingi za kuwekeza, wamekubali kulipwa fidia na kupisha mradi huo.

"Miaka mitano Tanzania Ghraphite hawajafanya lolote, tulishawaeleza watufidie, wakati wanataka kuchukua ardhi tutajua na hadi sasa hatujajua lolote, tunamilikia maeneo hayo tangu mwaka 1921, kuna mipangilio mingi tumekuwa nayo na lazima wafidie kulingana na hayo mazingira na soko.

"Kama wangekuwa na fedha wangelipa, walikuja Mahenge Resource, nikawaambia kama wanaingia kazini, lazima wawasiliane na kanisa, baadaye nimeaambiwa wamefanya utafiti hadi maeneo ya kazini."Kama kanisa, tunataka watulipe na tutasema tunahama kila mahali, lazima tuwaze kuwa na ubia maana ardhi ni yetu na kila mahali sasa watatuhamisha.

"Madini yapo lakini kampuni zinaweza kuchimba, na je wamefidia? Tanzania Ghraphite wamejenga nyumba mbili za mfano eneo la Epanko, lakini hadi sasa hawajaja kanisani kufanya mazungumzo kwamba watatulipaje," anasema.

Askofu huyo anabainisha kuwa upo uwezekano mkubwa wa athari za kimazingira hasa kwenye maji, kwa kuwa uchimbaji utafanyika milimani na wananchi wanategemea maji kutoka kwenye milima hiyo.

"Katika hili, tunataka mazungumzo kwa kuwa maji haya yanakwenda hadi Mto Kilombero, unaotegemewa na mamilioni ya wananchi kwa ajili ya chakula, kunywa na shughuli za kilimo. Tunataka kujua ni kwa kiasi gani maji hayataharibika," anasema.

### KIINI CHA TATIZO

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Kihiyo, anasema kwa mujibu wa sheria tathmini inapofanyika, inatakiwa wahusika walipwe fidia ndani ya miaka miwili, na inapopita wahusika wanapaswa kulipwa gharama za usumbufu na tathimini kufanyika upya.

Anasema kwa Kampuni ya Tanzania Graphite inayowekeza katika Kijiji cha Epanko, muda wa kulipa fidia uliisha Novemba mwaka jana, na iliahidi kulipa fedha za usumbufu ili ifanye uthamini upya, lakini hadi sasa ukimya umetawala.

Kihiyo anasema kampuni hiyo imejenga nyumba za mfano kwenye kaya mbili ambazo zimeshawishi wananchi wengi kukubali fidia na kuachana na msimamo wa awali.

"Kampuni hiyo ilijenga nyumba mbili za mfano za matofali ambazo kwa hadhi ya kijijini, ileta mabadiliko makubwa na wananchi wengi wamejikuta wanapenda kujengewa nyumba kama hizo," anasema.

Kihiyo anasema mabadiliko ya sheria ya madini yaliyotaka serikali iwe na hisa asilimia 16 kwenye kila mgodi, yaliwafanya wawekezaji washindwe kusonga mbele kwa kuwa hawakuwa na uhakika na usalama wa uwekezaji wao.

Kihiyo anasema kitendo cha serikali kuingia makubaliano na Kampuni ya Barrick hivi karibuni, kimetoa mwongozo wa namna mgawanyo wa hisa unavyopaswa kuwa.

"Tathimini ikishafanyika, kazi zinasimama, wananchi wameshindwa kufanya maendeleo yoyote kwa miaka miwili wakisubiri kulipwa fidia, lakini sheria inasema ukishafanyiwa tathimini, miaka miwili ikipita, wanatakiwa kuanza upya, na ili wapewe kibali cha tathimini nyingine, lazima waonyeshe ushahidi wa fedha za kulipa ili wasisumbue watu," anasema.

Kihiyo alisema halmashauri hiyo ilianishwa mwaka 1984, lakini tangu wakati huo, haijawahi kupata hata senti moja kutokana na uchimbaji wa madini hayo, matarajio yakiwa ni kunufaika na asilimia 0.3 ya mauzo kisheria.

"Tunataraji kupata asilimia 0.3 inayotokana na mauzo ya migodi yote, mfano wakiuza vipande 1,000, sisi tunachukua vitatu, matarajio kama migodi yote mitatu itaanza uzalishaji, tutapata Sh. bilioni moja hadi mbili kwa mwaka kwa mujibu wa bei ya madini kwenye soko la dunia," anasema.

Kwa mujibu wa Kihiyo, uchimbaji wa madini hayo, ukianza rasmi, utaleta maendeleo makubwa wilayani humo, ikiwa ni pamoja na kuongeza mzunguko wa fedha, kuboresha miundombinu ya barabara ambazo zitaboreshwa ili kupitisha magari makubwa zaidi ya 30,000.

■ITAENDELEA KESHO

## Sheria kufumuliwa kuvutia wawekezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, amesema serikali inafanya mapitio ya sheria ya uwekezaji ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuvutia wawekezaji.

Aidha, ameshauri benki ziwekewe masharti ili zitoe mikopo katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Kairuki alisema hayo jana alipokuwa akifungua kongamano la sita la Jukwaa la Wadau wa Sera za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, jijini hapa kwa niaba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alisema serikali imedhamiria kuimarisha uwekezaji kwenye kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwa ni sekta zitakazoifikisha Tanzania katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

"Tunaendelea kufanya mapitio ya sheria yetu ya uwekezaji ili kuhakikisha tunakuwa sheria ya kisasa, itakayokwenda na wakati, itakayohimili ushindani, itakayomkomboa kweli mwekezaji katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi," alisema.

Kuhusu mikopo, Kairuki alisema: "Suala la mitaji tutaendelea kuziongezea benki zetu, lakini hata tunapoelekea kwenye ilani za vyama eneo linapaswa kuangalia benki zetu zinawekewa masharti badala ya kukopesha wafanyakazi tu pia iangaliwe namna ya kukopesha sekta hizi muhimu."

Pia waziri huyo alisema wameanza kufanyia kazi kuwa na vivutio maalum kwa mkoa wa Dodoma ili kupata wawekezaji wengi zaidi.

"Tumeamua kuimarisha uchumi wetu kupitia sekta ya viwanda, kilimo ndio msingi mkuu wa maendeleo ya viwanda. Sekta hizi zinategemeana na ukuaji wa pamoja kilimo na viwanda, asilimia 65 ya malighafi hapa nchini inatokana na sekta ya kilimo," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka 2018, miradi 2821 ilisajiliwa na kituo cha uwekezaji na asilimia 17.9 ya miradi ni ya

INAENDELEA UK. 8

# Wanaokwenda China kuchukuliwa alama za vidole

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imesema Ubalozi wa China nchini Tanzania imeanzisha mfumo wa kuchukua alama za vidole kwa waombaji Visa.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Emmanuel Bohohela.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na kuanzishwa kwa mfumo huo Desemba 24, mwaka jana, mwombaji atalazimika kufika ofisi ya ubalozi huo ili kuchukuliwa alama za vidole kama sehemu ya kukamilisha taarifa za uombaji wa visa.

"Ubalozi umeeleza kuwa utaratibu huu hautawahusu waombaji walio katika makundi ambayo ni wenye umri chini ya miaka 14 na zaidi ya miaka 70. "Wengine ni waombaji wenye pasi za kusafiria za kidiplomasia na za utumishi, waombaji walioomba visa kwa kutumia pasi ya awali ambayo tayari alama za vidole zilichukuliwa na haijamaliza muda wa miaka mitano," ilisema taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo ilitaja makundi mengine ambayo hayatahusika kuwa ni wale wenye matatizo ya alama za vidole katika vidole vyote 10 vya mikono au vyote vyenye ulemavu ambao hautawezesha alama za vidole kuchukuliwa.

"Serikali ya China inaendelea kuboresha taratibu za mifumo ili kuwezesha mwingiliano wa China na mataifa mengine na inawakaribisha wageni wote kutembelea nchi hiyo," ilisema taarifa hiyo.








TASAF — TANZANIA SOCIAL ACTION FUND — MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII**

**KIPINDI CHA PILI CHA AWAMU YA TATU**

**UTANGULIZI**

Kipindi cha Kwanza cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kilitekelezwa kuanzia 2012 na kukamilika Desemba 2019. Utekelezaji ulifanyika katika halmashauri 159 za Tanzania bara, Unguja na Pemba na kufikia kaya milioni1.1 zenye zaidi ya watu milioni 5.

Tathmini ya utekelezaji wa sehemu ya kwanza inaonyesha kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Mpango huu umefanikisha azma ya serikali ya kupunguza umaskini nchini. Takwimu zinaonesha kwamba umaskini wa mahitaji ya msingi umepungua kwa asilimia 10 na umaskini uliokithiri umepungua kwa asilimia 12 kwa kaya maskini.

Utekelezaji umewezesha walengwa kujikita kwenye ufugaji, uvuvi, kilimo na biashara na kujiimarisha kiuchumi. Vile vile Mpango umeongeza idadi ya watoto kutoka katika kaya maskini kuandikishwa shule kwa kiwango cha asilimia 7.2. katika sekta ya afya, Mpango umeongeza mahudhurio ya kliniki kwa watoto walio na umri chini ya miaka 5 kwa kiwango cha asilimia 1.5

Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Kipindi cha Pili kinatekelezwa katika halmashauri 185 za Tanzania bara, Unguja na Pemba katika vijiji/mitaa/shehia zote ikiwa ni pamoja na Vijiji/Mitaa/Shehia zaidi ya 5,000 ambavyo hazikufikiwa katika utekelezaji wa kipindi cha Kwanza. Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitafikia kaya milioni 1.4 zenye watu wapatao milioni 6 kote nchini.

Madhumuni ya Kipindi cha Pili cha TASAF ni kuwezesha kaya zilizoandikishwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za kiuchumi na kijamii na kuendeleza rasilimali watu husuan watoto.

Taarifa ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2011/2012 inaonesha asilimia 28.2 ya watanzania wanaishi katika umaskini huku asilimia 9.7 wanaishi katika umaskini uliokithiri hivyo utekelezaji wa Kipindi cha Pili utawezesha kaya maskini kujikwamua kutoka kwenye umaskini na kufanya kazi na kujiimarisha kiuchumi na kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025

Utekelezaji wa Kipindi cha Pili cha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Shughuli kuu zitakazofanyika ni kutoa fursa ya ajira za muda kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini, elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira. Kuhamasisha walengwa kujiunga katika vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji mali na kutoa ruzuku kwa masharti ya elimu na afya kama kichocheo cha mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki ili kupata elimu na huduma za afya na hivyo kuwajengea maisha bora. Aidha wadau katika ngazi mbali mbali watajengewa uwezo kwa njia ya mafunzo ambayo yatawawezesha kutekeleza na kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

**Matarajio**

Matarajio ya Serikali kupitia utekelezaji wa TASAF ni kupunguza kiwango cha umaskini kwa kutoa fursa kwa walengwa kushiriki kwenye kazi za kilimo na uzalishaji na hivyo kuchochea ukuaji wa viwanda, kuboresha miundombinu ya elimu afya hivyo kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto na kuongeza kiwango cha wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kupitia miradi ya kuongeza kipato kaya maskini ziweze kuboresha lishe kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, na kupunguza udumavu na utapiamlo kwa watoto.

***Kipindi cha Pili cha Awamu ya III ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kitazinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.***

***Kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Dar es Salaam, tarehe 17/02/2020***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadaiwa NHC dawa ni kulipa

**WAZIRI** Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha waliohama kwenye nyumba za shirika hilo na kuacha madeni wanalipa fedha hizo kabla ya Juni mwaka huu.

Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa wapangaji waliohama bila kulipa wanadaiwa Sh. bilioni 4.353, wakati wapangaji waliopo wanadaiwa kiasi cha Sh. bilioni 1.286, hivyo kufanya deni lote lifikie Sh. bilioni 5.641.

Majaliwa ameitaka bodi hiyo kuwaandikia barua wapangaji wote, ikiwamo baadhi ya taasisi za serikali wanaodaiwa kodi na shirika hilo na wahakikishe zimelipwa ifikapo Mei 30, mwaka huu. Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na viongozi na wajumbe wa Bodi ya Shirika jijini Dar es Salaam, huku akitaka wote hao wafuatilie na walipe madeni yao.

Miongoni mwa wapangaji wa nyumba hizo ni taasisi zote za serikali ambazo nazo zimetakiwa zilipe madeni. Ni wazi kuwa agizo hilo la Waziri Mkuu ni kaa la moto kwa viongozi wa taasisi zilizopanga na kuamua kuhama kwenye majengo hayo kabla ya kulipa madeni.

Waziri Mkuu aliweka bayana kuwa chombo chochote cha serikali kinaishi na bajeti, kwa hiyo hata kama wamejenga ya kwao, walipaswa walipe madeni ya pango kabla hawajahama.

Tunaunga mkono hatua hii ya agizo la Waziri Mkuu kwa kuwa linalenga kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha za umma na kuondoa mianya ya kuikosesha mapato serikali, uzembe na uwajibikaji.

Katika kuonyesha kuwa hataki ujanja ujanja katika jambo hilo Waziri Mkuu aliagiza apatiwe orodha ya taasisi za serikali zinazodaiwa ili azifuatilie mwenyewe. Aliahidi kuwa atawaita wakuu wa taasisi hizo mmoja mmoja ili apate mrejesho kuhusu madeni hayo. Waziri Mkuu alitaja madeni ambayo taasisi za serikali zinadaiwa yanafikia Sh. bilioni 4.3, ambazo kama zitalipwa, zitalisaidia shirika kuendelea na mpango wake wa ujenzi wa nyumba nafuu kwenye maeneo mbalimbali.

Hatua ya Majaliwa ni mwendelezo wa jitihada za serikali kuwataka wadaiwa wote sugu wa shirika hilo kulipa madeni yao. Kwa mfano, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameshawatangazia wapangaji wote na kuwapa notisi kuwa wataondolewa kwa nguvu katika nyumba hizo. Shirika pia limeshatoa notisi kama hiyo kupitia vyombo vya habari.

Wadaiwa hao kwa hakika wanapaswa kubanwa kulipa madeni yao, kwa kuwa kuchelewa ama kukwepa kulipa ni kuminya hatua za maendeleo zinazopaswa kufikiwa na shirika hilo na kunufaisha serikali na jamii kwa ujumla.

Miongoni mwa mambo ambayo shirika hilo linatakiwa lijikite nalo ni pamoja na ujenzi wa nyumba bora na za bei nafuu, kwa sababu mahitaji ya nyumba nchini bado ni makubwa. Aliyoagiza Majaliwa yakitelekezwa, yatasaidia wananchi wa kipato cha chini kumudu na kunufaika na uwapo wa shirika hilo, hivyo kuonyesha maana halisi ya kuwapo kwa shirika hilo.

Viongozi wa NHC wanapaswa kuchukua hatua kadhaa ili kulifanya shirika kujiendesha na kutoa huduma bora kwa wateja na taifa kwa ujumla, zikiwamo kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha kodi zinakusanywa kwa njia ya kielektroniki.

Utaratibu wa kuruhusu maofisa kwenda nyumba kwa nyumba na kudai Sh. 500,000 kwa risiti za kuandika unatia shaka na kutoa mwanya wa kufanyika udanganyifu.

Pia utaratibu huo unazua maswali kwa nini NHC linajichelewesha katika kutumia control number, ili mwananchi kulipia kwa simu au benki ili fedha ziingie moja kwa moja katika shirika kama inavyofanywa na mashirika kadhaa ya umma yakiwamo Tanesco, Dawasa kwa kutaka baadhi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hatuna mbadala, safari ya nishati ndio ahueni misitu

Na Sabato Kasika

**MAZINGIRA** ni jumla ya mambo na vitu vyote vinavyomzunguka viumbe hai na kwa kawaida, vinategemea mazingira, hata viumbe visivyo hai pia hutegemea mazingira, yanajumuisha ardhi, maji, hewa uoto, na vingine ambavyo kwa ujumla wake husababisha kuwapo kwa uhai.

Kutokana na umuhimu huo, kuna haja ya kupambana kwa kila njia ili kuhakikisha mazingira yanalindwa mazingira, kwa vile binadamu na viumbe vingine wa pamoja wanahitaji kuishi, hivyo jamii haina budi kushiriki kikamilifu kwenye kutunza nna kulinda mazingira hata kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Bila ya kufaya hivyo, madhara yake yatakuwa ni makubwa, kwani athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira zinaweza kusababisha jamii kupata athari zikiwamo za ukame ambazo mwisho wake siku ni kukosa mazao ya chakula na biashara na hivyo kuathirika kiuchumi.

Nimegusia hilo kwa kifupi, ili kujadili kidogo suala la ukataji wa mitu kwa ajili ya biashara mkaa, ambayo imekuwa ikifanyika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha uharibifu wa mazingira, ambayo mwisho wake nchi inaweza kugeuka jangwa kama kasi ya kukomesha biashara hiyo haitakuwa kubwa.

Inawezekana, kuna sababu zinazowafanya Watanzania kutumia nishati ya mkaa na baadhi ikiwamo utamaduni na mazoea, kwa kuamini kwamba mkaa unaivisha chakula vizuri, tofauti na nishati nyingine na pia gharama yake siyo kubwa sana kama ilivyo kwa matumizi ya umeme, lakini ukweli unabaki palepale kwamba matumizi ya mkaa yanaharibu mazingira.

Hebu fikiria, magunia ya mkaa yanayoingizwa jijini Dar es Salaam kila siku, ni wastani wa 400,000 hadi 500,000 huku matumizi ya kuni nchini yakiwa ni zaidi ya asilimia 71 ya watu wote. Hapa maana yake ni kwamba, miti mingi inakatwa kwa ya nishati na kusababisha uharibifu wa mazingira.

Hivyo ndivyo, Bunge limeelezwa juzi huku serikali ikisema kuwa inaendelea na mikakati yake ya kuhakikisha gesi asilia inatumika majumbani, ili kupunguza uharibifu wa mazingira, watu 600 wameshanza kutumia gesi hiyo.

Ni jibu la Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kwa swali la nyongeza la bungeni, alipohojiwa jitihada za serikali katika kulinda misitu na mikakati ya haraka wa matumizi ya gesi, ili kupunguza uharibifu wa mazingira. Dk. Kalemani anasema, wiki iliyopita ameunganisha gesi kwa wafanyakazi 110 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni mkakati mzuri wa kupunguza uharibifu huo na kwamba ya pili, itakuwa ni kwa mikoa yote ya Tanzania Bara, kwa kuanza kusambaza mitungi iliyoshindiliwa gesi na kujenga mabomba kwenye mikoa hiyo kuanza kusambaza katika vijiji vyote ikiwa ni mkakati wa kupunguza uharibifu wa mazingira.

Ninaweza kusema kuwa hii ni habari njema na kama mkakati huo utakamilika, basi kwa kiasi fulani utapunguza matumizi ya mkaa ambayo kwa kweli yanachangia katika uharibifu wa mazingira ambao mwisho wake ni nchi kuwa jangwa, kutokana na miti mingi kukatwa.

Wafanyabiashara wa mkaa nao hawana budi kuliona hilo badala ya kujali pesa tu huku wakiharibu mazingira, kwani kama Dar es Salaam tu inapokea magunia ya mkaa kiasi hicho, ina matumizi ya mkaa kwa nchi nzima ni makubwa, kwani sidhani kwamba hakuna mkoa usiotumia nishati hiyo.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constatine Kanyasu, Tanzania ina rasilimali za misitu zinazokadiriwa kufikia hekta milioni 48.1, ambapo asilimia 34.5 inasimamiwa na Serikali Kuu, asilimia 6.5 inasimamiwa na halmashauri na pia asilimia 45.7 inasimamiwa na vijiji, asilimia 7.3 inasimamiwa na sekta binafsi.

Asilimia sita ya misitu iko katika ardhi huria.

Anasema, kulingana na taratibu za serikali, misitu ya Tanzania inasimamiwa na Sheria ya Misitu ya Mwaka 2002.

Katika mamlaka za usimamizi wa misitu nchini, zipo wizara kuu mbili, ambazo ni Maliasili na Utalii, ambayo imekasimu mamlaka kwa Wakala wa Misitu (TFS), ambayo ina jukumu la kusimamia misitu ya hifadhi ya serikali kuu na misitu mingine yote ambayo haijahifadhiwa kisheria.

Naibu Waziri Kanyasu anabainisha utafiti uliopo, misitu ya Tanzania inakabiliwa na matatizo makubwa mawili, mojawapo ikiwa ni uharibifu mkubwa unaofikia kiasi cha hekta 372,000 kwa mwaka na mahitaji ya mazao ya misitu kwa mwaka yanayozidi uwezo wa misitu kwa zaidi ya mita za ujazo milioni 19.5.

# Serikali yazitaka kampuni za bima kutanua wigo

**Na Zuwena Shame**

SERIKALI imezitaka kampuni za bima na taasisi za kifedha nchini kutanua wigo wa huduma zao ndani ya miji ili kupata faida katika taasisi zao na jamii.

Mkurugenzi msimamizi wa masoko na leseni kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) nchini, Samwel Mwiru, alisema hayo wakati wa uzinduzi wa huduma za bima kutoka benki ya Diamond Trust (DTB) Bancassurance.

DTB-Tanzania inakuwa benki ya kwanza na taasisi ya kifedha kuzindua huduma za Bancassuarnce nchini baada ya serikali kupitia Benki Kuu (BoT) na TIRA kuweka sheria inayoruhusu taasisi za kifedha kujikita kwa ufanisi kutoa huduma za bima nchini mwaka jana.

Mwiru alisema maendeleo ya tasnia ya bima yanahitaji msaada wa wawekezaji binafsi ili kuchochea kupenya bidhaa za bima sokoni.

Mwiru alisema licha ya kiwango kizuri cha ukuaji wa uchumi wa taifa, na uwapo wa bidhaa mbalimbali za bima bado mchango wa bima kwenye Pato la Taifa upo chini, lakini mahitaji na faida zake ni kubwa.

"Kwa niaba ya TIRA, naikaribisha DTB-Tanzania katika biashara ya Bancassurance huku tukiweka msukumo kwa wadau wote wa umma kwa ujumla katika kuchochea ukuaji wa tasnia ya bima," alisema Mwiru.

Mkurugenzi wa DTB -Tanzania, Viju Cherian, alisema, ushirikiano na kampuni ya bima utatoa suluhisho kamili la bima kwa wateja.

Cherian aliongeza kuwa moja ya lengo ya huduma mpya Bancassurance ni kujikita kwa wajasirimali wadogo na wa kati (SME) waweze kumudu na kuhudumia huduma za bima na kujiongezea kipato.

"Kwa ukubwa wa wateja wetu tunaamini kuwa upelekaji wa huduma za bima kwa mtu wa kawaida na wajasiriamali wadogo itasaidia kupunguza hatari kwa mtu binafsi," alisema Cherian.

Pia alisema, DTB Tanzania imeleta toleo kamili la bidhaa ambalo linajumuisha bidhaa za bima ndani ya matawi ya benki hiyo na lengo pia ni kutoa huduma kwa wateja wa aina zote za biashara na shughuli za kiuchumi.

Benki ya DTB-Tanzania ina mtandao wa matawi 27 nchini ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza , Dodoma, Tanza, Kahama, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mtwara, Tabora, Tanga na visiwani Zanzibar.


TANZANIA PORTS AUTHORITY

**BANDARI COLLEGE DAR-ES-SALAAM**

**APPLICATION FOR ADMISSION INTO BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE AND ORDINARY DIPLOMA PROGRAMMES FOR ACADEMIC YEAR 2020/2021 (MARCH INTAKE)**

Bandari College Dar-es-salaam invites application for admission into various Basic Technician Certificate (NTA Level 4) and Ordinary Diploma (NTA Level 5-6) Programmes for the Academic Year 2020/2021 (March Intake) as follows:-

| S/N | PROGRAMME | ENTRY QUALIFICATION | DURATION |
|---|---|---|---|
| 01 | Basic Technician Certificate in Shipping and Ports Management | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects. | 1 year |
| 02 | Basic Technician Certificate in Freight Clearing Forwarding and Ports Management | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects. | 1 year |
| 03 | Basic Technician Certificate in Logistics and Transport Management | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects. | 1 year |
| 04 | Basic Technician Certificate in Business Administration | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects. | 1 year |
| 05 | Basic Technician Certificate in Engineering and Maintenance Management | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects, three of which must be Basic Mathematics, Physics/Engineering Science and English Language. | 1 year |
| 06 | Basic Technician Certificate in Information and Communication Technology | Holder of Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with a pass in at least four (4) non-religious subjects, two of which must be Basic Mathematics and English Language. OR Holder of NVA Level III and Certificate of Secondary Education Examination (CSEE) with passes in Basic Mathematics and English Language. | 1 year |
| 07 | Ordinary Diploma in Shipping and Ports Management | Holder of Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Shipping and Ports Management. OR Holder of Advanced Certificate of Secondary Education Examination (ACSEE) with at least one principal pass and one subsidiary in non-religious subjects. | 2 years |
| 08 | Ordinary Diploma in Freight Clearing Forwarding and Ports Management | Holder of Basic Technician Certificate (NTA Level 4) in Procurement and Supply, Logistics, Clearing and Forwarding. OR Holder of Advanced Certificate of Secondary Education Examination (ACSEE) with at least one principal pass and one Subsidiary in non-religious subjects. | 2 years |

**TUITION FEE**

Tuition fee is Tshs 900,000/= for Basic Technician Certificate and **Tshs 1,000,000/=** per year for Ordinary Diploma, and it is paid in four installments.

**HOW TO APPLY**

Applicants should apply directly to Bandari College, application fee is **10,000/= TZS** for Tanzanians and **30,000/=TZS** for Non-Tanzanian. Applicants should apply from **15 January, 2020 to 20th February, 2020.**

**COMMENCEMENT OF STUDIES**

The studies will commence on **02nd March, 2020.**

**For any inquiries, please call +255658782843,**
**Email Address: pbc@ports.go.tz**

**Issued by the Principal**
**Bandari College**

# Membe, Makamba, Kinana wawekwa kiporo siku saba

INATOKA UK. 2

Makao Makuu ya chama hicho Dodoma na kuhojiwa kwa zaidi ya saa tano. Sintofahamu iliibuka kuhusu sababu za Makatibu Wakuu hao wastaafu kutokuhojiwa wiki iliyopita kama wito wa kamati hiyo ulivyowataka.

Katika hatua nyingine, Polepole alisema kamati kuu hiyo pia ilipokea taarifa ya muendelezo wa aandalizi ya Mwelekeo wa Sera za CCM kwa Mwaka 2020 hadi 2030 na Ilani ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Alisema kamati hiyo imepokea taarifa ya Maendeleo ya Uandishi wa Waraka huo muhimu wa kisera na kujiridhisha na kazi nzuri ambayo imeshafanyika mpaka ngazi ya rasimu.

"Kamati Kuu pia imepitia zoezi la uandishi wa Ilani ya CCM katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kuagiza maoni ya wadau mbalimbali kujumuishwa na kuzingatia ratiba ya kukamilisha uandishi wake ili vikao vya chama vifanye uamuzi na kupitisha," alisema Polepole.

Katika hatua nyingine, Polepole alisema Kamati Kuu ilipokea taarifa ya maombi ya kujiunga na CCM kutoka kwa Waziri Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye, na kupongeza kazi nzuri inayofanywa na chama na Serikali ambayo imekiletea chama heshima kubwa na kukubalifu kwa umma wa wananchi, wanachama na viongozi wa vyama vingine vya siasa.

"Kikao kimempongeza Sumaye kwa uamuzi wake, kimeelekeza utaratibu wa kujiunga rasmi katika chama ufuatwe kwa mujibu wa Katiba ya CCM," alisema Polepole.




Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza, ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, John Mongella (mwenye shati la kitenge na kofia), wakiwa kwenye boti jana, kuanza ziara ya kutembelea visiwa vidogo vilivyomo kisiwani Ukerewe, ili kutatua changamoto za afya na elimu. **PICHA: ROSE JACOB**

# Ndege kufundishia marubani kutua Okt.

INATOKA UK. 3

wa ndege na kwamba vingine inaendelea kununua. Alisema chuo kimeshapata fedha kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya utekelezaji wa suala hilo.

Prof.Mganilwa alisema chuoni hapo wameshaanza kufundisha masomo ya wahudumu ndani ya ndege lakini wanakabiliwa na uhaba wa vifaa katika ufundishaji.

"Tumeshaagiza vifaa vingine vingi sana vyenye thamani ya Sh. bilioni 50 vyote kwa ajili ya kufundisha Watanzania stadi za usafiri wa ndege, reli na sekta ya majini. Walimu tunao, wahudumu ndani ya ndege tumeshatoa mikupuo miwili na wa mkupuo wa tatu wapo darasani," alisema Prof. Mganilwa.

Aliongeza kuwa wahandisi wa ndege wameshahitimu mikupuo miwili, lakini upande wa marubani bado hawajaanza kufundisha na wanasubiri ujio wa ndege hizo.

Kuhusu wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo, Prof. Mganilwa alisema kabla hawajahitimu wanapelekwa kwenye miradi mikubwa inayojengwa na serikali na wanapohitimu wanaajiriwa kutokana na mahitaji yao.

Mwenyekiti wa Baraza la NIT, Prof. Bavo Nyichomba, alisema lengo kuu la kuanzishwa kwa NIT ni kutoa wanafunzi watakaosaidia ujenzi wa uchumi wa viwanda na kusaidia taifa katika nyanja mbalimbali.

Alisema dhumuni la ziara ya wajumbe katika chuo hicho ni waone na kutoa ushauri utakaokiwezesha NIT kuwa chuo cha kisasa na bora katika ukanda wa Afrika Mashariki katika kutoa wahitimu kwenye nyanja za reli, anga, magari na majini.

# Sheria kufumuliwa kuvutia wawekezaji

INATOKA UK. 5

kilimo.

"Bado tunahitaji jitihada za makusudi katika sekta ya kilimo ili kuvutiwa zaidi na wawekezaji kuwekeza kwa kuwa sensa iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuhusu idadi ya watu na ukuaji wa miji, inaonyesha kiwango cha ukuaji wa miji ni asilimia 29.1, hivyo miji yetu inakuwa kwa kasi," alisema.

Kairuki alisema serikali itahakikisha inafanya kazi kwa karibu na wadau hao ili kupunguza kero mbalimbali za kisera na kisheria.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema kuna ng'ombe milioni 32.5, mbuzi milioni 20, kondoo milioni 5.5, kuku milioni 79.1 na mayai bilioni nne.

"Sekta ya uvuvi hadi kufikia mwaka 2018, samaki waliopo baharini ni kilo bilioni 2.8 na mwaka huo tulikuwa tunatumia Sh. bilioni 56.04 kuagiza samaki kutoka nje, lakini imeshuka ndani ya mwaka mmoja hadi Sh.Milioni 37 ni punguzo la asilimia 99.93,"alisema.

Aidha, alisema ukanda wa bahari kuna viwanda sita na kwamba kunahitajika uwekezaji mkubwa kwenye eneo hilo.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa, alisema ni vyema serikali ikatekeleza ushauri wa Bunge kwa haraka na kuzifanya Wizara za Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuwa na kipaumbele.

"Kuna kero ya gharama kubwa za uzalishaji kamati itaendelea kupaza sauti ya utekelezaji wa bajeti, pia itafuatilia kwa karibu mkakati wa mnyororo wa thamani, mikopo," alisema.

# Idadi vifo corona sasa yafikia 1,113

INATOKA UK. 3

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Serikali ya Jimbo la Hubei imechukua hatua kadhaa za kuwalinda wanafunzi wa kigeni dhidi ya maambukizo ya virusi na kukidhi mahitaji yao ya kila siku na mwongozo wa kisaikolojia, pamoja na kuanzisha timu maalumu kutunza wanafunzi wa kigeni, utoaji wa milo ya bure kila siku, na barakoa (masks).

Vile vile, dawa za kuua wadudu, wamepanga wafanyakazi wa China kununua nakala za matumizi ya kila siku kulingana na ombi la wanafunzi wa kigeni na ufunguzi wa simu za moja kwa moja ili kutoa msaada katika maisha ya kila siku na ushauri wa kisaikolojia.

Ubalozi huo ulisema kuwa licha ya ugonjwa huo, uchumi wa China ni imara na ina nguvu, rasilimali na uwezo wa kukabiliana na dharura.

Benki ilitengeneza mpangilio maalumu wa sera kwa kutoa mikopo ya upendeleo ya jumla ya RMB bilioni 300 (Dola za Marekani bilioni 43) kwa wafanyabiashara muhimu wanaohusika katika uzalishaji, usafirishaji au uuzaji wa vifaa muhimu vya matibabu na mahitaji ya kila siku.

"Tuna hakika kwamba China haitashinda tu vita ya kupambana na janga, lakini itapunguza athari za janga kwenye uchumi wake," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

## Wadau wa misitu waipa tano TNBC

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa sekta ya misitu wamepongeza jitihada zinazofanywa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) za kuwaleta pamoja kupitia vikao vya vikosi kazi vinavyoandaliwa na baraza hilo kujadili changamoto zilizopo na kuzifanyia kazi.

Wakizungumza baada ya Mkutano wa Kikosi Kazi cha Misitu jijini Dar es Salaam na kuongozwa na mwenyekiti wake ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, walisema kuwa wanaamini uwapo wa baraza ni kiunganishi muhimu kati ya sekta za umma na binafsi.

"Uwapo wa vikosi kazi ndani ya baraza umesaidia kupatikana kwa mawazo mbadala kutoka kwa wajumbe wanaowakilisha makundi mengi zaidi na hivyo kuongeza ufanisi ndani ya baraza," alisema Prof. Lucian Msambichaka.

Prof. Msambichaka alisema misitu ni moja ya sekta inayochangia vizuri katika viwanda na kwa kufanya hivyo Watanzania wengi na hasa vijana watapata ajira.

"Wakati umefika kwa Watanzania kuacha kulalamika na badala yake kama Taifa tujikite katika kutumia rasilimali misitu ambayo ni muhimu katika kufikia azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alieleza.

Julius Kandawala, alisema ushiriki wake katika mikutano ya vikosi kazi inayoandaliwa na baraza imekuwa na mchango mkubwa kwa wadau na Taifa kwa ujumla kuleta maana ya uwepo wake.

"Sekta binafsi kwa muda mrefu tulikuwa tukihitaji mijadala ya mara kwa mara kati yetu na wenzetu wa serikali, tunapokutana kama hivi tunaweza kujadili jambo na kutoa mapendekezo muhimu kwa ajili ya sekta husika kwa faida

# Mahiga ataka bajeti mahakama mikoa, wilaya

**Na Lydia Churi,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, ameiomba ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kutenga bajeti kwa ajili ya kamati za maadili za maofisa wa mahakama za mikoa na wilaya ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama sheria inavyozitaka.

Sheria hiyo pia inazitaka mahakama hizo kukutana na kuwasilisha taarifa zake kwa Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya kutotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria kutokana na upungufu wa bajeti. Kamati hizi ziliundwa baada ya kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mahakama Namba 4 ya Mwaka 2011.

Akizindua mwongozo wa uendeshaji wa kamati za maadili za maofisa wa mahakama leo jijini Dodoma, Waziri Mahiga alisema wizara yake itahakikisha Tume ya Utumishi wa Mahakama inapatiwa rasilimali fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zake ikiwamo Kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama kwa ufanisi unaotakiwa. Aliwataka wajumbe wa kamati hizo kuutumia mwongozo huo wa uendeshaji kuondoa changamoto mbalimbali zilizokuwapo na kuwa matarajio ya Tume na Serikali ni kuona utekelezaji wa majukumu unaozingatia matakwa ya sheria, kanuni na taratibu.

Alisema kwa kuona umuhimu wa kuimarisha dhana ya utawala bora kupitia sheria ya uendeshaji wa mahakama, serikali imeruhusu uwapo wa kamati za maadili za maoafisa wa mahakama ambazo ni pamoja; Kamati ya Maadili ya Majaji, Kamati ya Maadili ya Maofisa wa Mahakama na Kamati ya Maadili ya Mahakama ya Mkoa na Wilaya.

Kwa mujibu wa Waziri Mahiga, kamati hizi zina nafasi kubwa katika kusimamia, kuendeleza na kudumisha maadili ya utumishi wa mahakama.

Aliongeza kuwa suala la kuwapatia wajumbe wa kamati mwongozo huo ni suala la msingi kwani sasa watatekeleza majukumu yao kwa kufuata msingi wa sheria, kanuni na taratibu.

Aliwataka watumishi wachache wanaoendelea na vitendo vya ukiukaji wa maadili kuacha mara moja ili kulinda heshima ya Mhimili wa Mahakama na pia kwa usalama wa ajira zao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, akizungumza kwa niaba ya wakuu wote wa mikoa nchini, alisema kupitia mwongozo uliozinduliwa, serikali imeruhusu uwepo wa sura ya utendaji wa pamoja baina ya mihimili yote mitatu ya dola.

Alisema palipo na maadili pana amani, haki, uaminifu katika utendaji kazi, umoja na ushirikiano. Aliongeza kuwa kuwapo kwa maadili pia ni kichocheo cha maendeleo ya Taifa. Aidha, Dk. Nchimbi alisema suala la uwapo wa maadili miongoni mwa watumishi wa Mahakama ya Tanzania husaidia kuifanya mahakama kuwa rafiki na karibu zaidi na wananchi.

Kamati za Maadili za Maofisa wa Mahakama ngazi za mikoa na wilaya huongozwa na wakuu wa mikoa na wilaya, ambao hupokea na kuchunguza malalamiko dhidi Mahakimu wa Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo.



Mkuu wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, akikata utepe kuzindua duka jipya la Tigo, lililopo katika Mtaa wa Sokoni, wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Balozi Ibuge ateta na ujumbe wa SADC

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Kanali Wilbert Ibuge, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Taarifa iliyotolewa na wizara ilisema pamoja na mambo mengine, Ibuge alipokea taarifa ya ziara ya sekretarieti ya SADC na kuwahakikishia ushirikiano wa serikali ya Tanzania hususan Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kufanikisha mikutano yote ya jumuiya hiyo kipindi cha uenyekiti wa Tanzania.

Ujumbe wa Sekretarieti ya SADC unaongozwa na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa SADC, Bodo Tanrely Radaody Ravarosy, na uko nchini kwa ajili ya maandalizi ya mkutano wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa SADC.

Mkutano huo unatarajiwa kufanyika macho 10- 11, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Ujumbe huo, pamoja na mambo mengine, ulipata fursa ya kukutana na Balozi Ibue na kumpa taarifa ya maandalizi ya mkutano huo.

Agosti, mwaka jana, Rais John Magufuli alipokea rasmi uenyekiti wa SADC katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Aidha, hatua hiyo ilifuatiwa na mikutano mbalimbali ya kisekta iliyofanyika na inayoendelea kufanyika nchini kwa kipindi cha kuanzia Septemba, mwaka jana hadi Agosti, mwaka huu, ambapo hadi sasa imeshafanyika mikutano mitatu ya kisekta.

Mikutano hiyo ni pamoja na ya Mawaziri wa SADC wenye dhamana ya masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama), habari, uchukuzi na hali ya hewa, mkutano wa pamoja wa mawaziri wa sekta ya afya na ukimwi pamoja na mkutano wa mawaziri wa mazingira, maliasili na utalii.

## Waziri azuia mifuko mbadala bila viwango

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amepiga marufuku uingizwaji na utengenezaji wa mifuko mbadala ambayo haijakidhi viwango vilivyowekwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Zungu alisema utafanyika msako nchi nzima kuwasaka wasambazaji na watengenezaji ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

"Uchunguzi wetu unaonyesha wapo wafanyabiashara wasio waaminifu kutoka nchi jirani ambao wamekuwa wakishirikiana na wafanyabiashara wa hapa nchini kuhujumu mapato ya serikali kwa kufanya biashara hiyo kwa njia za magendo. Tumeweka mipango yetu ya kushughulika na wahujumu hao wa uchumi wa nchi," alisema.

Alisema licha ya kuingiza mifuko hiyo kwa njia za magendo, ubora wa bidhaa hizo umekuwa ni hafifu na usiokidhi vigezo vilivyowekwa ili kuyafanya mazingira yanakuwa salama nchini.

"Wafanyabiashara hao wamekuwa wakiingiza au kuzalisha mifuko ambayo haina nembo za mzalishaji, nembo ya shirika la viwango pamoja na ubora wa GSM 70, hivyo inatulazimu kuchukua hatua kali ili kulinda viwanda vya ndani ambavyo bidhaa zake zimekuwa zikipata ushindani," alieleza.

Aliwaonya Watanzania kuacha kutumia mifuko mbadala ambayo haina vigezo vilivyokubaliwa kwani ni hatari kwa afya zao.

"Mifuko hii haikubaliki na haifai kutumika kama vifungashio vya bidhaambalimbali kwa kuwa haijaidhinishwa na kuthibitishwa na shirika la viwango nchini hivyo ni rahisi kupata madhara ya kiafya na hata kuzidi kuleta athari zingine katika mazingira yetu," alisema Zungu.

Aliongeza kuwa hatakubali kuwa sehemu ya watu wanaoweza kumwangusha Rais John Pombe Magufuli hasa kufuatia maamuzi ya serikali ya upigaji marufuku wa matumizi ya mifuko ya plastiki nchini.

"Mwezi wa sita mwaka jana, serikali ilipiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilikuwa imetapakaa na kuleta kadhia kubwa katika mazingira, marufuku hiyo ndiyo ikapelekea kuzalishwa kwa mifuko mbadala, sasa tunapowaona wenzetu wanataka kutumia fursa hiyo vibaya inabidi tuwe wakali wa kusimamia sheria kanuni na taratibu zilizowekwa," alifafanua.

# Vijana watumika kudhibiti nzige

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MKUU wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, amesema serikali ya wilaya imeandaa vijana 50 kila kata kuzunguka vijijini kufuatilia kama kuna uvamizi wa nzige ambao wameripotiwa kuingia katika maeneo kadhaa kutokea Kenya.

Vijana hao wanafanya kazi hiyo sambamba na timu ya wataalamu ili kufanya uchunguzi dhidi ya madai ya wadudu hao kukaribia eneo hilo.

Akizungumza na Nipashe juzi kwa njia ya simu, Apson alisema tayari amewasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Taveta nchini Kenya, kupata taarifa za awali kama nzige hao wamekaribia mpakani na kwamba amemthibitishia kwamba hakuna nzige waliokaribia Taveta.

"Hatujachukulia mzaha maneno yanayoendelea katika mitandao ya kijamii, tumeandaa vijana 50 kila kata kwenye wilaya yetu ambao hivi sasa wanazunguka huku na huko vijijini kuona kama kuna nzige wameingia na kutoa taarifa haraka wilayani," alisema.

Juzi, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema wamepokea taarifa hiyo kutoka wilayani humo na kwamba timu ya wataalamu imejipanga vyema kukabiliana na wadudu hao waharibifu wa mazao.

"Ndege za kupulizia dawa ziko tayari, tumeandaa watu, dawa na wananchi. Tukisikia tu wamekaribia eneo letu tutaanza kupuliza. Tumetuma wataalamu wa kutosha kwenye mipaka yetu," alisema Waziri Hasunga.

Wiki iliyopita, Waziri Hasunga alisema viuatilifu maalum vya kudhibiti nzige, zikiwamo lita 7,000 na wataalamu wako kwenye mipaka ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mara.

Nzige hao walianza kusambaa wakitokea nchini Ethiopia na kwenda Somalia na baadaye walingia Kenya na kuathiri majimbo matano, licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa.




Mafundi wakiendelea na upanuzi wa Barabara ya Morocco-Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zahanati Kigoma zatakiwa kupunguza vifo vya uzazi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, ameagiza zahanati zote mkoani hapa kutoa huduma bora za afya ya uzazi ili kupunguza idadi ya vifo vya kinamama.

Akizungumza wakati alipotembelea zahanati ya Bangwe na Kigoma katika Halmashauri ya Kigoma Ujiji, Dk. Chaula alisema asilimia 80 ya wanawake wanaojifungua hawana matatizo makubwa na kuwa ndiyo maana baadhi yao wanajifungulia nyumbani na wanakuwa salama.

"Asilimia 20 ndiyo wana matatizo ambayo yanahitaji uangalizi mkubwa na ndiyo maana tunataka wajawazito wajifungulie hospitali ili mwenye matatizo aweze kutambuliwa mapema na kupewa huduma inayostahili," alisema.

Aliwataka watoa huduma katika zahanati hizo kuwa karibu na wajawazito wanaotaka kujifungua, hatua itakayosaidia kuelewa maendeleo yao na kama itabainika viashiria vya tatizo la kiafya ni vyema rufani ikatolewa mapema ili mgonjwa apelekwe ngazi nyingine yenye uwezo zaidi. "Mama anahangaika na uchungu mpaka roho inataka kutoka na hasikilizwi matokeo yake anajifungua mtoto anakufa au mtoto mwenye matatizo ya akili, hii tabia ife maana lengo la serikali ni kuhakikisha mama anayejifungua anakuwa salama na mtoto pia," alisema.

Kwa upande wake Diamon Sadick ambaye pia anatoka katika wizara hiyo, alisema kwa miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2020 wizara inatumia mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF) unaolenga kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

"Mpango huu unaoanzia ngazi ya zahanati, kituo cha afya na hospitali, unaendelea kunufaisha mikoa tisa nchini ambayo ilibainika kuwa na idadi kubwa ya vifo ikiwamo minane ya Kanda ya Ziwa na mkoa mmoja wa Pwani," alisema Sadick.

Alisema fedha hizo hutolewa kulingana na uhitaji ili kuhakikisha lengo lake linatimia pamoja na kutoa motisha kwa wafanyakazi baada ya kujiridhisha kuwa wanastahili, kutokana na kuongeza ufanisi wa kazi.

"Ili kupata fedha za RBF ni lazima walengwa wawajibike kuboresha huduma kwa kuzingatia ubora na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa," aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Tiba kutoka katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Magembe, alizitaka zahanati kujiwekea malengo ya kuongeza ubora katika aina ya huduma wanazozitoa ili kuwezesha kufikia hadhi ya nyota tatu au nne katika utoaji wa huduma.

Magembe alisema, ili kulifanikisha hilo zinahitajika nguvu za mtumishi mmoja mmoja kujiwekea malengo ya kuboresha utoaji wa huduma, kisha kuwa na malengo ya pamoja ambayo yataongeza ufanisi hasa katika utendaji kazi.

Mganga Mfawidhi katika Zahanati ya Kigoma, Godlove Mayinga, alisema kuwa gawio la fedha RBF kwa mwaka 2017 na 2018 lilikuwa Sh. milioni 27.4 ambazo walizitumia kuboresha utoaji huduma wa zahanati na kusaidia kupandisha hadhi yake kutoka nyota moja hadi mbili.

# Fursa ujenzi mradi bomba la mafuta

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara, Chelestino Mofuga amewataka wananchi wa wilaya hiyo kuchangamkia fursa za kibiashara kwenye mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Tanga hadi nchini Uganda. Mofuga aliyasema hayo juzi wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

Alisema wananchi wa Mbulu wanapaswa kuchangamkia fursa mbalimbali za uwapo wa mradi huo unaopita katika Mkoa wa Manyara, ikiwamo kufanya biashara tofauti. Alisema mradi wa bomba hilo la mafuta kutoka jijini Tanga hadi Hoima nchini Uganda, kwenye Mkoa wa Manyara, litapitia kwenye wilaya mbili za Kiteto na Hanang'.

"Tuwape elimu wananchi wetu wachangamkie fursa zitakazojitokeza kwenye mradi huo, ili wasiwe watazamaji huku wakiwaachia wajasiriamali wengine wafaidi wakati uwezo wa kuchangamkia fursa wanao," alisema Mofuga.

Alisema kila kambi ya ujenzi wa bomba hilo itakuwa na watu 2,000 hivyo ni wakati sahihi wa kuchangamkia nafasi hiyo kwa kufanya biashara ya vitunguu na kuku badala ya kuwa watazamaji. "Tuwaandae wananchi wetu wapate elimu ya ufanikishaji hilo kwa kuwa na bidhaa bora na tutawaita wataalamu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ili wawape elimu zaidi," alisema Mofuga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Hudson Kamoga, alilieleza baraza hilo kuwa ujenzi wa miradi ya hospitali mpya ya wilaya na jengo la utawala wa halmashauri hiyo inaendelea vizuri.

"Tunamshukuru Rais John Magufuli kwa kutupatia fedha mbalimbali za miradi hiyo ikiwamo za hospitali mpya na makao makuu mapya ya halmashauri katika Kata ya Dongobesh," alisema Kamoga. Diwani kutoka Tarafa ya Dongobesh, Elimiana Shishi, alisema atatumia nafasi hiyo kwa kuwaeleza wananchi wa eneo hilo kuchangamkia fursa ya ujenzi wa bomba hilo la mafuta.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kushoto), akizungumza na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, kuhusu masuala ya ulinzi na usalama, baada ya kuwasili jijini humo jana, kwa ziara ya kikazi. **PICHA: WMNN**

# Muro awageukia wazazi wapiga porojo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amewaagiza wazazi wilayani humo kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni, badala ya kutumia muda mwingi kwenye masuala yasio na tija na kupiga porojo kwenye simu za viganjani.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wazazi kwenye shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Tumaini Mission iliyopo Kata ya Imbaseni, wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Muro alisema, wazazi wengi siku hizi wanatumia muda mwingi kwenye simu za mkononi na kusahau majukumu ya kuwalea watoto wao, hali inayochangia kuharibika kwa watoto hao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Hebu tujitafakari kwanini watoto wetu wanaharibikia, halafu kesho tunalaumu walimu, hii siyo sawa tupunguze matumizi ya mambo yasio na tija au kupiga umbea kwenye simu zetu haitusaidii," alisema.

Muro alisisitiza umuhimu wazazi kufuatilia taarifa za watoto wao shuleni ili anapofanya uzembe, mzazi anagundua mara moja na kuwasiliana na walimu.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Namnyaki Leng'ida, alisema, shule hiyo ilianza rasmi mwaka 2012 ikiwa na wanafunzi 16 na hadi sasa ina 298 na inafanya vizuri katika mitihani ya kata, wilaya, ujirani mwema na taifa kwa ujumla.

Namnyaki alisema, shule hiyo inafadhiliwa na marafiki kutoka nchini Denmark, jumla ya watoto 100 wanaotokea katika mazingira magumu wanaofadhiliwa, huku wengine wakichangia gharama kwa ajili ya uendeshaji wa shule hiyo. Alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitabu vya kufundishia kutambua kipi ni kitabu cha Kiada na Ziada na kuomba kupatiwa ufumbuzi wa suala hilo.

Kwa upande wa Mfadhili wa shule hiyo kutoka nchini Denmark, Torkild Jensen alisema, wanasaidia watoto wanaotokea mazingira magumu katika kuhakikisha wanapata elimu iliyo sawa na wengine.

Pia alisema wanasaidia shule zingine katika kuhakikisha wanainua kiwango cha elimu nchini.

# Wanafunzi 36 wasaidiwa kuendelea masomo

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, imewasaidia wanafunzi 36 wa shule za sekondari wanaoishi katika mazingira hatarishi kuendelea na masomo yao.

Makamu Mwenyekiti mstaafu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Albert Msole, aliyasema hayo jana wakati akielezea mafanikio na changamoto kwenye miaka minne aliyoongoza kamati ya kudhiti Ukimwi katika wilaya hiyo.

Msole alisema kati ya wanafunzi 36, watatu walifanikiwa kufikia hatua ya chuo kikuu na wanaendelea na masomo hayo hadi hivi sasa.

Alisema hali ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwenye wilaya hiyo imepungua kutoka asilimia tatu mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 2.8, mwaka huu lengo likiwa kufikia malengo ya taifa asilimia 90 kwa mwaka 2020, kupunguza maambukizi kwa wanaotumia dawa.

"Tutafikia asilimia 90 kwa kupima maambukizi, asilimia 90 watakaokuwa na maambukizi kutumia dawa na asilimia 90 ya wote wanaotumia dawa," alisema.

Pia, alisema wamewafikia na kuhamasisha wananchi 36,670 wakiwamo wanaume 21,711 na wanawake 14,266 kupima hali zao za maambukizi, watu 373 walikutwa na VVU na wameanza kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo.

Alisema Simanjiro inaongoza kwenye Mkoa wa Manyara kwa jamii kuitikia upimaji, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Kiteto, Babati mjini, Hanang' na Mbulu mjini.

"Tunakabiliwa na changamoto katika kupambana na Ukimwi na upungufu wa rasilimali kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kamati ya kupambana na janga la Ukimwi," alisema Msole.

Pia, alisema baadhi ya vijana wa jamii ya wafugaji, wanaosafiri nchi za jirani au mikoa mbalimbali, hawajikingi na maambukizi mapya ya Ukimwi kwa kuwa wakirudi nyumbani kwao huwaambukiza wenza wao.

Alidai changamoto ya baadhi ya wachungaji, mitume na manabii wa madhehebu mbalimbali wanaohubiri dini zao, huwaambia waumini wao wenye maambukizi ya Ukimwi watupe dawa za kufubaza Ukimwi (ARV) kwa madai watapona kwa imani.

"Walioathirika na VVU wanapata wakati mgumu kuendelea vizuri kiafya kutokana na wahubiri hao kuwahamasisha waumini wao kuwa Mungu anaponya hivyo watupe dawa za ARV," alisema.

Alisema elimu inapaswa kuendelea kutolewa kwenye eneo hilo la wafugaji ambalo bado uelewa ni mdogo hivyo kuzidi kupoteza nguvu kazi ya taifa.



## Serikali yatoa mil. 500/- kukarabati FDC

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

SERIKALI imekikumbuka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Mamtukuna (FDC) kilichopo Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, baada ya kupeleka Sh. milioni 500 za kukarabati upya majengo na miundombinu yake.

Chuo hicho kilikuwa katika hali mbaya kutokana na uchakavu wa majengo na miundombinu, jambo ambao lilikuwa likitishia usalama wa wanafunzi wake.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imechukua uamuzi huo wa kukikarabati chuo hicho na kukifanya kuwa kipya ili kuvutia idadi kubwa ya vijana wanaoshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kujiunga na chuo hicho kuanzia mwaka ujao.

"Wilaya ya Rombo tunayo bahati kubwa, hivi sasa Wizara ya Eimu, Sayansi na Teknolojia imetuletea fedha za kutekeleza miradi miwili ya elimu ambayo ni ujenzi wa ofisi za udhibiti ubora wa shule, kiasi cha Sh. milioni 152 na Sh. milioni 500 za kukifanya upya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mamtukuna," alisema.

Alisema serikali ipo mstari wa mbele kuwaletea wananchi wa Rombo maendeleo kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali katika sekta za elimu, afya, barabara na umeme bila kujali itikadi, rangi, dini wala ukabila.

Chuo hicho ni miongoni mwa vyuo ambavyo serikali imeweka nguvu katika kukuza ujuzi na stadi za ajira.

Ukarabati huo utasaidia kuongeza nguvu zaidi katika kutekeleza vipaumbele vya serikali vilivyoainishwa katika mkakati wa serikali wa kufikia Tanzania ya viwanda ifikapo 2025, pia kuwezesha vijana kupata ujuzi kwa vitendo kuliko nadharia pamoja na kujengea uwezo vyuo vya kati.

Katika hatua nyingine, Hokororo aliwataka wadau wa elimu kutoiona Ofisi ya Udhibiti Ubora wa shule kama washtaki, bali wafanye kazi kwa kushirikiana kunyanyua kiwango cha elimu na ufaulu kwa wilaya hiyo, hasa kwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

# Wananchi Siha kupata huduma bure usafishaji ukungu macho

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

JOPO la madaktari bingwa wa macho kutoka hospitali mbalimbali nchini, kwa kushirikiana na Hospitali ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, imetangaza kuanza kwa huduma ya upasuaji na usafishaji wa ukungu kwenye mboni ya jicho.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo (DMO), Dk. Andrew Method, alisema huduma nyingine zitakazotolewa bure na mabingwa hao ni pamoja na kupima index ya molekuli ya mwili na shinikizo la damu.

Dk. Method alikuwa akizungumza jana na Nipashe wilayani hapa kuhusu huduma hiyo itakayoanza kutolewa bila malipo kati ya Februari 15 hadi 16, mwaka huu katika Hospitali ya wilaya hiyo mji mdogo wa Sanya Juu.

"Ni kweli tumepata ufadhili wa kutoa huduma hiyo baada ya Kampuni ya Africado Limited inayozalisha parachichi, Lions Club ya Dar es Salaam na Lions Club ya Moshi/Kilimanjaro.

Nyingine ni PKF na Hospitali ya Wilaya ya Siha na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro, kuwaleta madaktari hao kufanya uchunguzi wa macho kwa wananchi wa Siha," alisema Dk. Method.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu huyo, huduma nyingine zitakazotolewa ni pamoja na kupima macho, kisukari, ushauri wa lishe kwa wagonjwa wa kisukari.

"Tunawaomba wagonjwa wa aina hii wafike Hospitali ya Wilaya ya Siha kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni kwa ajili ya uchunguzi zaidi," alisema Dk. Method.

Hospitali ya Wilaya ya Siha, inahudumia wakazi zaidi ya 116,313 (kulingana na takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012), kutoka katika vijiji 60 vilivyopo wilayani humo.

Hospitali hiyo ilianzishwa mwaka 2007 ikiwa kama kituo cha afya, baada ya vyama viwili vya ushirika wilayani humo kutoa ekari 40 za ardhi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kushoto) na Meneja Mkuu wa Chuo cha Kilimo Kilacha Moshi, Jerome Silayo, wakionyesha mikataba baada ya kusaini makubaliano chuoni hapo, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana, ambapo SBL, itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 kutoka katika jamii za wakulima kila mwaka kwa kuwalipia ada kwenye vyuo vya kilimo kwa kipindi chote cha masomo yao. **PICHA: JAMES LANKA**

# Aomba wizara idhibiti nzige kuingia nchini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU chache baada ya serikali kupeleka wataalamu wake katika wilaya zote zilizopo mipakani kuchunguza iwapo kuna uvamizi wa nzige, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, amesema Wizara ya Kilimo lazima ihakikisha wadudu hao hawaingii, kwa kuwa madhara yake ni makubwa kiuchumi.

Boisafi aliyasema hayo jana mjini hapa, wakati akizungumza na viongozi wa mbalimbali wa kisiasa.

"Tuiombe sana Wizara ya Kilimo itusaidie kuhakikisha wadudu hao waharibifu wa mazao wasiingie nchini kwetu na hasa Mkoa wa Kilimanjaro ambao uko mpakani mwa Tanzania na Kenya.

"Ile taharuki iliyojitokeza wiki iliyopita kutokana na kuwapo kwa baadhi ya taarifa ambazo hazikuthibitishwa na wataalamu, imetupa nguvu ya kujipanga na kuiagiza serikali kuwa makini wakati wote kuzuia nzige wasijaribu kupenya na kuja kwetu kwa sababu madhara yake ni makubwa kiuchumi achilia mbali kusababisha njaa."

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, alisema katika kukabiliana na uvamizi wa nzige, tayari serikali wilayani humo imeandaa vijana 50 kila kata kuzunguka vijijini kufuatilia kama kuna uvamizi wa wadudu hao.

"Tumeandaa vijana 50 kila kata kwenye wilaya yetu ambao hivi sasa wanazunguka vijijini kuona kama kuna nzige wameingia na kutoa taarifa haraka wilayani," alisema.

Pia Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alinukuliwa akisema timu ya wataalamu iliyopelekwa mipakani imejipanga vyema kukabiliana na wadudu hao waharibifu wa mazao.

"Ndege za kupulizia dawa zipo tayari, tumeandaa watu, dawa na wananchi. Tukisikia tu wamekaribia eneo letu tutaanza kupuliza. Tumetuma wataalamu wa kutosha kwenye mipaka yetu," alisema Waziri Hasunga.

Wiki iliyopita, Waziri Hasunga alisema viuatilifu maalum vya kudhibiti nzige, jumla ya lita 7,000 na wataalamu wapo kwenye mipaka ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Mara.

Nzige hao walianza kusambaa wakitokea nchini Ethiopia na kuelekea Somalia na baadaye waliingia Kenya na kuathiri zaidi majimbo matano, licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa.

ama
ALHAMISI FEBRUARI 13, 2020
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**SIKU YA UKEKETAJI**
**Yanayojificha yaibuliwa upya hadharani**



**LINI CORONA ITAKOMA?**

Ukurasa 19

Rais Trump, wataalamu dunia kila mmoja anabashiri lake



Ukurasa 14

**KAMPENI TUMEBORESHA AFYA**

# TMDA yatamba ufanisi wa 90%



# Balozi wa China: Uamuzi wa busara wanafunzi Watanzania kubaki Wuhan

Ukurasa 16




Monica Dongban-Mensem, akiwa kazini barabarani. **PICHA: MTANDAO.**

# Ajali iliyoua mwanawe yamgeuza trafiki

**ABUJA,** Nigeria

WAKATI anapokuwa na muda wa ziada, hakimu mstaafu Monica Dongban-Mensem, huongoza magari barabarani katika mji mkuu, Abuja, katika majumu sawa na Polisi wa Usalama Barabarani. Ni miaka minane tangu mwanawe wa kiume kufa kwa kugongwa mna gari.

Hajui ni nani aliyehusika na kifo cha mwanawe, lakini anataka kukabiliana na baadhi ya uendeshaji mbaya wa magari anaoushuhudia na alianza kwenda kwenye vituo vya magari kuongea na madereva juu ya usalama barabarani, nchini Nigeria.

Alichobaini na kumshitua ni kwamba, kuna madereva wengi hawakuwa wamepata mafunzo sahihi ya sheria za barabarani, hivyo hawaendeshi kwa usahihi magari.

Akiwa na umri wa miaka 62, ameanzisha shirika lisilo na faida lililopewa jina la marehemu mtoto wake 'Kwapda'as Road Safety Demand ' kuwaelimisha madereva usalama, pia amepanga kuanzisha shule ya uendeshaji magari kwa madereva wanaoendesha magari ya kibiashara, wanakoweza kupata mafunzo hayo bure.

Lakini bado hakuridhika, Hakimu Dongban-Mensem alitaka kushiriki katika kudhibiti uendeshaji wa magari mwenyewe na baada ya wiki kadhaa za mafunzo ya Tume ya Usalama Barabarani, alipata ujuzi wa kuongoza magari.

AFYA

## KAMPENI TUMEBORESHA SEKTA AFYA

# TMDA yatamba ufanisi wa 90%

• Mkurugenzi: Bidhaa feki 'zayeyuka' • Mipakani 'stop'dawa, vifaa tiba feki • Mageuzi kuhamia digitali; maabara kisasa



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo (wa tatu kushoto) akipatiwa maelezo na watalaamu wa ukaguzi wa viwanda, ndani ya moja ya kiwanda kinachojengwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), wakala mpya kutoka iliyojulikana kama Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vifaa Tiba (TFDA).

Hivi sasa majukumu ya udhibiti chakula na vipodozi yamehamishiwa katika Shirika la Viwango Tazania (TBS), hatua inayotokana na mabadiliko ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi mwaka 2019.

Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na taasisi zote zilizopo chini yake, inaendelea na ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji huduma, kutathmini mafanikio yaliyopatikana hadi sasa.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara ya Afya, Gerald Chami na maofisa mawasiliano wa taasisi zote zilizopo chini ya wizara hiyo, wanafanya ziara kupitia kampeni iliyopewa jina 'Tumeboresha Sekta ya Afya.'

> **Lengo ni kujihakikishia kuwa bidhaa hizi zinaendelea kuwa ni bora, salama zenye ufanisi baada ya usajili na kuruhusiwa kuingia kwenye soko.**

Hapo ndipo 'mguu' wa ziara unafika katika makao makuu ya TMDA, jijini Dar es Salaam, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa kuangaza mafanikio yake.

**BOSI TMDA**

Katika ofisi za TMDA jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Adam Fimbo, anakaribisha ugeni kwa majigambo ya kuongeza idadi ya vibali vya kuingizaji na kutoa bidhaa nje ya nchi.

Hapo anataja takwimu, kuwa ni kutoka vibali 13,018 kwa mwaka 2015/16 hadi vibali 26,478 mwaka 2018/19 sawa na ongezeko la asilimia 203.

Fimbo anasema, mafanikio hayo yametokana na kuwapo mfumo wa kieletroniki katika utoaji vibali vya kuingiza na kutoa bidhaa nchini, unaowezesha wateja kutuma maombi, kufanya malipo popote walipo, hatimaye kupata kibali ndani ya saa 24.

Awali huduma hiyo ilitolewa kwa mfumo wa 'analogi' kwa ujazaji fomu kwa mkono na wateja walilazimika kufika ofisini, hali anayosema imechelewesha mchakato wa utoaji huduma.

"Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali TMDA ambayo awali ilikuwa TFDA, tumefanikiwa kuboresha huduma hasa za utoaji wa vibali, baada ya kuwa na mfumo huu mpya unaotoa huduma kisasa," anafafanua Fimbo.

Anaeleza, pia mamlaka hiyo imefanikiwa kupunguza idadi ya bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi ya binadamu, baada ya kuboresha utendaji kazi.

KAMPENI UBORA

Hapo tena Fimbo anataja takwimu, kutoka tani 140,705 za mwaka 2017/18 zilizokuwa na thamani ya Sh. milioni 22.394 hadi kufika tani 664 mwaka wa fedha 2018/19.

"Hii inaashiria kupungua bidhaa zisizokidhi viwango katika soko la Tanzania, kutokana na kazi kubwa inayofanywa na mamlaka za kudhibiti uingizaji," anasema Fimbo.

Katika kuhakikisha kwamba, bidhaa hizo haziwarudii walaji au watumiaji tena, hivi sasa wameongeza kazi ya kuteketeza bidhaa zisizokidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi,

Fimbo anasema mpango wa ufuatiliaji ubora wa bidhaa katika soko, kuna jumla ya sampuli 1,136 za dawa za binadamu zilifuatiliwa na kuchunguzwa katika kipindi cha miaka minne na asilimia 96 zilendelea kukidhi vigezo vya ubora.

Sambamba na hilo, anaeleza kati ya sampuli 144 za dawa za mifugo zilizochunguzwa katika kipindi hicho, asilimia 90 zinaendelea kukidhi vigezo vya ubora.

Fimbo anasema TMDA, imeweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na vifaa tiba, ili kutambua, kutathimini na kuzuia madhara yasiyovumilika yasitokee kwa wananchi.

Anaeleza kwamba, wameanzisha mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa taarifa za madhara yatokayo na matumizi ya dawa kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta na njia ya kutuma ujumbe wa simu.

Kuhusu mipango na malengo yao, anasema wanadhamiria kujenga maabara kubwa na ya kisasa, katika ofisi za makao makuu jijini Dar es Salaam na makao makuu ya nchi, jijini Dodoma, ili kuboresha utendaji kazi wa mamlaka hiyo.

Anaeleza litakuwa jengo kubwa la ghorofa saba, yenye maabara kubwa na ya kisasa, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya kutosha.

**TMDA KASKAZINI**

Meneja wa TMDA Kanda ya Kaskazini, Proches Patrick, anaelezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho, walitoa jumla ya vibali 1,160 vya kuingiza bidhaa na dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika kipindi cha miaka minne.

Anasema kuna jumla ya shehena 3,160 za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ilikaguliwa katika vituo vya forodha katika kipindi cha

AFYA

# TMDA yatamba ufanisi wa 90%

miaka hiyo.

Patrick anasema, vibali vilivyotolewa katika kipindi hicho ni matokeo ya elimu wanayotoa ya udhibiti kwa wadau, hivyo inawafanya kutii sheria bila ya shuruti, kama inavyoelekeshwa na sauti ya dola.

"Muda uliokuwa unatumika kuchakata maombi nao umepungua hadi kufika siku moja, hivyo kuongeza ufanisi na kupunguza malalamiko kutoka kwa wateja," anaeleza Patrick.

Kuhusu shehena zilizokaguliwa kwa kipindi hicho, anasema zimetokana na kuimarisha utoaji huduma katika vituo vya forodha vya mipaka ya anavyovitaja kuwa ni Namanga, Tarakea na Holili (mpakani na Kenya) na katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA).

Meneja huyo anafafanua kuwa, maabara yake imechukua jumla ya sampuli 243 za dawa na kupima ubora, usalama na ufanisi wake, kwa kutumia maabara inayohamishika na sampuli zote zilifaulu.

Anasema, inapotokea sampuli haijafaulu maabara, sampuli huchukuliwa, ikiwamo kuondoa dawa husika sokoni kwa matoleo yasiyokidhi vigezo.

Patrick anasema, pia wanafanya ukaguzi kwenye maneo ya famasi, maduka ya dawa muhimu (DLMD), maghala hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Anasema katika kipindi cha miaka minne iliyopita, kuna jumla ya maeneo 5,017 yaliyokaguliwa katika halmashauri 21 wanazosimamia.

Pia, kuna watendaji wa sekta za afya 858 kutoka vituo 152 waliopewa mafunzo kuhusu utoaji taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

"Taarifa za za madhara yatokanayo na huduma hizo hupokewa moja kwa moja na ofisi ya TMDA na baada ya kuchakatwa, huingizwa kwenye kanzidata inayojulikana kama 'vigiflow," anasema Patrick.

### KANDA ZIWA

Sophia Mziray, Meneja wa TMDA Kanda ya Ziwa, anasema wana jukumu la kusimamia na kuetekeleza udhibiti kwenye maeneo ya ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, katika mikoa sita na halmashauri zake.

Anataja mikoa hiyo iliyogawanywa katika kanda mbili; Kanda ya Ziwa Magharibi, ikijumuisha mikoa ya Mwanza, Geita, Kagera na Kanda ya Ziwa Mashariki yenye mikoa ya Simiyu, Mara na Shinyanga.

Anasema katika kipindi cha miaka minne sasa, TMDA Kanda ya Ziwa, wamefanikiwa kukagua majengo 2,043 ya biashara za dawa, vifaa tiba na vitendanishi yaliyosajiliwa na kupewa vibali vya kufanya biashara.

Sophia anasema, TMDA iliyathibitisha kuwa kama yanakidhi vigezo vya utunzaji, usambazaji, uuzaji na utengenezaji bidhaa hizo.

Anasema sasa wameweka wakaguzi wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusu mzigo kuingia au kutoka nje ya nchi.

"Lengo ni kuharakisha uingiaji na utoaji wa mizigo katika vituo vya forodha vya mipaka ya Sirari(Mara), Mtukula (Kagera) na Bandari ya Mwanza Kusini," anasema Sophia.

Kwa mujibu wa meneja huyo, jumla ya shehena na mizigo 6,668 ya dawa vifaa tiba na vitendanishi vilikaguliwa katika vituo vya forodha 10 vya Mtukula, Rusumo, Mulongo, Kabanga, Bandari ya Mwanza, Bandari Musoma, Bandari kavu ya Isaka na Kemondo.

Anasema pia wanafuatilia ubora wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika masoko kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo katika maduka ya jumla na rejareja, hospitali, vituo vya afya, zahanati na maghala yanayohifadhi bidhaa hizo na kuchukua sampuli za bidhaa hizo kwenye soko na kuzifanyia uchunguzi wa kimaabara.

"Lengo ni kujihakikishia kuwa bidhaa hizi zinaendelea kuwa ni bora, salama zenye ufanisi baada ya usajili na kuruhusiwa kuingia kwenye soko," anasema Sophia.

Pia, anafafanua kuwa, katika kipindi cha miaka minne sasa, jumla ya maeneo 3,501 yalikaguliwa katika mikoa yote sita ya Kanda ya Ziwa na maeneo 2,898 yalikidhi vigezo na kusajiliwa sawa na asilimia 82.77.

Sophia anasema, katika kipindi hicho wameona kupungua bidhaa zisizokidhi vigezo vya ubora katika masoko na mwaka 2017/18 jumla ya tani 1,067.48 zenye thamani ya Sh. bilioni mbili ukilinganisha na tani 53.75 zenye thamani ya Sh.milioni 594 ziliteketezwa mwaka 2018/19.

Anafafanua kwamba, jumla ya sampuli 1,136 za dawa za binadamu zilifuatiliwa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara katika kipindi hicho na asilimia 96 zilienndelea kukidhi vigezo vya ubora.

Pia, anataja kati ya sampuli 144 za dawa za mifugo zilizochunguzwa, asilimia 90 ziliendelea kukidhi vigezo vya ubora na kuwa ufaulu kunathibitisha kuwa dawa zilizoko kwenye soko ni bora, salama na zenye ubora.

Anasema kupitia maabara zinazohamishika zilizowekwa na TMDA katika Hospitali ya Rufani ya mikoa ya Kanda ya Ziwa na vituo vya forodha, kuna jumla ya sampuli 243 zilifanyiwa uchunguzi na zote zilifaulu vigezo vya ubora.

Anaeleza kwamba, pindi inapotokea sampuli haijafaulu hatua stahiki huchukuliwa haraka ikiwa ni pamoja na kuondoa matokeo ya dawa husika kwenye soko.



Ofisa Mwandamizi wa Ukaguzi wa Kanda ya Ziwa wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Bugaru Nyamweru, akionyesha maabara za uchunguzi ambazo serikali imewekeza Sh.bilioni Saba.

> "Taarifa za madhara yatokanayo na huduma hizo hupokewa moja kwa moja na ofisi ya TMDA na baada ya kuchakatwa, huingizwa kwenye kanzidata inayojulikana kama 'vigiflow.



Akida Khea, kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), alipofafanua kwa waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu dawa, vifaa tiba, vitendanishi, dawa asili na tiba mbadala, jijini Dar e Salaam, Novemba.

AFYA

# Balozi wa China: Uamuzi wa busara wanafunzi Watanzania kubaki Wuhan

• Muhimu tahadhari, hakuna sababu ya kuhofu



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Wuhan, China, katika moja ya mahafali yao. **PICHA: MITANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na hofu ya kiafya, kuhusiana na kuwapo msambao wa maradhi ya corona kumefanyika mazungumzo ya ana kwa ana na Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke, kuhusu mlipuko mpya wa virusi vya corona, mnamo tarehe 7 mwezi huu. Ifuatayo ni mazungumzo hayo:

Swali: Tangu kuzuka kwake mnamo Desemba 2019, virusi vipya vya corona vimeambukiza zaidi ya watu 28,000 na kuenea katika zaidi ya nchi 20. Je, tunapaswa kuwa na wasiwasi na hofu?Jibu: Mlipuko mpya wa virusi vya corona umekuwa tatizo la pamoja ulimwenguni. Kwa kuwa maambukizi yake ya kwanza yaligunduliwa, huko Wuhan, mji mkubwa wenye idadi ya watu milioni 11 katikati ya China, Jimbo la Hubei, virusi vimekuwa vikienea kwa kasi zaidi ya vile ilivyotarajiwa. Hadi kufikia saa sita usiku, Februari 6, kesi 31,161 zilizothibitishwa na kesi 26,359 zilizoshukiwa ziliripotiwa China na vifo 636 na kesi 1,540 za wagonjwa waliopona. Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO), kufikia tarehe 5 Februari, nchi 24 zimeripoti jumla ya kesi 216 zilizothibitishwa na kifo kimoja tu.Kukabiliwa na changamoto kubwa kama hiyo, watu wa China hawajavunjika moyo. Tangu kuzuka kwa virusi vipya, serikali ya China imekuwa ikichukua hatua kamili na kali za kuzuia na kudhibiti na hisia kubwa za uwajibikaji kwa afya ya watu, hatua hizi nyingi zinaenda vizuri zaidi ya mahitaji ya kanuni za afya za kimataifa.Serikali ya China ilitoa maagizo maalumu kwa Mji wa Wuhan; hospitali mpya zimejengwa huko Wuhan, ili kuongeza zaidi uwezo wa kiafya wa ndani; likizo ya Mwaka Mpya wa Kichina imeongezwa, ili kuweka uhamiaji wa kitaifa katika kiwango cha chini; majimbo na manispaa 31, ikiwamo Beijing na Shanghai.

> **Kwa sasa, tahadhari za hali ya juu za dharura zimekamilishwa kote China na hatua kali za afya ya umma zimechukuliwa kutambua, kugundua na kujitenga na maambukizo au kesi zinazoshukiwa mapema.**

Pia, zimechukua hatua za kukabiliana na kiwango cha kwanza kwa dharura hii kubwa ya afya ya umma. Kwa sasa, tahadhari za hali ya juu za dharura zimekamilishwa kote China na hatua kali za afya ya umma zimechukuliwa kutambua, kugundua na kujitenga na maambukizo au kesi zinazoshukiwa mapema.Kwa zaidi, China imekuwa katika mawasiliano ya karibu na ushirikiano na Shirika la Afya Duniani (WHO) na nchi zingine, ikitoa habari kwa njia ya wazi na kushiriki mlolongo wa maumbile ya virusi na jamii ya kimataifa. Juhudi za China za kudhibiti janga hilo zimeleta habari za kutia moyo. Kwanza, kesi za waliopona zimezidi walio kufa kwa idadi kubwa. Kwa mfano, mnamo 5 Februari wagonjwa 261 walipona na kuruhusiwa kutoka hospitalini, wagonjwa 73 tu ndio waliokufa kutokana na ugonjwa huo.

Pili, idadi kamili ya kesi zilizothibitishwa nje ya China ni chini ya asilimia moja nchini China, ambayo inaonyesha kuwa juhudi za China katika kuzuia kuenea kwa janga hilo duniani ni nzuri sana.

Tatu, ni juhudi zisizo na mwisho za China, kiwango cha vifo vinavyosababishwa na virusi vipya vya corona nchini China ni karibu asilimia 2.1 chini sana kuliko viwango vya vifo vya homa ya H1N1 ya 2009, Ugonjwa wa Kupumua Mashariki ya Kati (MERS) ya 2012 na ebola, ambazo ni: 17.4%; 34.4 %; na 40.4%. Kuna hofu kadhaa ya kuambukizwa ugonjwa wa virusi vipya vya corona kutoka kwa waathirika wasio na dalili. Kwa kweli, kesi kama hizo ni nadra sana kwa sababu watu walioambukizwa na wasio na dalili huwa ni asilimia ndogo tu ya wagonjwa, wote walioambukizwa na idadi ya virusi katika watu kama huwa ni wachache sana.Kwa ujumla, nadhani hakuna haja ya kuogopa juu ya mlipuko wa virusi vipya vya corona na tuna imani kamili na uwezo wa kudhibiti mlipuko huo.



Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke. **NA MPIGAPICHA WETU.**

**Swali: Katika kukabiliwa na kuenea kasi ya virusi vinavyoua, nadhani mshikamano wa kimataifa na msaada ni muhimu sana kwa China kushinda vita dhidi ya janga hili. Hadi sasa, China imepokea msaada gani kutoka Tanzania?Jibu:** Hakika, China ikifanya juhudi zote za kupambana na janga hili, nchi nyingi zimetoa pole na msaada wao kwa China, pamoja na Tanzania.Rais John Pombe Magufuli hivi karibuni alinipa barua kwa Rais Xi Jinping, ambayo alionyesha nia ya Tanzania kusimama kidete na China kwa wakati huu mgumu.

Prof. Palamagamba Kabudi ni Waziri wa kwanza wa Mambo ya Nje wa Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, aliyepiga simu kwa Diwani wa Jimbo la China na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi, kueleza kutambua juhudi za China baada ya kuzuka kwa janga hilo.

Wakati wa kikao cha 146 cha mkutano wa Bodi ya Utendaji ya WHO, mjumbe wa Tanzania kwa niaba ya nchi za Afrika, alisisitiza kwamba kutokana na juhudi kubwa na kujitolea kwa China, Afrika hadi sasa hakuna kesi yoyote iliyothibitishwa.

China inathamini msaada unaotolewa na marafiki Watanzania ambao unatia alama ya uhusiano wetu uliokita mizizi.Swali: Shirika la Afya Duniani (WHO), limetangaza mlipuko mpya wa virusi vya corona, kama janga la afya la dharura kimataifa, lakini ilizuia kupitishwa kwa vikwazo vya kusafiri na biashara. Maoni yako ni nini katika hilo?Jibu: Kwa uwazi na haraka kabisa, serikali ya China inafanya kazi kwa karibu na WHO kwa kila hatua ya janga hili. Mnamo tarehe 30 Januari, WHO ilitangaza kuzuka kwa virusi vipya vya corona duniani kama janga la afya ya dharura kimataifa.Kama Mkurugenzi Mkuu, Tedros (Ghebreyesus) alivyosema, sababu kuu ya tamko hilo sio kile kinachotokea nchini China, lakini ni kwa sababu ya kile kinachotokea katika nchi zingine na hofu kubwa ya WHO, ni uwezekano wa virusi kuenea katika nchi zilizo na mifumo dhaifu ya kiafya na ambayo haijajitayarisha vizuri kukabiliana nayo.

Kweli, kwa njia nyingi, China inaweka kiwango kipya cha majibu ya mlipuko huo, ambayo yamekubaliwa na WHO. Ni kweli kwamba, WHO haipendekezi vikwazo vyovyote vya kusafiri au biashara, kulingana na habari iliyopo sasa.

> **Kweli, kwa njia nyingi, China inaweka kiwango kipya cha majibu ya mlipuko huo, ambayo yamekubaliwa na WHO.**

Kamati ya Dharura ya WHO, iligundua zaidi kwamba ushahidi umeonyesha kuzuia harakati za watu na bidhaa wakati wa dharura za afya ya umma, kunaweza kuwa si sawa, kukatiza misaada inayohitajika na msaada wa kiufundi, kuvuruga biashara na kuwa na athari mbaya kwa uchumi wa nchi zilizoathirika.

Katika kikao cha 146 cha Bodi ya Utendaji, WHO kwa mara nyingine ilitoa wito kwa nchi zote ulimwenguni kutekeleza maamuzi yenye

**INAENDELEA UK.18**

# Mtafiti Dk. Mihayo: Minyoo tumbo inavyokuingia...balaa!



Ndivyo walivyo minyoo na athari zao. **PICHA: MTANDAO**

**Na Beatrice Philemon**

**Swali: Unapozungumzia ugonjwa wa Minyoo ya Tumbo, kwa lugha ya kawaida kabisa, maana yake ni nini?**

**Jibu:** Ni hali ambayo vimelea vya minyoo huambukiza njia ya utumbo wa binadamu na wanyama wengine.Vimelea vya minyoo, vinaweza kuishi mahali popote kwenye mwili, lakini wengi wanapendelea ukuta wa utumbo.

**Swali: Kuna aina ngapi za minyoo na inasababishwa na nini kimaumbile au kimatendo?**

**Jibu:** Kuna ya aina tatu za minyoo ya tumbo: Minyoo Mviringo (rond worms), Minyoo Mjeledina na Safura

**Swali: Mtu anajitambuaje kama ana minyoo ya tumbo?**

**Jibu:** Mtu mwenye maambukizi ya minyoo anakuwa na dalili kama kuvimba tumbo, kuharisha, kuharisha damu, maumivu ya tumbo, kuwa na kichefuchefu, kutapika, kupoteza hamu ya kula, kupungua uzito, upungufu wa damu, ukuaji watoto ni hafifu na kuwashwa ngozi.

**Swali: Waathirika zaidi wa minyoo ya tumbo ni kundi gani la watu, mfano jinsia, umri na wakazi wa eneo gani zaidi wanaopata ugonjwa huu?**

**Jibu:** Waathirika zaidi wa ungonjwa wa minyoo, ni watoto wa jinsia zote kuanzia miaka mitatu hadi 17.

**Swali: Minyoo ya tumbo inaleta madhara gani katika jamii?**

**Jibu:** Inadhoofisha ukuaji maendeleo ya mtoto kimwili na kiakili, inachangia umasikini na huduma za uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla

Minyoo ya tumbo isipotibiwa mapema, inaongeza maambukizi na hata kifo

**Swali: Mtu akikaa na minyoo tumboni kwa muda mrefu bila ya kumeza dawa, anapata ugonjwa gani?**

**Jibu:** Mtu akikaa na minyoo ya tumbo kwa muda mrefu bila ya kumeza dawa anaweza kufariki

**Swali: Mtu akipata ugonjwa wa minyoo, anatakiwa kufanya nini?**

**Jibu:** Mtu akigundua kuwa na ugonjwa wa minyoo ya tumbo, anatakiwa kwenda katika vituo vya tiba kwa ajili ya kuchunguzwa na kupatiwa matibabu

**Swali: Mara nyingi inapatikanaje na maeneo gani?**

**Jibu:** Minyoo ta tumbo hupatikana katika maeneo ambayo binadamu anajisaidia hovyo, bila ya kutumia choo. Binadamu huvipata vimelea vya minyoo, kwa kula vyakula ambavyo havijaoshwa au kupikwa vizuri, kula vyakula bila ya kunawa mikono, kunywa maji yenye vimelea vya minyoo, kuweka mikono michafu kinywani na kutovaa viatu.

**Swali: Kitaifa, maeneo gani wanaathirika na ugonjwa huo na nini chanzo chake?**

**Jibu:** Maeneo yote ya mijini na vijijini ndio waathirika wa ungonjwa wa minyoo, ambayo usafi wa mazingira ni duni.

Swali: Naomba darasa la tiba yake na kama kuna vigezo vya kijinsia, umri na kadhalika?

Mgonjwa anatakiwa kufika vituo vya tiba kwa ajili kuchunguzwa, kujua aina ya minyoo, ili aweze kupewa ya matibabu sahihi.

**Swali: Hali ikoje katika athari za minyoo ya tumbo kitaifa?**

**Jibu:** Kiwango cha ungonjwa wa minyoo bado ni kikubwa nchini

**Swali: Minyoo inatibiwa katika ngazi zipi za tiba, kama vile zahanati, kituo cha afya au hospitali?**

**Jibu:** Inatibiwa katika ngazi zote za tiba, kuanzia zahanati, kituo cha afya hadi hospitali

**Swali: Nini changamoto mnayokabiliana nayo na namna mnavyofanikisha kuukabili mtihani huo?**

**Jibu:** Bado (jamii) ina uelewa mdogo juu ya maambukizi ya ugonjwa wa minyoo, hasa inapokuza suala la kutekeleza kampeni ya Tiba Kinga. Juhudi bado zinaendelea kuelimisha jamii juu ya ugonjwa wa minyoo.

Swali: Dawa zinazotakiwa kutumia kutibu minyoo ya tumboni aina zipi?

Jibu: Dawa za Mabendazole au Albendazole hutumika kutibu ungonjwa wa Minyoo,

**Swali: Mpaka sasa hali ya minyoo ya tumbo nchini ipoje, na katika wilaya ya Bagamoyo ikoje?**

**Jibu:** Katika wilaya ya Bagamoyo; matokeo ya utafiti wa mwaka 2015 kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa minyooni asilimia 28 (ya wakazi).

**Swali: Wananchi wanatakiwa kufanya nini, wasipate minyoo ya tumbo?**

**Jibu:** Wanatakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya choo na usafi wa mazingira kwa ujumla. Pia inatakiwa itolewe elimu ya afya kwa jamii jinsi ya kujikinga na magonjwa haya.

AFYA

# Balozi China: Uamuzi wa busara wanafunzi Watanzania kubaki



Ndio hali halisi ya mapya ya kila siku, jijini Wuhan. **PICHA ZOTE: MITANDAO.**

**INATOKA UK.17**



ushahidi na yasiobadilika.

**Swali: Je, serikali ya China inafanya nini kuhakikisha usalama wa wanafunzi wa Kitanzania ambao wamekwama huko Wuhan na hali yao ikoje? Je, inahitajika Tanzania kuwanusuru raia wake kutoka Wuhan na maeneo mengine yaliyoathiriwa zaidi, hivi saa nchini China?Jibu:** Kama mama, ninaelewa kikamilifu hisia na wasiwasi wa wazazi wa Kitanzania ambao watoto wao wanasoma huko Wuhan, kitovu cha mlipuko mpya wa virusi vya corona. Napenda kuchukua fursa hii kuwaambia Watanzania, hali halisi iliyoko huko Wuhan.

Kwanza, kwa jinsi ninavyojua, hakuna kesi ya virusi vipya vya corona au kesi inayoshukiwa miongoni mwa wanafunzi wa Kitanzania, ambao kwa sasa wanasoma Wuhan.Pili, wanafunzi wa Kitanzania Wuhan wako salama katika vyuo vikuu vyao. Wanatunzwa vizuri na viongozi wa eneo hilo. Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Wuhan, wanafunzi wa kigeni hupewa milo ya bure, barakoa (masks), ushauri wa kuua viini vya maradhi na wa kisaikolojia.

Wafanyakazi wa chuo kikuu wanaua viini vya maradhi maeneo ya karibu ya mabweni ya wanafunzi kila siku. Ofisi za Mambo ya Nje katika ngazi zote katika Jimbo la Hubei, zimefungua simu za moja kwa moja za saa 24 kwa wahamiaji, na kutoa habari kwa wakati na msaada unapohitajika.

Kwa kuongezea, kila chuo kikuu huko Wuhan kimechagua mtu wa mawasiliano kwa wanafunzi wa kigeni na kutangaza jina la mtu huyo na nambari ya simu mtandaoni. Tatu, kupunguza mawasiliano ya watu kwa watu, vyuo vikuu vyote huko Wuhan, vimeahirisha kuanza kwa muhula ujao. Tarehe maalum ya kuanza muhula mpya itatangazwa baadaye kulingana na hali ya janga.Pia, utoaji mahitaji Wuhan na miji mingine nchini China unajitosheleza. Serikali ya China imeahidi juhudi za kuendeleza usambazaji wa mahitaji muhimu katika maeneo yaliyoathiriwa na virusi vya corona, kupanga usafirishaji wa kila siku wa mboga mboga, mafuta ya kupikia, mchele na unga kwenda Wuhan.

> **Natumai pia, Watanzania watafuata maagizo na miongozo iliyowekwa na mamlaka husika, kitaifa na kimataifa.**

Tafadhali muamini kuwa wanafunzi wa Kitanzania huko Wuhan na miji mingine nchini China watapata chakula cha kutosha na msaada mwingine wa vifaa.Wakati wa kukutana kwa Mshauri wa Nchi ya China na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi huko, Beijing, Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus, anasema WHO haipendekezi uhamishaji raia na alitaka jamii ya kimataifa kuwa na utulivu na isiwe na jazba.

Kwa mujibu wa ushauri wa kitaalamu kutoka WHO na kuzingatia hali iliyopo Wuhan, ikiwamo juhudi za China inavyoyounganisha rasilimali zake katika mji huo kupambana na janga hilo, ni chaguo la busara na salama kwa wanafunzi wa Kitanzania kubaki Wuhan, kwani ni vizuri kwao, familia zao na nchi zao.

**Swali: Je, una ushauri gani kwa Watanzania na mamlaka za hapa?Jibu:** Serikali ya Tanzania imechukua hatua za haraka na za uwajibikaji kuzuia uingizwaji virusi vipya vya corona kutoka nchi za nje na kujiandaa kwa uwezekano huo.

Hatua kubwa zilizochukuliwa na mamlaka ya Tanzania, ni pamoja na uchunguzi wa abiria wote wanaoingia katika vituo vyote vya kuingia, kuweka vituo vya magonjwa ya kuambukiza; Kilimanjaro, Mwanza na Dar es Salaam, kutoa mafunzo kwa watendaji wa afya juu ya jinsi ya kushughulikia magonjwa ya kuambukiza na usimamizi wa janga.

Imefungua simu za bure za saa 24 kwa umma, kwa ujumla kuripoti kesi zinazoshukiwa. Tunaamini kuwa, serikali ya Tanzania itaongeza juhudi zake kuzuia kuenea kwa virusi vipya vya corona na China itasimama kidete na Tanzania katika suala hili.

Natumai pia, Watanzania watafuata maagizo na miongozo iliyowekwa na mamlaka husika, kitaifa na kimataifa, ili kujua ugonjwa na kujilinda kwa njia nzuri na ya kisayansi.

Kwa upande mwingine, watu wanapaswa kuwa waangalifu na makini zaidi na usafi na matengenezo ya maisha mazuri. Kwa mfano, osha mikono yako na sabuni mara nyingi zaidi; epuka kuwasiliana karibu na mtu yeyote mwenye homa na kikohozi, kula chakula cha virutubishi na fanya mazoezi mara kwa mara.

Kwa upande mwingine, unapaswa kujifunza maarifa kadhaa juu ya virusi vipya vya corona, ili

AFYA

LINI CORONA ITAKOMA?

# Rais Trump, wataalamu dunia kila mmoja anabashiri lake



Harakati za kujihami na maradhi ya corona, katika uwanja wa ndege. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

UTAALAMU wa hisabati ya magonjwa ya mlipuko (epidemiology) uko katika mtihani mgumu kwa kutanzua kitendawili cha mwenendo wa ugonjwa wa corona, linaoendelea kuitesa dunia, huku China ikiwa mwathirika mkuu.

Suala hilo liko katika midomo na hisia za wataalamu kwani kupanga mahitaji ya raslimali na miundombinu ya kupambana na gonjwa hilo, na mahitaji ya ziada katika jamii, taasisi za nchi na hata bajeti inategemea ugonjwa huo unavyoendelea.

Likifikia kilele chake, maana yake ni kwamba wanaoambukizwa wanapungua kwa kasi na ugonjwa unaanza kupoteza makali yake ya awali, inakuwa kuwaangalia wagonjwa zaidi.

Mamlaka muhimu zaidi kuiongoza dunia katika suala hilo, ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya (WHO), ambalo limekuwa likiulizwa swali ni baada ya takriban wiki mbili za kuenea kwake.

Ndani ya kilichoonekana katika kipindi cha wiki mbili ni kuwa kasi yake hasa ilikuwa China na zaidi katika jiji la Wuhan ndani kabisa ya nchi hiyo, kitovu cha mitandao ya kibiashara ya aina tofauti kwa majimbo yaliyo mbali na ukanda wa bahari.

Kwingineko, athari zilikuwa haba, waathirika wachache kwa baadhi ya washirika wa karibu wa China, kwa mfano Marekani, iligundua watu wanne wenye virusi vya corona wakatibiwa na waliruhusiwa kutoka hospitali.

Kuelekea mwisho wa wiki ya kwanza ya mwezi Februari, maofisa wa ngazi za juu wa WHO wanaokutana kila wakati kutoa vielelezo vya wakati uliopo kuhusu kuenea na juhudi za kupambana na ugonjwa huo, bado hawakuwa na majibu.

Walisema tu kuwa 'ugonjwa huo bado haujafikia kilele chake' kwa maana kuwa kasi ya kuambukiza bado ndiyo kubwa, licha ya kuwa wanaopona na kutolewa hospitalini nao walikuwa wengi.

Wataalamu walianza kupata picha ya jinsi ugonjwa huo unavyoenea, wakilinganisha na mafua ya ndege (Sars) na ebola kwa upande wa Afrika, magonjwa ya mlipuko yanayoenezwa pia kwa kupumua.

WHO inasema bado mapema kusema ni wakati gani corona itafikia au itakuwa imefikia kilele chake, lakini baadhii walisema jijini Hong Kong kuwa inaelekea itakuwa mwezi wa Machi.

Hata hivyo, kuna taarifa zilizosikika katika televisheni, zikimnukuu mtaalamu kutoka Hong Kong, anayesema kilele cha corona huenda kisifikiwe kabla ya mwezi Mei.

Ni ubishi unaotokana na harakati za uchomozaji takwimu za awali, mifumo ya uambukizaji, uzuiaji na kupata jibu sahihi.

Rais Donald Trump wa Marekani, aliona aingie katika mkondo huo wa kubuni ni wakati gani corona inaweza kuanza kupungua nguvu, akasema katika ukurasa wake wa mtandao wa 'twitter kuwa wakati kipupwe kikipungua na kiangazi chepesi kuanza virusi hivyo vitapungua nguvu.

Ilikuwa ni baada ya kufanya mazungumzo ya simu na Rais Xi Jinping wa China, lakini haikuwa wazi kama hisia hiyo ilitokana na waliyojadiliana, ambako alitumia nafasi ya mtandao wa twitter kutoa pongezi kwa Rais Xi na jitihada na udhati wa kusukuma suala hilo anazoonyesha.

Amemwambia Rais Xi Jinping, kwamba anahisi China inafanya vizuri katika juhudi hizo, na ana mtazamo wa jinsi virusi hivyo vinavyoweza kupungua nguvu za joto, halafu huenda vitapotea kabisa.

Baada ya Rais Trump, kutoa hisia hizo wataalamu walirudia msimamo wa WHO kuwa bado ni mapema kujua kilele cha corona kitafikiwa wakati gani, licha ya kwamba muda huo wa Machi ni kuanza kupungua baridi kwa upande wa Kaskazini mwa Dunia.

Hapo ikawa vigumu kwa wachambuzi wa habari kueleza ni wapi ambako Rais Donald Trump, alipata picha hiyo, katika mpangilio wa kitaaluma uliofanya uhakiki wa kitakwimu wa mlipuko huo na hata kufikia tamati.

Ilikuwa vigumu kujua kama Rais Trump alilenga hisia halisi ya kitaaluma au alibuni fikra hiyo kiitikadi, ikizingatiwa ni mtaalamu na mahiri wa propaganda na ujanja wa kiitikadi anayejulikana sasa kimataifa, kuna uwezekano alibuni huo mwenendo tarajiwa.

Kwa kuambatanisha hali ya hewa na ugonjwa wa corona iliyoibuka katika kipindi cha baridi, kuna hisia virusi hivyo vinastawi katika baridi na joto likiingia, huenda litaipunguza nguvu, kwani siyo mazingira yake muafaka.

> Ni ubishi unaotokana na harakati za uchomozaji takwimu za awali, mifumo ya uambukizaji, uzuiaji na kupata jibu sahihi.

Wenye uzoefu na vimelea (bakteria) hivyo, wana mtazamo kwamba kuna walakini katika hisia hizo, kwani siku zote joto ni mazingira muafaka kumea na kuenea kila aina ya vimelea, hata vinavyokuwa mwilini.

Yako mazingira kimataifa pamoja na ubishi wa kiitikadi, kuhusiana na wakati wa kujiandaa kwa kampeni za uchaguzi mkuu Marekani mwaka huu, Rais Trump akiwania nafasi yake kwa muhula wa pili.

Mazingira hayo yanahusu mijadala ya janga la mabadiliko ya tabianchi, kutoka mtazamo wa kuongezeka joto kunaleta hali mbaya ya kuyeyuka barafu, kuongezeka maji baharini na kusababisha mvua kubwa, vimbunga na mafuriko katika maeneo mengi.

Rais Trump, ni mmojawapo ambao kwa takriban miaka 20 wamekuwa wakikataa ukweli huo na kuzuka ugonjwa huo, ambao haijaeleweka ilivyofumuka, kunatoa mwanya wa kufanya kejeli.

Wakati mazingira ya joto yanaongeza hatari ya vimelea kuwa na nguvu zaidi, binafsi kiongozi huyo anatoa rai kuwa huenda ndiyo vikakosa nguvu na kujifia, akiwa na maana jamii ianze kuona ongezeko la joto duniani kuna faida zake, na jamii isijisumbue kutatua.

Hata zaidi ya hapo, ni kuzuia wataalamu wasielekeze mawazo yao katika hali hii ya joto kuongezeka na vimelea vya wanyamapori wanaoliwa kuongezeka nguvu na kuzusha janga la kuambukizana na uwezekano wa milipuko baadaye.

AFYA

SIKU YA UKEKETAJI

# Yanayojificha yaibuliwa upya hadharani mchana

• Watoto waanika wanachofanyiwa • Wanaharakati wasimulia mapya



Baadhi ya wanafunzi wakiimba nyimbo zao za kupinga ukeketaji, katika maadhimisho yaliyoandaliwa na TGNP Mtandao katika viwanja vya Shule ya Sekondari Kitunda, Jijini Dar es Salaam.

**Na Yasmine Protace**

UKEKETAJI una madhara na hilo halina ubishi. Unamwathiri kisaikolojia na kama ni mwanafunzi, anaweza kukatiza masomo na kushindwa kufikia ndoto yake.

Kuna vijana wengi walioko masomoni hivi sasa, wanatarajia baada ya hapo kuna hatua zaidi ya ama shule au vyuo na wafikie kuwa watu wa aina fulani, katika kuchangia maendeleo ya taifa.

Ukeketaji kwa kiasi kikubwa umechangia matatizo makubwa ya kiafya, hasa kupitia upotezaji damu nyingi kwa tendo hilo. Inaelezwa, licha ya madhara hayo, bado kwa kiasi kikubwa jamii haijapata elimu sahihi ya athari hizo ambazo zimetajwa chache, kati ya nyingi zilizopo.

**MAADHIMISHO KITUNDA**

Hivi karibuni Februari 6 katika maadhimisho ya ukeketaji yaliyofanyika Kitunda jijini Dar es Salaam, kuna mengi yalizungumzwa kutokana na matukio hayo ya ukeketaji, kwenye eneo hilo ambako kunadaiwa kuna nyendo hizo.

Ni maadhimisho yanayofanyika kila siku hiyo duniani kote na kunapatiwa kaulimbiu yake kila mwaka.

Safari hii mwandaaji akiwa mwanaharakati wa kijinsia, TGNP Mtandao katika Shule ya Sekondari Kitunda, wananchi wa maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam, walishiriki, wakiwamo wanafunzi kutoka shule mbalimbali, ambao walikuwa walengwa wakuu.

**OFISA USTAWI**

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Kitunda, Anatolia Wabuke, anasema kuwa baadhi ya vijana wamejikuta wakitengwa na wazazi wao, kutokana na kuoa wanawake ambao hawajakeketwa.

"Ofisi yangu,imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa vijana na ambao wameoa wasichana ambao hawajakeketwa, hivyo familia zimekuwa zikiwatenga kutokana na kuoa wasishana ambao hawajakeketwa," anasema.

> **Malalamiko tunayapata ndoa zinavunjika, kutokana na baadhi ya wazazi kuwatenga watoto wao wa kiume, ambao wameoa wanawake hawajakeketwa, hivyo ili mwanaume asitengwe na familia yake inabidi avunje ndoa yake.**



Ofisa Programu wa TGNP Mtandao, Anna Sangai. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

Anaongeza kuwa, vijana wamekuwa wakitengwa na familia zao baada ya kubainika wameoa wasiokeketwa na ofisi yake imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wanawake, wanaoidai kuachwa na waume zao, kutokana na wazazi wa wanaume kuwakata watoto wao wa kiume, kutoendelea kuishi na wanawake ambao hawajakeketwa.

"Malalamiko tunayapata ndoa zinavunjika, kutokana na baadhi ya wazazi kuwatenga watoto wao wa kiume, ambao wameoa wanawake hawajakeketwa, hivyo ili mwanaume asitengwe na familia yake inabidi avunje ndoa yake," anasema.

Anafafanua kwamba elimu wameishatoa kwa mangariba, wanaodai kwa sasa wanatumia nyembe moja kukeketa watoto, lakini miaka ya nyuma walitumia moja kukeketa watoto wengi.

Wabuke anasema, ngariba pamoja na kudai wanatumia nyembe moja ili maambukizi yasitokee kutokana na kutumia nyembe moja kwa watoto wengi, tayari wameishawapatia elimu inazungumzia athari zitokanazo na ukeketaji.

Ofisa Ustawi Jamii huyo, anasema pamoja na kutoa elimu, lakini baadhi ya wazazi sio waaminifu, kwani wamekuwa wakitumia likizo za shule kwa watoto kwa kuwatoa mkoa mmoja na kuwapeleka mwingine na kuwafanyia ukeketaji.

Anasema, taarifa hizo zinatolewa na watoto, baada ya kurudi likizo na anaitaka jamii kutoa taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya ukeketaji, ili wahusika wachukuliwe hatua stahiki na wanaokeketwa, watoe taarifa ili wahusika wachukuliwe hatua haraka.

Wabuke anasema, wakeketaji wana mbinu nyingi katika kutekeleza azma zao, ikiwamo watoto wamekuwa wakitumia likizo kwa kuwasafirisha wanafunzi na kuwakeketa.

Anasema, amekuwa akipata malalamiko hayo kutoka kwa wanafunzi wanaorudi kutoka likizo, wanaotoa taarifa kwamba wamekeketwa.

**OFISA TGNP**

Anna Sangai, ni Ofisa wa TGNP Mtandao, anayesema kuwa ofisi yake imeamua kuzungumza na vijana, jinsi ya kujikinga na ukatili wa kingono.

Anasema katika kuadhimisha Siku ya Kupinga Ukeketaji Duniani, kila mwaka wana kaulimbiu ya mwaka huu ni 'nguvu ya vijana kupinga ukeketaji'.

Ofisa huyo anaonyesha takwimu zinaonyesha watu zaidi ya milioni nne duniani walishafanyiwa ukeketaji na anaongeza: "Tanzania mkoa wa Manyara unaongoza kwa matukio hayo, ukifuatiwa na Dodoma."

Anna anasema wanaofanya matukio hayo wamekuwa wakibadilisha mbinu na kwa sasa hata watoto wadogo zaidi wamekuwa wakifanyiwa ukeketaji.

"Wanaotenda ukatili huo wamekuwa wakibadili mbinu ambapo, kwa sasa asilimia 30 ya watoto wadogo wamekuwa wakifanyiwa ukeketaji," anasema.

Ofisa huyo wa TGNP Mtandao, anasema wajawazito na kinamama wanaotarajia kujifungua, wamekuwa wakifanyiwa ukeketaji na matendo hayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya familia.

Anasema, katika kupambana na matukio hayo, TGNP Mtandao imekuwa ikizungumza na vijana jinsi ya kujilinda na ukatili wa kingono na ikazindua kampeni ya ukeketaji, yamesababisha baadhi ya watoto ndoto zao kupotea kutokana na kufanyiwa ukatili.

Pia anafafanua ni wakati wa kila mmoja kutumia nafasi aliyo nayo, ili kutokomeza ukeketaji. Anasema: "Tanzania imejipanga ifikapo 2030 na masuala ya ukatili wa aina zote uwe umetokomezwa."

Anakiri vitendo vya ukatili ni vingi sana na vinafanywa na jamii yenyewe na anasema watoto wasiposimamiwa vizuri wakaendelea kufanyiwa ukatili ndoto za watoto hazitazaa matunda.

**MABINTI WANENA**

Hamidi Juma, ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Misitu, anaomba sheria iwabane mangariba, ambao wanaharibu ndoto za vijana kutokana na kuwakeketa.

Mwanafuzi huyo anashauri wazazi wanaoendekeza matukio ya ukeketaji,o wachukuliwe hatua kali, kwaniwatoto wengi wana matarajio akimaliza shule wawe sehemu fulani ya jamii, lakini kutokana na kufanyiwa ukeketaji, malengo yao yanawapotoka.

"Hapa kila mtoto anandoto zake, akimaliza shule, anataka kuwa nani, lakini ndoto zinapotea kutokana na kukatizwa na wakeketaji," anaeleza Ema.

Anasema, watoto wanapofanyiwa ukeketaji mara nyingi wanaathirika kisaikolojia na hapo ndipo unapokuta anashindwa kuendelea na masomo.

Ashura Jumanne, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kitunda, Dar es Salaam, anasema wazazi wanaotoa baraka ili watoto wakeketwe, sheria zinatakiwa zichukuliwe dhidi yao.

Anasema, hata vijana hawapaswi kukaa kimya na wanatakiwa kutoa taarifa, pale wanapoona kuna viashiria vya ukeketaji.



# Wafugaji kuishtaki halmashauri kwa Mpina

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAFUGAJI wilayani Chunya, mkoani Mbeya, wameunda kamati ya watu watano kwenda kuishtaki halmashauri ya wilaya hiyo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, wakidai kukwepa kuwalipa fedha zao zaidi ya Sh. milioni 94.

Fedha hizo ni ambazo halmashauri hiyo iliwatoza zaidi ya kiwango kilichokuwa kimeelekezwa na serikali wakati wa kupiga chapa mifugo mwaka 2017, badala ya kutozwa Sh. 500 kwa mfugo mmoja walikuwa wanatozwa Sh. 1000. Mwenyekiti wa chama cha wafugaji wa wilaya hiyo, Shang'ai Laboi, alisema halmashauri hiyo iliagizwa na Waziri Mpina kuwarejeshea fedha zao, lakini mpaka sasa hawajalipwa.

Alisema agizo hilo la waziri bado halijatekelezwa na halmashauri hiyo kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wake, imeweka masharti magumu kwa ajili ya kuwalipa fedha hizo hali ambayo wanahisi ni mbinu za kutaka kuwadhulumu. Alisema wameelezwa na Mkurugenzi kuwa watanatakiwa kulipwa kwa awamu tofauti na kwa kuwalipa mfugaji mmoja mmoja kwenye kila kijiji na watalipwa wale wenye risiti za malipo hayo.

"Sisi tuna chama chetu cha wafugaji na tuna akaunti benki, tunachotaka fedha zetu zitumwe kwenye akaunti yetu na ndicho wafugaji wote wanataka, huko ndio tuna uhakika wa fedha hizo kumfikia kila mfugaji, lakini timu tuliyoichagua ni kwa ajili ya kumwambia waziri kuwa agizo lake halijatekelezwa," alisema Laboi.

Alisema hawako tayari kulipwa fedha hizo kidogo kidogo kwa sababu wao walilipa zote kwa wakati mmoja.

Mmoja wa wafugaji hao, Juma Mihayo, alisema awali wakati wanaanza kutekeleza kupiga mifugo chapa, walitumia chama cha wafugaji kuwahamasisha, hivyo wanataka malipo yao yarejeshwe kupitia akaunti ya chama.

Mihayo alisema halmashauri hiyo haiwafahamu wafugaji na baadhi yao walishahama na wengine wamepoteza risiti hivyo itakuwa vigumu kupata haki zao.

"Sisi wafugaji hatuhitaji kulipwa mmoja mmoja, tunataka fedha zetu ziingie kupitia kwenye chama chetu cha wafugaji, zile ni fedha zetu na hatuhitaji kumpigia mtu magoti ili tulipwe," alisema Mihayo. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Sophia Kumbuli, alisema haiwezekani halmashauri hiyo ikalipa fedha hizo kupitia kwenye chama kwa madai kuwa sio makubaliano ya wafugaji wote.

Hata hivyo alisema ana mpango wa kukutana na kufanya mazungumzo na wafugaji hao ili kufikia mwafaka na kuwaelimisha kuhusu namna ya kulipana fedha hizo.



Maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) Taifa, pamoja na wananchi wa Kijiji cha Igoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiwa wameunganisha mikono kijijini hapo, juzi, kuashiria maridhiano ya kubadilishana mashamba kwa ajili ya shughuli mbalimbali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ataka wana-CCM kujitathmini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Dk. Stephen Mwakajumilo, amewataka viongozi wa CCM na serikali kujenga utamaduni wa kujitathmini katika utendaji wao kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ujenzi wa maendeleo ya taifa.

Alitoa wito huo, juzi wakati akizungumza na wanachama wa CCM katika Kata ya Ruiwa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya na kubainisha kuwa amekuwa akisikitishwa na tabia ya baadhi ya viongozi wa ndani ya CCM na serikali ambao wanasuasua kuharakisha maendeleo ya nchi.

Alisema kwa bahati mbaya kuna viongozi ambao hawajengi utamaduni wa kujipima na kujitathmini katika utendaji wao wa kila siku, hali ambayo inasababisha kuchelewesha jitihada za Rais kuharakisha maendeleo ya wananchi aliyoyakusudia kutekeleza kwa muda wa uongozi wake.

Akionyesha kukerwa, Dk. Mwakajumilo alitoa mfano agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu vijiji 366 vilivyokuwa karibu na hifadhi za taifa kutoondolewa na kusema kuwa mpaka sasa kumekuwa na ukakasi wa agizo hilo katika maeneo aliyoelekeza na kuweka wazi kuwa Wilaya ya Mbarali kuna vijiji 29 kati ya 33 ambavyo havipaswi kuondolewa.

"Tangu Rais Magufuli atoe agizo la vijiji 29 vilivyokuwa karibu na Hifadhi ya Ruaha katika Wilaya ya Mbarali kutoondolewa na badala yake vifanyiwe mchakato wa kuvirasimisha, lakini jambo la ajabu hakuna kiongozi yeyote ndani ya chama na serikali aliyefika katika vijiji hivyo kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa kina na kuainisha mpaka wao kati ya vijiji na hifadhi ili kuepusha sintofahamu," alisema Dk. Mwakajumilo.

Alisema kuna mpaka ambao awali uliwekwa na watendaji wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) katika Wilaya ya Mbarali na ambao unaofahamika kama GN 28, ni kero kubwa ndani ya CCM kutokana na wananchi kutokubaliana na mpaka huo baada ya kumega eneo kubwa la wilaya hiyo na hivyo kuathiri shughuli za ujenzi wa makazi na shughuli za kilimo.

Alisema viongozi wana wajibu wa kujenga utamaduni wa kutambua mahitaji ya wananchi wanaowaongoza na kuiga mienendo ya Rais Magufuli ya kuwa muwazi katika mambo mbalimbali.

Dk. Mwakajumilo aliwasihi wanachama wa CCM kuacha kubweteka na ushindi walioupata katika uchaguzi wa serikali za mitaa na kuwa wanajukumu kubwa katika uchaguzi ujao wa madiwani na wabunge kukiletea ushindi chama hicho.

Alisema umoja na upendo miongoni mwa wanachama wa CCM ndiyo msingi mkubwa wa mafanikio katika chaguzi mbalimbali na kuwa mwanachama yeyote hana budi kuhakikisha anaimarisha misingi hiyo kwa ajili ya maendeleo ya chama na serikali kwa ujumla.

Pia Mwakajumilo aliwatahadharisha wanachama wa CCM kuwa makini na wanaotaka kupata madaraka kwa kuwa hawatakuwa na nafasi katika uchaguzi ujao wa madiwani na wabunge na kuwa lengo kuu la CCM ni kuwapata viongozi wenye nia ya kweli katika kuwaongoza wananchi bila ya kuangalia uwezo wao wa kifedha.

Alisema kama kiongozi wa CCM taifa atahakikisha anafanya mikutano na wanachama maeneo ya vijijini kusaidia kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wanachama na viongozi wanaowaongoza.

## Madereva magari ya mizigo wakwama

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MADEREVA zaidi ya 30 wa magari ya mizigo wamekwama kuendelea na safari kwa muda wa siku sita, kufuatia kipande cha barabara ya Chang'ombe kwenda Mkwajuni wilayani Songwe yenye urefu wa kilometa 2.3, kusombwa na mafuriko. Wakizungumza na Nipashe jana madereva hao walisema mvua kubwa iliyonyesha hivi karibuni ilisababisha Mto Lupa kujaa maji na kuvunja kingo zake hali iliyosababisha maji kukosa mwelekeo na kusomba barabara.

"Ni siku ya sita sasa tuko hapa Mkwajuni barabara ya Chang'ombe kuelekea Mkwajuni imekatika mawasiliano baada ya kusombwa na maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, hatujui ni lini maji yatapungua ili tuanze safari maana magari yetu yamepakia mizigo," alisema mmoja wa madereva hao, Rafael Mwambaje.

Mwambaje alisema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo kampuni ya madini ya Shanta imepeleka vifaa na kuanza kumwaga vifusi vya mawe kuziba maeneo yaliyosombwa na maji. Aliiomba serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroad), Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) kusaidia kutengeneza kipande hicho cha barabara ili kurejesha mawasiliano na wananchi waendelee na shughuli zao.

Miongoni mwa wafanyabiashara Getrude Mwakyoma, alisema hadi sasa wanashindwa kufuata bidhaa mkoani Mbeya kwa sababu ya barabara hiyo kukatika. Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, Samwel Jeremiah, alisema barabara hiyo itafungwa kwa siku mbili ili kupisha matengenezo yanayofanywa na kampuni ya uchimbaji madini ya Shanta kwa kushirikiana na Tanroad, Mkoa wa Songwe.

Ameagiza Tanroad kuweka kambi katika barabara hiyo badala ya kuwaachia wadau ambao wamejitoa kuisaidia serikali. Hata hivyo Meneja wa Utawala Kampuni Madini ya Shanta, Saimon Rweyemamu, alisema watahakikisha kazi inakamilika kwa wakati ili wananchi wapate huduma ya usafiri ikiwa ni pamoja na magari ya mizigo zaidi ya 30 yaliyokwama.

Mhandisi wa Tanroad Mkoa wa Songwe, Nyembo Mhaga, alisema wanatafuta suluhu la kudumu kudhibiti mafuriko katika eneo hilo kwa sababu hata mwaka jana yalitokea na walidhibiti, lakini mvua za mwaka huu zimeleta madhara makubwa.





# Matumizi fedha za kigeni uagizaji vyakula yapungua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TIMU ya wachambuzi wa Sera za Kilimo (PAG), imesema kwa kipindi cha miaka mitano kumekuwapo na mafanikio makubwa kwenye uboreshaji wa sera ambayo yamechangia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa vyakula kutoka nje ya nchi.

Matumizi hayo yamepungua kutoka Dola za Marekani 640 hadi 250.

Hayo yalielezwa jana na Mshauri wa Sera za Kilimo na Mratibu wa timu hiyo, David Nyange, alipokuwa akizungumza kuhusu kujenga mazingira wezeshi katika sekta ya kilimo, kwenye kongamano la sita la Sera za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, jijini hapa.

Jukwaa la wadau hao linaundwa na taasisi 15 zinazojihusisha na utafiti na maendeleo ya sekta ya kilimo, zikiwamo ANSAF, ASPIRES, SAGCOT, TPSF, ACT, TAHA, FSDT, AMDT, MAFAP (FAO), ESRF, REPOA, ENGINE na EAGC. Pia, Dalberg, PASS Trust, TAHA na AGRA. Akizungumza katika kongamano hilo, Nyange alisema mafanikio ya maboresho ya sera, sheria, kanuni na taasisi za maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kipindi hicho inaonyesha mafanikio makubwa katika uboreshaji wa sera na maboresho zaidi ya 200 yamefanyika.

"Maboresho hayo yamelenga unafuu wa kodi kwa pembejeo na teknolojia mbalimbali zinazotumika katika uzalishaji wa mazao, mifugo na samaki, pia ongezeko la ushuru ili kulinda wazalishaji wa ndani, kupunguzwa kwa ushuru wa mazao unaotozwa na halmashauri za serikali za mitaa na kuondolewa au kupunguzwa kwa utitiri wa tozo mbalimbali," alisema.

Alieleza kuwa ongezeko la ushuru wa forodha kwenye maziwa, nyama, juisi pamoja na mvinyo katika kulinda viwanda vya ndani umechangia matumizi ya fedha za kigeni katika kuingiza vyakula kutoka nje kupungua kwa kiasi hicho.

"Kutokana na maboresho hayo, utafiti umeshuhudia matokeo ya awali kama vile kupanda chati kwa Tanzania kwa ngazi tatu katika ripoti ya Benki ya Dunia ya Mazingira ya Biashara (2020 Doing Business), kupungua kwa uingizaji bidhaa za vyakula, kuongezeka kwa mapato kwa baadhi ya halmashauri," alisema.

Kadhalika, alisema suala la kodi ya kampuni kwa Tanzania ni asilimia 30 huku Zambia na Msumbiji wakishusha na kuwa asilimia 10, na kushauri serikali kuliangalia suala hilo ili kuongeza ushindani.

Naye Mwenyekiti wa Timu hiyo, Audax Rukonge, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la wadau wa kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF), Audax Rukonge, alisema kiwango cha umaskini kinapungua kwa kasi ndogo na watafiti wanasema kwa kasi hiyo inahitajika miaka 50 kuondokana na umaskini.

"Hii ni kwa sababu sekta zinazojumuisha watu maskini hazijawekewa msukumo ikiwamo uwekezaji na kuwekewa kipaumbele na moja ya sekta hizo ni sekta ya kilimo ambayo inafanyika vijijini, maskini ndio wapo," alisema.

Alitaja sababu nyingine ni uwekezaji wa uchakataji mazao ya kilimo ni mdogo na kwamba kuna haja ya kuweka uwekezaji kwenye eneo hilo.

"Kundi la watafiti ndio maana tumekuja na maudhui ya kuangalia uwekezaji wa sekta binafsi na umma ili kuwapo na tija, tuangalia ukuaji wa sekta ya kilimo ukoje, kulingana na mageuzi yanayofanyika kwa kuwa serikali inabadili sera, tuangalie ukuaji wake unaendana, mazingira ya uwekezaji yakoje," alifafanua.



Waziri wa Mambo ya Ndani, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, George Simbachawene (kulia), akimwonyesha Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabiri Shekimweri (kushoto), athari za mafuriko yaliyokikumba Kituo cha Polisi Chipogoro, jimboni humo, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: WMNN**

# Mahiga awaonya watumishi mahakama

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga amewataka watumishi wa mahakama kuacha ukiukwaji wa maadili ili kulinda heshima ya mhimili huo.

Alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizindua mwongozo wa uendeshaji wa kamati za maadili kwa maofisa wa mahakama ngazi za wilaya na mikoa. Alisema kwa mujibu wa ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mahakama pekee ndiyo chombo chenye jukumu la utoaji haki na kutoa wito kwa watumishi wa mahakama kuendelea kutekeleza vyema jukumu hilo.

"Ninawaasa watumishi wachache ambao bado wanaendelea na vitendo vinavyokiuka maadili ya kazi yao waache ili kulinda heshima ya mhimili wa mahakama na pia usalama wa ajira zao," alisema.

Alibainisha kuwa serikali imeweka kipaumbele kwenye maadili ya utumishi wa umma ili kuongeza imani ya wananchi kwa serikali yao. Alisema jitihada hizo zimezaa matunda makubwa na maadili ya utumishi wa umma yameimarika kwa kiwango kikubwa, wananchi wengi wanaridhishwa na huduma zinazotolewa kwenye taasisi mbalimbali za umma.

"Katika kuhakikisha kuwa mahakama ya Tanzania inatoa huduma bora kwa umma imeamua kuweka kipaumbele katika kudumisha nidhamu na maadili kwa maofisa wa mahakama katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kuimarisha kamati za maadili za maofisa wa mahakama," alisema.

"Kamati hizo zina nafasi kubwa na umuhimu katika kusimamia, kuendeleza na kudumisha maadili ya utumishi wa mahakama ili kuufanya uwe wenye kutukuka, kuheshimika na kuvutia."

Kwa upande wake, Jaji Mkuu wa Tanzania Prof. Ibrahim Juma alisema bila kutoa elimu kwa umma kutasababisha wananchi wengi wenye malalamiko dhidi ya maofisa wa mahakama kuhangaika au kupeleka malalamiko yao kwenye mamlaka zisizo sahihi na hivyo kupoteza muda mwingi kabla ya malalamiko yao kushughulikiwa.

Alisema wenyeviti wa kamati za maadili ni wakuu wa wilaya na mikoa ambao wapo karibu na wananchi hivyo wana imani kuwa kero za wananchi zitawafikia na kuzishughulikia kwa haraka.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema miongozo hiyo iliyozinduliwa itawasaidia kuwapa dira ya kutatua kero na shida za wananchi hasa wanazokutana nazo wanapokwenda mahakamani.

# Serikali yaunda timu kutafiti zao la zabibu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeunda timu ya watu 12, ambayo itafanya utafiti wa zao la zabibu kama linaleta hasara au faida kwa mkulima pamoja na serikali.

Timu hiyo itafanya kazi ndani ya siku 10 pia imeagizwa kujua magonjwa yanayoathiri zao.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alipokuwa akizungumza na wadau wa zao hilo jijini hapa.

Alisema zao hilo ambalo linalimwa mkoani Dodoma linakua kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ndio maana ameamua kuunda timu hiyo ambayo itawasilisha ripoti wizarani.

Bashe alisema kuwa zao hilo ndio uti wa mgongo wa wakazi wa Dodoma hivyo kuna haja ya kuweka mpango mkakati kwa ajili ya kuinua zao hilo.

"Kamati ya watu 12 itakayoongozwa na Mwenyekiti Gungu Mibavu, kutoka Ofisi ya DPP, Sera na Mipango ambapo wote watafanya utafiti kwa muda wa wiki moja na kuwasilisha ripoti itakayoletwa na kamati hii itatusaidia kujua wakulima wa zabibu wako wangapi? Changamoto za wakulima, wazalishaji na wasindikaji, hivyo itatusaidia katika mikakati yetu," alisema Bashe.

Alisema mkakati mwingine wa serikali ni kufufua mabwawa yote yaliyotengenezwa kwa ajili ya umwagiliaji wa zabibu katika wilaya tatu zinazolima zao hilo ambazo ni Bahi, Chamwino na Dodoma.

Bashe aliwataka wadau wa kilimo hicho kuunda vyama vya ushirika ili kupata fursa kwenye taasisi za fedha.

Naye Mkurugenzi wa Doniya Estate, ambaye ni msindikaji wa zao la zabibu, Catherine Mwambe, alisema kuwa suala la kodi limekuwa kikwazo kikubwa kwa wazalishaji wa mvinyo.

"Kwa siku moja zinakuja taasisi zaidi ya tano kila moja inakuja kuchukua kodi, hata faida hatupati, maana hela yote inaishia kwenye hizo kodi," alisema Mwambe.

Alisema, gharama za uzalishaji ziko juu na soko la zabibu nchini bado na kuiomba serikali kuingilia kati na kuweka mazingira rafiki ya biashara ya zao hilo.



## Huduma CT-SCAN yakosekana Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imekiri kutokuwapo huduma za CT-SCAN katika Hospitali ya Abdallah Mzee Pemba.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Harusi Said Suleiman, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo Paje, Jaku Hashim Ayoub.

Jaku alihoji kuwa kukosekana kwa mashine hiyo kumesababisha wagonjwa kupelekwa Unguja ambako nako pia kifaa hicho kina tatizo na kutaka kujua wizara imechukua hatua gani kuhakikisha kifaa hicho kinarejea kutoa huduma kwa wananchi.

Akijibu Naibu Waziri alisema kuwa kifaa hicho kimeshindwa kufanyakazi kutokana na kuharibika.

Alisema mashine hiyo ilitumika kwa muda mfupi na kuharibika na bado mafundi hawajakamilisha matengenezo.

Alisema hadi sasa wameshatumia dola 25,000 kuifanyia matengenezo mashine hiyo.

Pia alisema serikali kwa sasa inangalia uwezekano wa kununua mashine nyingine ili itoe huduma hiyo.

# Mvua zaathiri mashamba pilipili kichaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Biashara na Viwanda imesema mvua kubwa zilizonyesha zimeathiri mashamba ya pilipili kichaa.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Hafidh Khamis, wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Viti Maalum nafasi za wanawake, Sada Ramadhan Mwenda, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alitaka kujua faida waliyoipata vijana kupitia kilimo hicho.

Alisema licha ya mvua kuathiri kilimo hicho, pia vijana ambao ndio waliokuwa walengwa wa mradi huo wa kilimo cha pilipili wameyatelekeza mashamba hayo.

Alisema vijana walikusanywa na kupewa elimu kuhusu umuhimu na faida watakayopata kupitia kilimo hicho na walionyesha utayari wa uzalishaji wa pilipili na walishiriki katika hatua za awali za uandaaji wa mashamba na upandaji.

Alisema wakati wa upaliliaji wa mashamba, vijana walianza kukatisha mahudhurio, kutofika na vifaa vya kulimia na baadhi yao kutofika kabisa.

"Hali hii iliashiria vijana kutokuwa na utayari wa kuendelea na mradi ipasavyo kwa kuwa mahudhurio yao hayakua mazuri wakati wa upaliliaji," alisema.

Alisema waliyatelekeza mashamba hayo baada ya kudai malipo kabla mavuno hayajapatikana.

Vilevile, alisema kutokana na mvua kubwa zilizosababisha mashamba kujaa maji hasa kijiji cha Panga tupu, Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Aliwataka kutumia fursa ya kilimo hicho kwa kuanzisha vikundi vya udhalishaji kwa kuzalisha pilipili kwa wingi kwa kuwa soko la uhakika lipo.

"Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) watanunua pilipili zote zitakazozalishwa kwa utaratibu uliowekwa," alisema.

Alisema hadi sasa hakuna mavuno yaliyofanywa kutokana na pilipili zilizolimwa kuwa chache.

Alieleza kuwa bado ipo haja viongozi wote ikiwamo wa wilaya, halmashauri na mabaraza ya vijana kushirikiana ili upatikane ufanisi wa mradi huo muhimu na wenye tija kubwa.

Alisema wizara yake itakaa na viongozi wahusika kurekebisha changamoto zilizojitokeza ili zisitokee tena na walengwa wapate mafanikio.

Naye waziri wa wizara hiyo, Balozi Amina Salum Ali, alisema mradi huo bado haujafeli na kuwataka vijana kufanya kazi ili kupata maendeleo.




Mwakilishi wa Viti Maalum (watu wenye ulemavu), Zaina Abdallah Salum (kushoto), akibadilishana mawazo na mwanafunzi Khairat Twalib Twaha (kulia), ambaye ni mwenye ulemavu wa uziwi kutoka Shule ya Mwanakwerekwe F, baada ya kusikiliza hotuba ya kamati ya ustawi wa jamii Wizara ya Elimu katika Baraza la Wawakilishi, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Shein ataka wananchi kuheshimu Tume za Uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wananchi kuheshimu kazi, majukumu na uamuzi wa Tume za Uchaguzi nchini, kwa kuzingatia kuwa taasisi hizo zimeundwa kwa mujibu wa sheria na Katiba za nchi.

Dk. Shein alisema hayo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria, Zanzibar.

Alisema kila mwananchi ana wajibu wa kuhakikisha anaheshimu kazi za vyombo hivyo katika uendeshaji na utoaji wa uamuzi katika masuala yote yanayohusu uchaguzi wa Zanzibar na wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema wananchi wana wajibu wakujiepusha na vitendo vyote vinavyokwenda kinyume na sheria na kanuni zilizowekwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Alisema ni vyema kuhakikisha kwamba kila mwenye sifa na haki ya kushiriki katika uchaguzi huo, anafanya hivyo kwa kuelewa kuwa huo ni msingi muhimu wa kudumisha utawala bora na demokrasia.

Alizitaka taasisi zinazoshughulikia masuala ya uchaguzi pamoja na usalama wa wananchi kufahamu wajibu walionao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo, akibainisha umuhimu wa usalama wawananchi kuwa ndio lengo la serikali.

"Ni vyema ikafahamika kuwa suala la kuendeleza demokrasia na kudumisha hali ya usalama na amani wakati wote ni wajibu wetu wa kikatiba," alisema.

Alisema Zanzibar ina nafasi ya kujifunza njia bora za kuendesha kampeni za uchaguzi kwa kuzingatia hoja, ajenda na mambo muhimu ya maendeleo ya jamii na nchi, kama ilivyobainishwa katika Ilani za Uchaguzi badala ya kutumia mwanya huo kufanya kampeni zenye kuleta mifarakano, chuki na uhasama.

Rais Dk. Shein alisema kuna umuhimu wa kuhakikisha kampeni za uchaguzi haziwagawi watu kutokana na rangi zao, makabila yao, dini au miji na vijiji walivyotoka. Akigusia kaulimbiu ya maadhimisho hayo isemayo "Dumisha Utawala wa Sheria na Demokrasia katika uchaguzi mkuu 2020," Dk. Shein alisema suala la kuendeleza demokrasia na kudumisha hali ya usalama na amani wakati wote ni wajibu wa kikatiba.

Alisema Serikali ya Zanzibar imetunga Sheria ya Uchaguzi Namba 4 ya 2018, ikiwa ni juhudi za kukuza na kudumisha demokrasia na utawala bora pamoja na kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Alisema sheria zimeeleza taratibu zinazopaswa kuchukuliwa pale wananchi wasiporidhika na hatua zilizochukuliwa na moja ya taasisi zinazoshughulikia mchakato wa uchaguzi.

"Iwapo mtu hukuridhika na uamuzi wa Tume ya Uchaguzi anaweza kupeleka shauri lake mahakamani kwa uamuzi," alisema.

Alieleza kuwa uamuzi wowote utakaokwenda kinyume na taratibu zilizowekwa na sheria, zitasababisha zogo na kuanzisha fujo na hivyo kuwa chanzo cha watu kugombana na hatimaye kupigana.

Alisema serikali haitasita kuchukulia hatua za kisheria dhidi ya watu wote watakaobainika kuhusika na matukio ya aina hiyo.

Dk. Shein alisema kila nchi duniani ina mfumo wake wa utawala na demokrasia na taratibu zakuendesha uchaguzi, ikiwamo namna ya kuwapata viongozi wa kushika nyadhifa tofauti serikalini.

"Watanzania tuna mfumo wa demokrasia unaokidhi hali ya usalama na mazingira yetu na ndio maana sio sahihi na sio halali, si haki na haifai kwa taifa jingine kuingilia mfumo na taratibu halali za uchaguzi wa nchi yetu zilizowekwa na Tume ya Uchaguzi," alisema.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuzingatia jukumu kubwa la kuwatumikia na kuwasimamia wanachama na wafuasi wao kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora.

"Si vyema chama cha siasa kushutumu kukosekana kwa misingi ya demokrasia katika chama kingine na taasisi nyingine wakati hali hiyo ni mbaya zaidi ndani ya chama kinacholalamika," alisema.

Dk. Shein alisema kuwa demokrasia ya kweli inahitajika ndani ya uongozi wa vyama vya siasa kwa kuweka misingi bora ya kuendesha chaguzi za viongozi, kutoa fursa za uongozi kwa watu wenye uwezo pamoja na kujiepusha na hatua za kung'ang'ania madaraka.

Alisema wakati taifa likijiandaa na uchaguzi mkuu ujao, ana imani kubwa na vyombo vya sheria kusisitiza umuhimu wa kutekeleza vyema majukumu yao kwa uadilifu na haki.

Alisema serikali itaendelea kuhakikisha hali ya amani na utulivu nchini inaendelea kudumu na kuwakumbusha wananchi jukumu la kuimarisha utawala wa sheria pamoja na kulinda usalama.

Akigusia uhuru wa mahakama, Dk. Shein alisema katika kipindi chote akiwa madarakani hajawahi kuweka azma ya kuingilia uhuru wa chombo hicho, kwakutambua kuwa ndio nguzo na mhimili wa utawala usiopaswa kuingiliwa.

Naye Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alisema kwa vipindi tofauti uchaguzi wa Zanzibar umekuwa na ushindani mkubwa wa kisiasa na kusisitiza umuhimu wa jamii kuendelea kulinda amani iliopo.

# DED akoshwa na ununuzi wa trekta sekondari

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashsuri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Changwa Mkwazu, ameipongeza Shule ya Sekondari ya Wavulana Ndanda kwa kununua trekta ikitumia fedha za mapato yake ndani.

Ununuzi huo umegharimu Sh. milioni 53.5, ukilenga kuboresha kilimo katika shule hiyo na kujiongezea mapato.

Mkurugenzi huyo alitoa pongezi hizo jana kwenye hafla ya fupi ya kupokea na kukabidhi rasmi trekta hilo, akieleza kuwa shule hiyo inapaswa kuigwa na shule zingine.

Alisema ni jambo la fahari kuona shule ikinunua zana za kilimo kama trekta kwa kutumia mapato yake ya ndani.

Mkwazu alisema jambo hilo linapaswa kuwa la mfano kwa shule zingine za halmashauri hiyo.

"Huu ni mfano wa kuigwa kwa shule zingine kwani mmeweza kununua trekta hili kwa fedha zenu za mapato ya ndani na siyo mkopo, hivyo mtaongeza mapato ya shule pamoja na kuwafanya wanafunzi kushiriki kazi zingine za maendeleo badala ya elimu ya darasani pekee, hongereni sana," alipongeza.

Akisoma taarifa kwa mgeni rasmi katika hafla ya kukabidhiwa trekta hilo, Mkuu wa Shule hiyo, Morega Mongate, alisema shule ilifikia uamuzi wa kununua trekta hilo ikiamini ni chombo kitakachoongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ikizingatia ina ekari 60 za kilimo.

"Uzalishaji ukiongezeka shule itakuwa na uhakika wa chakula kwa wanafunzi kwani kuna wakati bei za vyakula zinapanda hivyo uzalishaji ukiwa mkubwa ndani ya shule kutakuwa na uhakika wa upatikanaji chakula kwa muda wote shuleni hapa," alisema.

Mongate alisema shule inatoa elimu ya darasani na ya kujitegemea kwa wanafunzi, ikiwamo ufugaji wa kisasa wa kuku, ng'ombe, kilimo na shughuli zingine ili baada ya kumaliza shule, wajiajiri na kuajiri wenzao.

# Wajijengea shule kunusuru watoto wao

**Na Neema Emmanuel,** UKEREWE

WANANCHI wa Kisiwa cha Kweru Mtondogo kilichopo wilayani Ukerewe Mkoa wa Mwanza, wameamua kujenga shule ya msingi ili kunusuru maisha ya watoto wao waliokuwa wakivuka maji kwenda ng'ambo ya pili kuifuata elimu kwa kutumia mitumbwi.

Akizungumza wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Cornel Magembe, alisema Shule ya Msingi Shikizi ilijengwa kwa usimamizi wa polisi, baada ya kuibuka kundi la watu wakidai eneo hilo kuna makaburi ya babu zao, lengo likiwa ni kukwamisha harakati za ujenzi wa shule hiyo.

Alisema kipindi cha nyuma watoto walikuwa wakipanda mitumbwi kuifuata elimu kisiwa jirani, jambo ambalo lilisababisha watoto kupata adha mbalimbali, hivyo wananchi waliungana na kujenga vyumba vinne vya madarasa, ofisi moja na matundu ya choo mawili.

"Shule hii ni mradi uliogharimu Sh. 33,000,000 ukiwamo mchango wa mkurugenzi, mchango wa wananchi na Benki ya NMB na mfuko wa jimbo ukitolewa na mbunge wa mifuko 193 ya saruji," alisema Magembe.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, George Nyamaha, alisema kuwa lengo la wananchi wa kisiwa hicho kuwa ni kuboresha elimu, na kwamba wapo tayari kukamilisha ujenzi kwa mifuko 193 iliyotolewa na mbunge ili kupatiwa usajili.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliwapongeza kwa maendeleo hayo kwani kuna maeneo ambayo yanawakazi wengi, lakini hawana hamasa ya kujenga shule, hivyo alimwagiza ofisa elimu kuharakisha usajili wa shule hiyo ili kuwanusuru na adha hiyo, na kuahidi kuchangia bati 100 ili kuunga mkono juhudi za wananchi hao.

"Kuna maeneo watu ni wengi, lakini wanashindwa hata kujenga shule, ujenzi kwao ni ugomvi na mabishano... wananchi wote wangekuwa kama wakazi wa kisiwa hiki tungekuwa mbali sana kimaendeleo," alisema Mongella na kuahidi kuwa atafuatilia madarasa mawili yaliyosalia pamoja na ujenzi wa choo ili shule hiyo ipatiwe usajili kamili.

Ofisa Elimu Mkoa wa Mwanza, Michael Ligola, alisema shule hiyo inatakiwa kusajiliwa ili kuwanusuru watoto hao, hivyo wajitahidi kumalizia madarasa mawili na matundu ya vyoo ili kukidhi vigezo na kwamba baada ya hapo watawapitisha wakaguzi ili shule hiyo isajiliwe.




Mkurugenzi wa Bima wa Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (kushoto), akisalimiana na Balozi wa Heshima wa Zanzibar katika Shirikisho la Jamhuri ya Brazil, Abdulsamad Abdulrahim, wakati wa warsha ya wanawake na vijana wajasiriamali kuhusu masuala ya uchumi iliyoandaliwa na kampuni ya GS1 na kudhaminiwa na Benki ya NBC jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu Kanisa la Mennonite Tanzania, Askofu Nelson Kisare. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yakabidhiwa hospitali ya Maweni

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imekabidhiwa rasmi Hospitali ya Rufani ya Mkoa Maweni, iliyoko mkoani hapa.

Akikabidhiwa hospitali hiyo jana, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema anaishukuru sekretarieti ya mkoa kwa kuisimamia hospitali pamoja na watumishi katika kipindi hicho, hivyo kuwezesha wananchi kupata huduma zinazostahili.

"Pamoja na makadhibiano tutaendelea kushirikiana kwa ukaribu na ofisi yako RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) na bado utaendelea kuwasimamia watumishi hawa kwani wapo mkoani kwako," alisema.

Aidha, Dk. Chaula alisema wizara imetengeneza mkataba kati yake na RAS katika eneo la usimamizi hasa ya majengo ili yabaki kwenye uimara unaohitajika.

"Tunawashukuru watendaji wa ofisi ya Katibu Tawala kwa kazi nzuri waliyoifanya ya usimamizi wa hospitali hii hadi sasa tunakabidhiana. Tutakwenda kuzisoma nyaraka hizi moja baada ya nyingine, maana ni mali za serikali. Mmetueleza kuna madeni, tutayapitia na kuyafanyia kazi," alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchatta, alisema ataendelea kushirikiana kwa karibu na watumishi wa hospitali hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao ili wananchi wapate huduma bora.

"Watumishi sisi bado ni wamoja. Tutashirikiana bega kwa bega ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma zilizo bora," alisema.

Wakati huo huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Osmond Dyegula, alisema hospitali hiyo ina watumishi 233 n a kwa wastani wanaona wagonjwa kati ya 300 na 330 kwa siku kutokana na takwimu za mwaka 2018/19.

Wizara ya Afya imekabidhiwa hospitali hiyo ikiwa ni agizo la Rais John Magufuli kuhamishia usimamizi huo Wizara ya Afya mwaka 2017 kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi).

## HABARI KIMATAIFA

## Rais Kenyatta M/kiti Umoja wa Marais Afrika

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Marais wa Afrika wanaopambana na malaria ujulikanao kama African Leaders Malaria Alliance (ALMA).

ALMA ni Umoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali walioungana pamoja katika kuongeza juhudi za kutoa elimu na kutafuta fedha, ili kusaidia kupambana na kuutokomeza ugonjwa wa malaria ndani ya bara la Afrika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na ALMA, Kenyatta alikabidhiwa rasmi uenyekiti wa umoja huo juzi jijini Addis Ababa Ethiopia.

Kenyatta anakuwa mwenyekiti wa saba wa umoja huo na atashikilia kiti hicho kwa mhula mmoja wa miaka miwili kuanzia Februari 2020 mpaka Februari 2022.Anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Mfalme Mswati III wa Eswatini.

"Ninayo heshima kubwa kupata nafasi kuwa mwenyekiti wa ALMA. Tayari kuna mafanikio makubwa kwenye mapambano dhidi ya malaria, japo tumerudi nyuma kidogo katika miaka ya hivi karibuni. Tunapoingia kwenye muongo wa kumaliza kabisa ugonjwa huu, ninayo nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunayaendeleza mafanikio tuliyokwisha yapata ili kutokomeza kabisa malaria," alisema Rais Kenyatta na kuongeza:

"Jambo kubwa kabisa kwenye ajenda ya Afrika ya mwaka 2063: ni kuona kwamba tunakuwa na Afrika yenye watu wenye afya njema, wachapa kazi watakaosaidia kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya jamii."

## Maambukizi ya corona China, Japan yaongezeka

**BEIJING,** China

IDADI ya watu walioambukizwa virusi vya Corona hadi jana imepanda na kufikia 44,635 nchini China, huku Japan ikiripoti matukio 174 ambayo ni idadi kubwa zaidi ya maambukizi ya virusi hivyo nje ya China.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Afya ya China, matukio 97 yameripotiwa katika muda wa saa 24 zilizopita na kupandisha idadi ya vifo vilivyotokana na virusi vya Corona hadi kufikia watu 1,113.

**Wakati huo huo**, Wizara ya Afya ya Japan imethibitisha kuwa zaidi ya watu 39 waliokuwa ndani ya meli ya kifahari iliyozuiliwa kwenye pwani ya mji wa Yokohama wamegundulika kuwa na virusi vya Corona. Meli hiyo iitwayo ´Diamond Princess´ iliwekwa kwenye karantini kwa muda wa wiki moja ikiwa na maelfu ya abiria na wale waliothibitika kuwa na virusi vya Corona wameondolewa na kupelekwa hospitali. **DW**

# Uhuru Kenyatta, Ruto, Raila wanena mazito maziko Moi

**NAKURU,** Kenya

RAIS wa awamu ya pili wa Kenya Hayati Daniel arap Moi, alizikwa jana, baada ya jeshi kutoa heshima kwa kupigiwa mizinga 19, huku wanasiasa wakimmiminia sifa.

Maofisa wa kijeshi walitoa heshima kwa kufyatua mizinga lilipo kaburi eneo la Kabarak. Ndege za kijeshi ziliruka kutoa heshima kwa Hayati Moi.

Tofauti na mtangulizi wake Mzee Kenyatta, ambaye alipata heshima ya mizinga 21, Mzee Moi alipigiwa heshima ya mizinga 19 kwa kuwa alifariki akiwa tayari ameondoka madarakani.

Mizinga ilifyatuliwa kwa mpangilio wa kila dakika tatu. Moi alizikwa kijijini kwake karibu na kaburi la marehemu mkewe Lena aliyeaga dunia mwaka 2004.

Mwili wa Moi uliondoka katika chumba cha kuhifadhia maiti cha Lee Funeral jijini Nairobi saa moja asubuhi, huku msafara wake ukielekea katika uwanja wa ndege wa Wilson ambapo uliwasili nyumbani kwake huko Kabarak muda wa saa mbili na dakika 40.

Mwili huo uliosafirishwa kwa kutumia ndege ya kijeshi uliwasili na kufunikwa na bendera ya Kenya. Ulisindikizwa na msafara wa magari ya polisi, maofisa wa jeshi na familia ya Mzee Moi.

**Nakumbuka nilipopigiwa simu ya kwanza nikamwambia mke wangu ashike, ya pili ilipopigwa mke wangu akakataa kushika kwa sababu alijua moto uliokuwapo.**

### Rais Uhuru Kenyatta

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta kwa upande wake, alisema kwamba anampatia kwaheri mtu aliyemtaja kama baba yake.

Uhuru anasema kwamba Moi alimlea hadi alivyo sasa akisema kwamba alikuwa mwalimu wake na mshauri wake mkuu maisha yake yote. Amesema kwamba alijifunza siasa kutoka kwa mzee Moi.

Alisema kwamba kiongozi huyo alikuwa mkali na wakati mmoja alilazimika kujificha kwa muda baada ya kumtaka kukutana naye.

"Nakumbuka nilipopigiwa simu ya kwanza nikamwambia mke wangu ashike, ya pili ilipopigwa mke wangu akakataa kushika kwa sababu alijua moto uliokuwapo. Nilishika simu nikasomewa na nikaambiwa nifike Kabarak katika kipindi cha saa moja. Nilijua kile ambacho kilikuwa kinanisubiri hivyo basi niliamua kujificha. lakini baadaye niliomba msamaha na akanisamehe," alisema Rais Uhuru Kenya.

Aliwataka Wakenya kuiga maisha ya Mzee Moi katika kila walichokuwa wakikifanya kila siku.

### William Ruto

Naibu wa Rais, William Ruto, alisema kwamba licha ya kwamba Moi hakuwaza yeye na viongozi wengine waliofanikiwa pakubwa kutokana na ulezi wa kisiasa wa Rais mstaafu Moi, anamshukuru kiongozi huyo kwa manufaa ya uongozi aliowaletea Wakenya.

Alisema Moi alipenda sana elimu hivyo basi akatoa elimu kwa Wakenya wote bila ubaguzi.

"Tunajivunia wasomi katika mataifa mengi ya kigeni wanaotuletea fedha za kigeni kutokana na elimu bora iliotolewa na Moi wakati wa uongozi wake," alisema kiongozi huyo. Alimsifu Rais huyo mstaafu kwa kuleta amani Afrika na duniani kwa jumla kupitia kupelekwa walinda amani katika mataifa mbalimbali.

Alisema Moi alikuwa na chama thabiti kilichomsaidia kuunganisha makabila tofauti ili kuleta umoja nchini Kenya.

### Raila Odinga

Aliyekuwa Waziri Mkuu nchini Kenya, Raila Odinga, alisema Moi alikuwa mti mkuu uliowaacha wengi wakiyumba baada ya kifo chake.

Amesema ni kutokana na hilo kwamba Wakenya wanafaa kusherehekea maisha yake. **BBC**



Umati ulioshuhudiwa nje ya Chuo Kikuu cha Kabarak huko Baringo, Kaunti ya Nakuru katika maziko ya Rais mstaafu wa Kenya, Daniel arap Moi, jana. **PICHA: BBC**

# Serikali ya Sudan kumkabidhi Bashir ICC

**KHARTOUM,** Sudan

SERIKALI ya Sudan na makundi ya waasi wamekusudia kumkabidhi aliyekuwa rais wa taifa hilo, Omar al-Bashir kwa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita mjini The Hague, Uholanzi .

Uamuzi huo ulifikiwa katika mji wa Juba na kukubaliana kwamba Omar Bashir na wenzake wafikishwe katika mahakama ya kimataifa ya uhalifu wa kivita ICC, ambao wamekuwa wakitafutwa na mahakama hiyo.

Hayo yameelezwa na waziri wa habari wa Sudan, Faisal Saleh wakati akizungumza na waandishi wa habari juzi.

Bashir ambaye aliondolewa madarakani na jeshi mwaka jana kutokana na maandamano ya umma, anasakwa na ICC kwa mashitaka ya uhalifu dhidi ya binadamu na mauaji ya halaiki yaliyohusiana na mgogoro wa Darfur. Tangu kuangushwa kwake Aprili, mwaka jana, Bashir amekuwa kizuizini mjini Khartoum, kwa mashitaka ya ufisadi na mauaji ya waandamanaji.

Mahakama ya The Hague ICC imemfungulia mashtaka kiongozi huyo wa zamani wa Sudan pamoja na wasaidizi wake wa zamani watatu kwa makosa ya mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu na uhalifu wa kivita katika jimbo la Darfur kufuatia mgogoro wa kikatili uliozuka mwaka 2003.

Uamuzi huo umefikiwa mjini Juba katika mazungumzo yaliyolenga kutafutwa haki na maridhiano katika jimbo la Darfur.

Takriban watu 300,000 waliuawa na mamilioni waliachwa bila makazi ulipozuka mgogoro huo. **DW**

# Raia wakigeni wadaiwa kufanya uhalifu ndani ya Ziwa Victoria

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAVUVI wilayani Ukerewe wamelalamikia kitendo cha kuvamiwa na watu wanaodaiwa kuwa raia wa kigeni kutoka nchi jirani na kuwapora mali zao ikiwamo mitumbwi, nyavu na samaki, hivyo kuhatarisha maisha yao.

Wakitoa malalamiko yao juzi mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alipofanya mkutano wa hadhara katika kisiwa kidogo cha Ryegoba, wavuvi hao walisema hali si shwari ndani ya Ziwa Victoria.

Kwa mujibu wa wavuvi hao, wanakoelekea ni kufilisika kwa kuwa wengi wao wana mitaji inayotokana na mikopo ya benki, hivyo wanaiomba serikali kuwasaidia kupambana na uvamizi huo.

Aidha, wavuvi hao walisema wako tayari kutoa mitumbwi yao kwa ajili ya kufanya doria ziwani, lakini kinachowakwamisha ni ukosefu wa askari.

"Mkuu kiukweli sisi wavuvi tunakumbana na changamoto ya kiusalama katika maeneo yetu ya kazi. Unapokwenda kutupa nyavu kunakuwa hakuna shida, lakini ukifika tu muda wa kwenda kuvuta makokolo, wanajitokeza watu wakiwa na silaha, wanatunyang'anya vitu vyetu na tunashindwa tufanyeje. Inabidi tuwe wapole kwa kuhofia kupoteza maisha yetu," alisema Mahande Mafuru kwa niaba ya wenzake.

Baada ya kusikiliza kero hiyo katika visiwa vya Ryegoba, Sizu, Kwelu Kubwa, Bushengele, Bulazu, Kulaza, Garinzila na Kwelu Mto, Mongella aliwataka wavuvi kuhakikisha wanawaumbua Watanzania ambao wanashirikiana na raia kutoka Kenya, Uganda na Rwanda kufanya unyang'anyi ndani ya ziwa ili hatua kali zichukuliwe.

Mongella alisema vitendo hivyo vinafanywa na watu wa ndani na nje kwa kuwa hakuna mgeni atakayefanya uhalifu pasipo kuwa na wenyeji.

Aidha, Mongella alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Cornel Magembe, kufanya haraka kuandaa namna ya kukabiliana na uhalifu unaolalamikiwa kutokea ndani ya jamii ya wavuvi ili kumaliza tatizo hilo.

"Suala la uvamizi unaojitokeza kwa wavuvi wetu halitokubalika. Serikali ya awamu ya tano inataka kuona kila mwananchi anayejishughulisha na kazi yoyote anakuwa huru na mwenye amani. DC (Mkuu wa Wilaya) na kamati yako ya ulinzi na usalama mtajua nini cha kufanya ili kuwalinda watu hawa kwa kushirikiana nao," alisema Mongella.

Mongella yuko ziarani katika Wilaya ya Ukerewe kwa muda wa siku tano, ikiwa ni kuhakikisha ulinzi na usalama kwa wananchi waishio visiwani unaimarika na wanafanya kazi zao kwa amani bila bughudha yoyote.

Naye Magembe alimweleza Mongella kuwa tayari ameishaitisha kikao cha wavuvi wote wa wilaya hiyo kitakachofanyika Februari 19, mwaka huu, ili kuweka mikakati na kuanza doria katika maeneo yote yaliyo ndani ya Ziwa Victoria.



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Meneja Mamlaka ya Maji Mijini na Vijijini (RUWASA), Pascal Kibang'ule (kushoto), alipofanya ziara ya kukagua miradi ya maji ya Mkoa wa Pwani, inayosimamiwa na mamlaka hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ajali ya lori, basi yajeruhi 26

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BASI la abiria la kampuni ya Saibaba, limegongana uso kwa uso na lori aina ya Scania na kusababisha majeruhi 26, kati yao 13 wakielezwa kuwa na hali mbaya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo katika barabara kuu ya Morogoro, eneo la Kongowe wilayani Kibaha.

Nyigesa alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 1:00 asubuhi baada ya lori lenye namba za usajili T.641 DPJ/T 643 DPJ, dereva wake akiwa hajafahamika, likitokea Dar es Salam kwenda Chalinze, kutaka kuyapita magari mengine.

Kamanda Nyigesa alisema lori hilo likiwa katika mwendokasi, lilikutana uso kwa uso na basi la Saibaba lenye namba za usajili T.779 ARW, likiendeshwa na Richard Wilfred, likitokea Sumbawanga kwenda jijini Dar es Salaam.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa lori kuendesha kwa mwendokasi eneo lisiloruhusiwa na kutaka kuyapita magari mengine na kugongana uso kwa uso na basi hilo.

Wankyo alisema hadi sasa hajapata idadi kamili ya abiria waliokuwa kwenye basi hilo na kwamba dereva na utingo wa lori hawajafahamika majina yao kutokana na hali zao.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Rufani ya Mkoa wa Pwani, Tumbi, Dk. Edward Wahi, alithibitisha kupokea majeruhi 26 wa ajali hiyo.

Dk. Wahi alisema kati ya majeruhi hao, watano wamehamishiwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Tawi la Mloganzila, kutokana na hali zao kuwa mbaya kwa kuvunjika baadhi ya viungo.

Pia alisema majeruhi 13 walitibiwa na kuruhusiwa huku wanane wakiendelea na matibabu hospitalini hapo.

# Wafikishwa kortini madai kughushi mkataba

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne wakiwamo wakurugenzi watatu wa kampuni ya Civmark Ltd na Wakili wa Kujitegemea, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka manne ya kughushi mkataba kwa lengo la kupata zabuni ya kujenga barabara katika Manispaa ya Bukoba kwa kiwango cha lami.

Washtakiwa hao ni Crispin Mwombeki na Hadija Nyumbwe wanaodaiwa kuwa ni mke na mume, Joseph Nyamwero na Wakili Glory Benne.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Akiwasomea mashtaka hayo, Wakili wa Serikali, Adolf Lema, alidai kuwa Septemba 17, 2017 jijini Dar es Salaam, Mwombeki na Nyamwero kwa nia ya kudanganya, walighushi mkataba wa makubaliano ya pamoja kuonyesha kuwa kampuni mbili za Civmark Ltd na Mecco Ltd zimekubaliana kuunda mkataba huo kwa jina la Cvmark Mecco Jv kwa lengo la kupata zabuni ya kujenga barabara ya Rubya-Kanyamabogo.

Katika shtaka lingine, ilidaiwa kuwa Septemba 20, 2017 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Mwombeki, Nyumbwe na Benne kwa nia ya kudanganya, walighushi nguvu ya uwakilishi wa kisheria kuonyesha kampuni hizo zimekubaliana kutoa nguvu ya uwakilishi wa kisheria kwa Nyamwero kuwawakilisha kwenye zabuni hiyo.

Pia alidai kuwa Oktoba 10, 2017 maeneo ya Bukoba mkoani Kagera, Mwombeki alighushi nyaraka kuonyesha kampuni ya Mecco imekubali kutoa nguvu ya uwakilishi wa kisheria kwa Nyamwero kuiwakilisha kampuni katika zabuni ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa tano kwa kiwango cha lami.

Ilidaiwa kuwa Mwombeki akiwa Bukoba mkoani Kagera, alighushi nyaraka akionyesha kuwa kampuni ya Mecco Ltd ina uwezo wa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami wakati akijua si kweli.

Washtakiwa wote walikana mashtaka na upande wa mashtaka ulidai upelelezi bado haujakamilika na kwamba hawana pingamizi na dhamana endapo watakidhi masharti.

Wakili wa Utetezi, Paschal Kamala, aliiomba mahakama hiyo iwape wateja wake masharti nafuu ya dhamana kwa sababu kwa miaka mitatu wamekuwa wakiripoti polisi bila kukosa.

Hakimu Chaungu aliwataka kila mshtakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka serikali za mitaa, nakala ya kitambulisho na kutia saini ahadi ya Sh. milioni tano.

Washtakiwa wote walitimiza masharti na wameachiwa kwa dhamana mpaka Februari 26, mwaka huu, kwa ajili ya kufanya mabadiliko ya hati ya mashtaka.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME NA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA.MWENYE NYUMBA 0757 804 970


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GAUDIOUSE PROSPER MGUSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 725 AQV RAV 4.** Chassis namba **SXA110035888.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No: **9910811116124.**

115627802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 15 YA 2020**

**MARRY CHARLES.......................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**JOHN JOSEPH POLE...................MAREHEMU**

**Kwa: Yeyote anayehusika au mwenye maslahi.**

Kwa kuwa mdai ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hii, kwa hiyo mtu yeyote mwenye maslahi katika maombi ya mirathi tajwa hapo juu anapaswa kuweka pingamizi na kuhudhuria katika mahakama hii ya wilaya binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa kabla au siku ya tarehe 16 mwezi March, 2020 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vilelezo vyote vinavyohusiana na maombi ya mirathi hii.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 12 mwezi February, 2020.

MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATE

KINONDONI

DAR ES SALAAM

115627602

## KUPOTEA KWA KADI

**DIPEN JAGDISH TANNA** anatanagza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Mitsubish Fuso yenye usajili wa namba T281 BHT iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania .

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **TAN/TAN/RB/134430/2020**

215627702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**UASIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKANG'WA CHAMWINO**
**Usimamizi wa MRATHI No.3/2020**

Ombi la AVELDA JOSEPH MAEDA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu JACKSON LINDILAEL SHANSI

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII NA MWENYE PINGAMIZI LOLOTE

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 3/04/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

215627202

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT SAMORA AVENUE**
**CIVIL CASE NO. 82/2018**
**MOHAMMED AMOUR**
**VERSUS**
**MASUDI M. KATIMULE**

**TO: MASUDI M. KATIMULE**
**P.O BOX DAR ES SALAAM.**

**TAKE NOTICE** that the plaintiff has instituted a suit against you with particulars of claim set out in plaint filed in this court.

You are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or an agent duly authorized on 27 February 2020 at 8:30 a.m. when this suit will be mentioned.

**TAKE FURTHER NOTICE** that should you default to enter appearance in Court on the day time mentioned above, the suit will proceed and judgment may given in your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 20 day of January 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

115626802

## KUPOTEA KWA KADI

**JIAXING JIANG** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **T/CRUISER** yenye usajili wa namba **T367 DEW** iliyotolewa na Mamlaka ya mapatao Tanzania.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KJN/RB/130321/2020**

115627002

## KUPOTEA KWA VYETI



115626902

**MWINYIMBEGU CHAMOSI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0182-0048** kilichotolewa na **AL-FAROUQ SEMINARY** November, 2001. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0351-0539** kilichotolewa na BAGAMOYO SEKONDARI May, 2004. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DR/KIJ/RB/135556/2020.**


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe kila*

*siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DEMBELE NJE MIEZI SITA BARCA




**BARCELONA,** Hispania

OUSMANE Dembele atakuwa nje ya dimba kwa takribani miezi sita baada ya kufanyiwa operesheni ya misuli ya nyama za paja, Barcelona imethibitisha.

Mchezaji huyo raia wa Ufaransa atakikosa kipindi chote cha msimu kilichobaki na hakuna uhakika kama ataweza kurudi haraka kuichezea timu yake ya taifa katika michuano ya Euro 2020, ambayo inaanza Juni mwaka huu.

Barca ilithibitisha Februari 6 kwamba Dembele alikuwa anatarajiwa kufanyiwa upasuaji nchini Finland katika mguu wake wa kulia.

Baada ya kufanyiwa upasuaji huo Jumanne, Barca inamtarajia mchezaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund kurudi dimbani Agosti mwaka huu.

Dembele amekuwa akisumbuliwa na majeruhi ya mara kwa mara hapo Barca tangu atue Camp Nou kwa ada ya awali ya euro milioni 105 Agosti mwaka 2017.

Msimu huu amecheza mechi tisa tu katika mashindano yote, huku mchezo wa mwisho ukiwa dhidi ya Dortmund Novemba 27.

Majeraha hayo yatamsababisha kukosa kuichezea Ufaransa kwenye michuano ya Euro 2020.

Dembele alikuwa akicheza mara kwa mara kwa mabingwa hao wa Dunia tangu alipoanza kuwacheza kwa mara ya kwanza mwaka 2016, lakini hataweza kucheza kwenye michuano ya Ulaya.

# Adebayor ajiunga Olimpia ya Brazil

**LONDON,** England

EMMANUEL Adebayor amejiunga na mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester City, Roque Santa Cruz katika timu ya Olimpia, na Yaya Toure pia akihusishwa na klabu hiyo na Amerika Kusini.

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid, Arsenal na Tottenham mwenye umri wa miaka 35, alijiunga na timu hiyo na kukutana na Santa Cruz ambaye alicheza naye pale Uwanja wa Etihad kati ya mwaka 2009 na 2010.

Rais wa Olimpia, Marco Trovato alisema Ijumaa iliyopita kwamba alitaka wanachama wapya 20,000 kwa ajili ya kutangaza ujio wa Adebayor Jumatatu kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili.

Muda mfupi baada ya kuwasili wanachama 14,922 walijiandikisha kwa klabu hiyo na kumkaribisha rasmi mchezaji huyo wa zamani wa Togo.

Toure anaweza kuwa mchezaji mwingine mkongwe anayetarajia kwenda Amerika Kusini.

Toure, ambaye alitua City akitokea Barcelona mwaka 2010 na kutwaa mataji ya Ligi Kuu ya England mara tatu, mwaka 2019 alikuwa akicheza soka nchini China katika klabu ya Qingdao Huanghai na sasa anaonekana yupo kwenye rada za klabu hiyo ya nchini Brazil.






# PSG haina uharaka kupona kwa Neymar

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain haitakuwa na haraka na kupona kwa Neymar, kocha Thomas Tuchel amesisitiza.

Nyota huyo alikosa mechi ya PSG ya ushindi wa 2-1 dhidi ya Nantes na ushindi wa 4-2 dhidi ya Lyon wiki iliyopita baada ya kuumia mbavu kwenye mchezo wa Februari Mosi. Alirudi kwenye mazoezi Ijumaa iliyopita, lakini Tuchel amesema hatakuwa na haraka ya kumrudisha dimbani.

"Neymar ameumia, tunatakiwa kuwa watulivu," alisema Tuchel. "Tutaamua kama anaweza kucheza baada ya mazoezi."

Tuchel alithibitisha pia Marquinhos amepona jeraha lake la kigimbi, na hivyo anaweza kurudi uwanjani kwenye mchezo wa ligi dhidi ya Amiens Jumamosi ijayo.

Thiago Silva na Bernat nao watarudi dimbani, lakini Presnel Kimpembe na Marco Verratti walioumia kwenye mchezo dhidi ya Lyon watakuwa nje.

HABARI MICHEZO

# Pochettino: Nataka kurudi tena EPL

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino amesema "angependa" kufanya kazi tena kwenye Ligi Kuu ya England huku kocha huyo wa zamani wa Tottenham akiendelea kuhusishwa na Manchester United.

Pochettino aliiongoza Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, lakini alifukuzwa Novemba na nafasi yake kuchukuliwa na Jose Mourinho.

Barcelona walionekana kuwa na nafasi ya kumchukua Pochettino kabla ya mabingwa hao wa LaLiga kumchukua Quique Setien.

Pochettino ameripotiwa kwamba anatakiwa na United kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer ambaye amekuwa na wakati mgumu pale kwenye dimba la Old Trafford, ambapo 'Mashetani Wekundu' hao wapo nafasi ya nane na wakipitwa pointi sita kwenye mbio za nne bora.

"Kiukweli kabisa, ningependa kufanya kazi kwenye Ligi Kuu," alisema Pochettino akiwaambia waandishi wa habari.

"Itakuwa ngumu, najua na kwa sasa ni wakati wa kusubiri na kuona nini kitatokea.

"Ni wakati wa kujirekebisha, kufikiria kuhusu wewe mwenyewe kidogo na kuwa tayari kwa sababu kwenye soka kitu chochote kinaweza kutokea na unatakiwa kuwa tayari.

"Niko tayari na nasubiria changamoto mpya. Nina imani na najiamini kwamba changamoto ijayo itakuwa nzuri zaidi."

Pochettino aliongeza: "Nilikuwa nchini Argentina, nilikuwa Qatar, nilikuwa Hispania na nilikuwa na Jesus (Perez, msaidizi wa Pochettino pale Spurs) ambaye anafuatilia kila aina ya habari."






# KLOPP ATAJIWA MBAPPE LIVER

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa zamani wa Liverpool, Danny Murphy amemtaka kocha wa timu hiyo Jurgen Klopp kumbadili Roberto Firmino na Kylian Mbappe ili kukifanya kikosi chake kutisha zaidi.

Liverpool kwa msimu huu imekuwa kwenye moto kweli kweli, ikishusha tu vichapo, ambapo kwenye mechi 25 ilizocheza Ligi Kuu England imeshinda mara 24 na kutoka sare moja tu, huku wakiweka pengo la pointi 22 kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Wametinga pia kwenye hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo msimu uliopita walibeba taji lao la sita kwenye michuano hiyo, huku wakiwa kwenye raundi ya tano ya Kombe la FA.

Firmino mwenye umri wa miaka 28, amekuwa sehemu ya mafanikio ya Liverpool, akitengeneza 'upatina' mzuri kwenye safu ya ushambuliaji sambamba na Sadio Mane na Mohamed Salah, lakini Murphy anamtaka Mbappe Anfield kuchukua nafasi yake.

Nyota huyo wa Brazil alihusishwa na mpango wa kwenda Bayern Munich kwenye dirisha lililopita la majira ya kiangazi na Murphy anasema kama hilo litafanyika mwisho mwa msimu, basi Liverpool wakubali na wazibe pengo lake kwa kumchukua Mbappe.

"Kuna mshambuliaji mwingine utampata ambaye atafunga mabao mengi kama Firmino? Ndio," alisema Murphy.

"Firmino amekuwa mchezaji mzuri kwenye mfumo wa kiuchezaji wa Liverpool hasa kwa namna mawinga wawili wanavyocheza.

"Lakini ni jambo la kawaida, hata Kevin Keegan alipoondoka, Kenny Dalglish akaja. Luis Suarez alipoondoka akaja Sadio Mane, Mohamed Salah na Firmino. Firmino anapendwa, kama ilivyokuwa kwa Suarez.

# *Fifa kuwalipa wachezaji wa klabu zilizofilisika*


**GENEVA,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka Duniani (Fifa), na chama cha umoja wa wachezaji wa kulipwa, wanaandaa mfuko utakaosaidia kuwalipa wachezaji wasio na mishahara na wale ambao hawapati mishahara pindi klabu zao zinapopitia changamoto za kiuchumi.

Hiyo imekuja kufuatia mwendelezo wa klabu nyingi duniani kuporomoka kiuchumi, ambapo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, jumla ya klabu 20 duniani zimeanguka kiuchumi na kukwamisha mamia ya wachezaji.

Mfuko huo utazisaidia kulipa mishahara klabu zilizoporomoka kiuchumi huku zikiwa zinafanya biashara ili zirejee katika hali yake.

Rais wa Fifa, Gianni Infantino amesema ametenga kiasi cha pauni milioni 12.3 kwa ajili ya kuwasaidia wachezaji ambao hawatalipwa na klabu zao kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2022 huku takriban pauni milioni 3.8 zikitengwa kuwalipa wachezaji ambao hawajalipwa kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# COUTINHO AITOLEA UDENDA LIVERPOOL

**Inapaa, lakini pia sishangazwi kwa sababu ya kikosi chao kizuri na kocha...**

**MUNICH,** Ujerumani

PHILIPPE Coutinho hashangazwi na kuona klabu yake ya zamani ya Liverpool inatawala Ligi Kuu England, lakini amesisitiza hawezi "kutazama nyuma" licha ya kupitia wakati mgumu tangu ameondoka Anfield.

**Coutinho aliondoka Liverpool na kujiunga na Barcelona Januari 2018 katika usajili uliogharimu euro milioni 160 (pauni milioni 142), lakini baada ya mwanzoni kuvutia hapo Camp Nou, alishindwa kushawishi katika msimu wake mzima wa kwanza LaLiga na kisha akaruhusiwa kuondoka kwenda kujiunga na Bayern Munich kwa mkopo, ambayo pia ina kipengele kinachoiruhusu kumnunua jumla.**

Pia amekuwa akipitia wakati mgumu Bundesliga, hata hivyo, ameanza mechi 12 tu kati ya 21.

Bayern tayari imeamua haitatumia kipengele chake cha kumnunua jumla, ambacho kiliripotiwa kuwa euro milioni 120.

Wakati Coutinho amekuwa akihaha baada ya kuondoka Liverpool, 'Wekundu' hao wameendelea kuimarika kila uchao na wanakaribia kuongeza ubingwa wa Ligi Kuu kutoka ule wa Ligi ya Mabingwa Ulaya waliotwaa msimu uliopita, lakini Mbrazil huyo amesisitiza mawazo yake ni furaha tu kwa klabu yake hiyo ya zamani.

"Liverpool inapaa, na hainishangazi," Coutinho aliliambia Jarida la Sports Illustrated. "Tayari tulishaliona hilo mwaka jana wakati walipotwaa Ligi ya Mabingwa, lakini sishangazwi kwa sababu ya kikosi chao kizuri na kocha.

"Ni mwenye furaha sana, kwa sababu nina marafiki wengi sana pale, wachezaji wenzangu wa zamani, hivyo ni mwenye furaha sana kwao. Lakini hivyo ndivyo ilivyo. Siwezi kutazama nyuma.

"Ninatazama njia nyingine, na sasa nipo katika safari nyingine, zaidi kama ilivyo kwa yeyote yule. Nimejikita kabisa kama wao, kufikia ndoto zangu.

"Ni mwenye furaha kwa kile nilichofanya siku zilizopita, na sasa ninaweza kutazama mbele pekee."

Licha ya masuala ya Coutinho hapo Bayern, Hansi Flick, ambaye yupo anakiongoza kikosi hicho hadi mwishoni mwa msimu hivi karibuni alitoa maneno ya kumfariji, nyota huyo wa kimataifa wa Brazil ambaye amekuwa akivutiwa na kocha msaidizi wa zamani, Niko Kovac.

"Yeye [Flick] anafanya kazi sana, na shukrani kwake timu inacheza vizuri na hicho ndicho kitu cha muhimu," aliongeza.

"Haiwezi kuwa rahisi kuiongoza timu kama Bayern Munich, na ninadhani amekuja na amekuwa akifanya kazi nzuri."

Kufuatia sare tasa waliyoipata Jumapili dhidi ya RB Leipzig, Bayern imeendelea kuwa mbele kwa pointi moja dhidi ya kikosi hicho cha Julian Nagelsmann katika mbio za ubingwa wa Bundesliga.

## ZISIKUPITE

### UTD KWA GREALISH, MADDISON

MANCHESTER United inapanga kutumia pauni milioni 160 kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish, 24, na yule wa Leicester City, James Maddison, 23, majira haya ya joto. ***(Sun)***

### JICHO KWA UPAMECANO

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho alikuwa miongoni mwa waliotazama mechi ya sare tasa kati ya Bayern Munich na RB Leipzig Jumapili, wakati huu beki wa Leipzig, Mfaransa Dayot Upamecano, 21, akiwa mmoja wa wachezaji anayevutiwa naye. ***(Mirror)***

### ARSENAL YAMFUATILIA GUEYE

ARSENAL inamfuatilia kiungo Mfaransa Pape Gueye, 21, ambaye anacheza Ligue 2 katika Klabu ya Le Havre, mkatakati huo ukiwa ni kuelekea dirisha la majira ya joto. ***(Mail)***

### SANCHO LULU UTD, CHELSEA

MANCHESTER United inapanga kuipiku Chelsea katika vita ya dau la pauni milioni 120 kumnasa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19. ***(Mirror)***

### VAN DIJK KUONGEZWA MZIGO

LIVERPOOL inajiandaa kumpa ofa ya mkataba mpya beki Mholanzi Virgil van Dijk, 28, ambayo itamfanya alipwe pauni 150,000 kwa wiki. ***(Football Insider)***

### DEMBELE ANUKIA UNITED

MANCHESTER United inaweza kuruhusiwa kumsajili mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Moussa Dembele, 23, katika majira ya joto. ***(L'Equipe, via Manchester Evening News)***

### AKE AANDALIWA DAU SPURS

TOTTENHAM inaandaa pauni milioni 40 ili kujaribu kutoa ofa kwa beki wa kati wa Bournemouth, Nathan Ake, 24, ***(Express)***

### MERTENS AVUTIA VIGOGO EPL

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Ubelgiji Dries Mertens, 32, uwezekano wa kuondoka bure katika majira ya joto umeongezeka- na Chelsea, Manchester United na Arsenal zote zinatolea jicho saini yake. ***(Mail)***

### ZIYECH KUTAZAMWA CHELSEA

CHELSEA itamtazama Mmorocco Hakim Ziyech, 26, kwa kipindi cha msimu kilichobaki baada ya kushindwa kutoa ofa ya kumnunua winga huyo wa Ajax katika dirisha la Januari. ***(Telegraph)***

### VERTONGHEN ATEGWA AJAX

AJAX inazingatia uwezekano wa kwenda kumsajili beki wa Tottenham na Ubelgiji, Jan Vertonghen, katika majira ya joto wakati mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, atakapomaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu. ***(Guardian)***

### LIVER, ATLETICO NA KUMBULLA

MANCHESTER City, Manchester United, Liverpool na Atletico Madrid zote zinavutiwa na beki wa Verona na Albania, Marash Kumbulla, 20. ***(Gazzetta dello Sport, via Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

# Amri atoa sababu Yanga kunusurika

Na Saada Akida

BAADA ya kuwakosakosa Yanga juzi kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Said, amesema kwa sasa anaumiza kichwa kufanyia kazi safu yake ya ushambuliaji kutokana na kukosa umakini hivyo kushindwa kutoa ushindini.

Mbeya City juzi iliihenyesha Yanga hadi timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani kulazimika kusubiri dakika ya 75 ili kupata bao la kusawazisha kupitia kwa winga wao, Mghana Bernard Morrison wakati wakitoka sare ya bao 1-1.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Amri alisema kitendo cha washambuliaji wake kutokuwa makini katika nafasi za kufunga wanazopata zinamfanya awe na kazi kubwa ya kufanyia marekebisho katika eneo hilo.

Alisema ana imani ya kujinusuru katika nafasi waliyopo sasa na ili wasishuke daraja lazima wapambane kuhakikisha wanapata ushindi kwa kila mechi na hali hiyo inawabidi kuwa makini hasa katika safu yake ya ushambuliaji.

"Safu ya ushambuliaji bado ina shida kidogo, hivyo nitafanyia kazi kwa sababu wote tumeona mchezo wetu na Yanga, tumekosa nafasi nyingi za wazi hii inatokana na kutokuwa makini kwa washambuliaji," alisema.

Amri alisema washambuliaji wake wangekuwa makini anaamini katika mchezo huo wangeondoka na pointi tatu muhimu na kuzidi kupanda juu na hatimaye kujinasua katika nafasi ya kushuka daraja.

Mbeya City ambayo Jumamosi itakuwa ugenini kuvaana na Ruvu Shooting hadi sasa imeshuka dimbani mara 21 na kushinda mechi tatu pekee huku ikipoteza michezo tisa kutoa sare tisa na kujikusanyia pointi 18 ambazo zinaifanya kukalia nafasi ya 18 katika msimamo wa ligi hiyo.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (wa pili kushoto), akitoa msaada wa vyakula kwa Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hashimu Mgandwila (wa pili kulia). SportPesa ambao ni wadhamini wa Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, hivi karibuni ilitoa msaada huo kwa ajili ya kusaidia familia takriban 100 zilizoathirika na mafuriko. **NA MPIGAPICHA WETU**

# KOCHA AZAM ADAI MOJA MOJA SI HABA LIGI KUU

Na Saada Akida

KOCHA msaidizi wa Azam FC, Idd Nassor 'Cheche' amesema ushindi wa bao moja, kila mechi kwa upande wao ni muhimu kwa kuwa wao wanaangalia zaidi pointi tatu katika kila mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Kauli ya kocha huyo imekuja baada ya kushinda bao 1-0 katika mchezo wao dhidi ya Polisi Tanzania uliochezwa juzi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na Nipashe jana, Cheche alisema malengo yao ni kupata pointi muhimu katika kila mechi na suala la idadi ya mabao watalifikiria hapo baadaye.

Alisema wanatambua umuhimu wa idadi kubwa ya mabao, lakini kwa sasa wanachoangalia ni pointi muhimu ambazo zinawaweka katika mazingira mazuri ya kutwaa taji hilo ambalo lipo mikononi mwa mabingwa watetezi, Simba waliopo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakiwa na alama 53.

"Huu ni mzunguko wa pili ni mgumu sana kwani kila timu imefanya maboresho yake kwa ajili ya kujinasua katika suala la kushuka, hivyo unapopata nafasi ya kufunga bao moja, linasaidia kupata pointi.

"Ushindi huu wa bao moja unatuongezea pointi na kusonga mbele zaidi, licha ya ukweli kwamba kufunga idadi kubwa ya mabao ni jambo zuri kwa ajili ya kuweka akiba hapo baadaye pale timu zitakapofungana kwa pointi," alisema.

Cheche alisema ushindani mkubwa wa ligi uliopo kwa sasa, benchi lao la ufundi lipo makini kufanyia kazi mapungufu yanayojitokeza yasijirudie katika michezo yao ijayo husus an Jumamosi wiki hii watakapoikaribisha Coastal Union ya Tanga katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Matokeo hayo yanaifanya Azam kuzidi kujiimarisha katika nafasi ya pili ya msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na alama 44 baada ya mechi 21 huku Polisi Tanzania ambao Ijumaa watakuwa wageni wa KMC FC wakibaki na pointi zao 30.



Wananchi wa Kijiji cha Mazingara Nkumba wilayani Handeni, Tanga, wakiangalia mechi kati ya Simba na JKT Tanzania iliyoisha kwa Simba kufungwa bao 1 -0 wiki iliyopita, katika banda la makuti. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Wawa: Hakuna kulala hadi ubingwa*

Na Mwandishi Wetu

HUKU akiwa mmoja wa wachezaji wa Simba walioonyesha kiwango cha kuvutia wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro juzi, beki kisiki wa timu hiyo, Pascal Wawa, amesema kasi hiyo itaendelea hadi watakapotwaa ubingwa.

Wawa alifanya kazi kubwa ya kuzima mashambulizi ya Mtibwa Sugar kwa kufuta makosa yaliyokuwa yakifanywa na beki mwenzake wa kati, Mbrazil Tairone Santos katika mchezo huo.

Wachezaji wa Simba pamoja na benchi lao la ufundi walitupiwa lawama kubwa kutokana na kupoteza mechi iliyopita dhidi ya JKT Tanzania, hatua ambayo juzi iliwaamsha na kucheza soka la kuvutia lililozima kelele za mashabiki wao.

Akizungumza na Nipashe juzi, Wawa alisema soka walilolionyesha pamoja na wachezaji wenzake watahakikisha wanaendelea kwa kiwango hicho hadi watakapotwaa ubingwa msimu huu.

"Si katika mchezo huu pekee, bali kila mchezaji anaelewa malengo tulizojiwekea ya kutwaa ubingwa, hivyo tutaendelea kucheza kwa ari ya kusaka ushindi hadi malengo yetu yatimie," alisema beki huyo.

Alisema benchi la ufundi linaendelea kufanyia kazi makosa yanayojitokeza katika kila mchezo jambo ambalo linawafanya kuimarika katika kila mechi.

Simba ambayo Jumamosi itakuwa ugenini katika Uwanja wa Samora mjini Iringa kuvaana na Lipuli FC, ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 53 baada ya mechi 21 ilizocheza hadi sasa, wakati Mtibwa ambayo nayo imecheza idadi kama hiyo ya mechi, imebaki na alama zake 23 katika nafasi ya 14.

# Michezo

Alhamisi Februari 13, 2020

Nipashe




Coutinho aitolea udenda Liver

UKURASA 30

HUFUNGI...



Kipa wa Mbeya City, Haroun Mandanda, akijipanga kumkabili mshambuliaji wa Yanga, David Molinga, asizione nyavu kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa juzi na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sven akubali mfumo Kagere, Bocco mbele

●●● Achambua muziki utakavyokuwa sasa huku Katwila akitaja sababu kipigo ni...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, kuweka wazi kwamba chanzo cha kupoteza juzi ni kutokana na wapinzani wao kuwa wazuri eneo la katikati, Mbelgiji wa Simba, Sven Vandenbroeck amekiri washambuliaji wawili mbele walichangia ushindi wao wa mabao 3-0 pamoja na ari kubwa kutoka kwa kikosi kizima.

**Sven kwa muda mrefu amekuwa akilalamikiwa na mashabiki wa timu hiyo kwa kukumbatia mfumo wake wa mshambuliaji mmoja mbele, jambo ambalo wanadai linatoa nafasi kwa mabeki wa timu pinzani kucheza kwa uhuru zaidi na kuwapa mwanya wa kusukuma mashambulizi mbele.**

Hata hivyo, kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa JKT Tanzania Ijumaa iliyopita, kilimuamsha Sven na juzi dhidi ya Mtibwa kulazimika kuanza na washambuliaji wawili mbele, Meddie Kagere na John Bocco, hatua iliyosaidia kwenda mapumziko wakiwa wanaongoza 1-0.

Bao hilo likifungwa na Bocco kwa ushirikiano mzuri na Kagere na kiungo Clatous Chama kabla ya kipindi cha pili Mohamed Hussen 'Tshabalala' na Hassan Dilunga 'HD' kuongeza mawili, hivyo kushinda kwa 3-0. Baada ya mechi hiyo, Katwila alisema wapinzani wao walikuwa bora zaidi eneo la katikati, hivyo kuharibu mipango yao na kisha kutumia mwanya huo kusukuma mashambulizi mbele na kufanikiwa kuwaadhibu.

"Simba walikuwa bora zaidi katikati, jambo lililoharibu mipango yetu na kusababisha kushambuliwa zaidi, nimeyaona makosa yaliyofanyika na nitakwenda kuyafanyia kazi kabla ya mechi ijayo [dhidi ya JKT Tanzania]," alisema.

Lakini Sven licha ya kuwapongeza wachezaji wake kwa ari kubwa ya ushindi waliyoionyesha mwanzo mwisho wa mchezo huo wa juzi, Nipashe lilipomuuliza anauonaje mfumo wa washambuliaji wawili mbele alikiri kufanya kazi vizuri.

"Ni kweli wamecheza vizuri na umeonekana kutupa matokeo, lakini kwa ujumla timu nzima imecheza vizuri na wachezaji walikuwa na ari ya ushindi mwanzo mwisho wa mchezo.

"Itakapolazimu tutakuwa tukibadilisha mfumo kutokana na aina ya mechi na ninatumai ari hii kwa wachezaji itaendelea pia katika mechi nyingine," alisema kocha huyo aliyerithi mikoba ya Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems huku akiongeza.

"Kwa ujumla matokeo mazuri ni kitu tulichokuwa tunakihitaji, hata wachezaji pia walikuwa wanalitambua hilo, kujituma kwao na juhudi zao ndio mafanikio yetu."

Simba ambayo imeshuka dimbani mara 21 hadi sasa ikiwa kileleni na alama 53, Jumamosi itakuwa ugenini katika Uwanja wa Samora kuvaana na Lipuli FC iliyopo nafasi ya tisa na alama zake 29 baada ya kucheza idadi ya mechi kama hizo za mabingwa hao watetezi.

# Eymael alilia ratiba Yanga

**Na Saada Akida**

PAMOJA na Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, kulalamikia mwenendo wa ratiba, amesema ana uhakika mkubwa wa timu yake kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu kutokana na mabadiliko makubwa yanayoonekana katika kikosi chake.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Luc alisema wana ratiba ngumu kwao kwa sababu wanacheza mechi zaidi ya tisa katika mwezi mmoja, hivyo watapambana kuhakikisha wanapata pointi kwenye kila mchezo ili kufikia malengo yao.

Alisema kutokana na ugumu wa ratiba yao na wachezaji kuchoka atahakikisha kikosi chake kitakuwa na mabadiliko ya mara kwa mara lengo likiwa ni kutafuta pointi muhimu ambazo zitawafanya kutwaa taji la ligi hiyo linaloshikiliwa na watani zao, Simba waliopo kileleni wakiwa na alama 53 baada ya mechi 21 ikiwa ni alama 15 zaidi ya Yanga yenye michezo miwili mkononi.

"Licha ya ratiba kuwa changamoto kwetu, kikubwa ambacho nakiona kwenye timu yangu imebadilika kwa kiwango kikubwa na kadiri siku zinavyo kwenda ndiyo inazidi kuwa bora, naamini nafasi ya ubingwa tunayo tena kubwa.

"Hatupaswi kutishwa na anayeongoza ligi, kubwa ni kuendelea kupigana kuona kwanza tunawapita wapinzani wetu ili kuweza kufikia ubingwa kitu ambacho bado kipo kwenye uwezo wetu," alisema huku akilalamika kuwa wachezaji wake si maroboti, kutokana na ugumu wa ratiba ambayo inawafanya kucheza kila baada ya siku tatu .

Yanga ilicheza Alhamisi iliyopita kisha Jumamosi wakacheza tena na juzi Jumanne walicheza na Mbeya City katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam timu hizo kutoka sare ya bao 1-1, sasa itashuka tena dimbani Jumamosi kuikaribisha Tanzania Prisons.



9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042